Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 10 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2003/2004.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA (k.n.y. MHE. JOHN S. MALECELA – MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 200

**Nchi Zilizofutiwa Madeni kwa Njia ya HIPC**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali yetu imefanikiwa kuingia katika kundi la nchi chache zilizoingia kwenye *HIPC* na hivyo kufutiwa madeni:-

(a) Je, Tanzania ilikuwa inadaiwa kiasi gani cha fedha kabla ya kufutiwa madeni hayo, kwa madeni ya *Paris Club* na wadai wengine?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho hadi sasa kimeshasamehewa katika madeni hayo; na katika madeni yaliyosamehewa fedha hizo zimeelekezwa katika sekta zipi ikionyesha kiasi cha fedha kwa kila sekta?

(c) Je, deni la Taifa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2002 ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania iliingia katika Mpango wa *HIPC* Aprili, 2000. Wakati huo kwa takwimu za mwezi Juni, 2000, Serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 5,816.8 sawa na *USD* milioni 7,276 milioni. Kati ya deni hilo, shilingi bilioni 1,712.44 ni za kundi la *Paris Club* na shilingi bilioni 875.73 lilikuwa deni la kundi lisilo la *Paris* na shilingi bilioni 2,855.27 la Taasisi za Kimataifa. Wakati ilipofikia *completion point* mwezi Novemba 2001, Serikali ilikuwa na deni la jumla ya *USD* bilioni 6,186.8. Kati ya hizo, deni la kundi la *Paris* lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,547.3, madeni ya kundi lisilo la *Paris* *USD* milioni 926, *USD* milioni 3,514.8, Asasi za Kimataifa na *USD* milioni 197.7 ni madeni ya kibiashara.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili, 2003 jumla ya shilingi bilioni 897.5 zimekwishasamehewa. Kati ya fedha hizo Dola za Kimarekani milioni 675.5 ni kutoka Kundi la *Paris,* Dola milioni 184.4 toka Asasi za Kimataifa na Dola milioni 37.7 kutoka China.

Mheshimiwa Spika, msamaha huo wa madeni unahusu madeni yatakayopevuka kwa kipindi kirefu. Madeni yaliyopevuka katika vipindi husika na kusamehewa ndiyo yaliyopelekea kuwepo kwa fedha za Bajeti za kuboresha huduma za jamii , barabara, kilimo, Mahakama na Ukimwi kama Serikali ilivyokubaliana na wafadhili. Hivyo, fedha zilizookolewa kutokana na msamaha wa madeni hayo hadi hivi sasa zimeelekezwa katika sekta nilizozitaja. Fedha hizo zimesaidia sana kuongeza mgao wa fedha za matumizi katika sekta hizo kama ilivyoonyeshwa katika Bajeti ya miaka ya 2001/2002 na 2002/2003 na katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004.

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya deni la Taifa la ndani na la nje hadi kufikia Desemba 31, 2002 lilikuwa shilingi bilioni 8,005 ambazo ni sawa na Dola za

Kimarekani milioni 8,199.3. Kati ya deni hilo shilingi bilioni 6,591.3 ni la nje na shilingi bilioni 1,413.7 ni la ndani.

**SPIKA:** Kabla hujauliza swali la nyongeza ninataka kueleza Waheshimiwa Wabunge kwamba Hati kwa utaratibu wetu ikishawasilishwa mezani inakuwa sasa ni *public document* yaani inaweza kusomwa na kila mtu. Kwa hiyo, kuanzia leo baada ya kuwasilisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri mezani, hotuba zinagawiwa moja kwa moja kwa Waheshimiwa Wabunge ndiyo kazi inayofanyika hivi sasa. *(Makofi)*

Pili, kabla hatujaendelea napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge, kwamba tunao ugeni wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Waheshimiwa Wawakilishi watano wako kwenye *Gallery* leo wanasikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa madhumuni makubwa ya nchi tajiri kutupunguzia madeni ni kuwezesha nchi zetu kuweza kujitegemea na kuondokana na mzigo wa madeni. Kutokana na takwimu alizozitoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, hivi sasa inaonyesha bado nchi yetu ina deni kubwa hata kabla ya pale ambapo tulikuwa bado hatujasamehewa madeni. Je, atakubaliana nami kwamba bado mkakati wa kupunguza mzigo wa madeni kwa nchi yetu huu mpango wa *HIPC* bado haujatusaidia.?

(b) Kwa kuwa bado Bajeti yetu ni tegemezi kwa asilimia isiyopungua 47. Je, Serikali na kwa kuwa madeni hayo yanakua, ina mpango gani wa kuhakikishia kwamba tunaondokana na Bajeti tegemezi hasa ukilinganisha bado deni letu limekuwa kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, msamaha wa madeni tulioupata umetusaidia sana kama nilivyoeleza katika jibu la msingi na kinachoangaliwa hapa siyo ukubwa wa deni bali ni uwezo wa uchumi wetu kulipa deni hilo. Kinachoangaliwa ni kitu kinachoitwa *debt sustainability ratio* ambacho ni uwezo wa uchumi wetu kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, madeni yaliyosamehewa yanapevuka kila mwaka. Tumesamehewa jumla ya bilioni za Kimarekani 3 katika kipindi cha miaka 20. Kwa hiyo, yanapopevuka ndipo tunaposamehewa na tunayaingiza kwenye Bajeti.

La pili, Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ni kweli ni tegemezi na katika hotuba ya ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna mikakati ambayo imeelezewa kwenye Bajeti ya mwaka huu ya kupunguza utegemezi huo, na nia yetu kwamba utegemezi huo utaendelea kupungua kadri uchumi wetu unavyoimarika.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa

Fedha kuhusu deni tulilonalo sasa hivi tunalipa wastani wa shilingi ngapi kwa mwezi na kama kuna deni ambalo tumeshindwa kulipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama unazo hizo takwimu. Endelea kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kuna madeni ya aina tatu. Kwanza, kuna madeni baina ya nchi na nchi na pili kuna madeni ya Taasisi za Kimataifa, na mwisho kuna madeni ya kibiashara na madeni hayo nimeyaeleza kiasi gani tunadaiwa kwa kila nchi. Kuna takwimu ambazo ninazo hapa Mheshimiwa Mbunge akizihitaji nitaweza kumpa.

Na. 201

**Biashara katika Bandari ya Zanzibar**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo habari kwamba utaratibu mzima ulioboreshwa wa kuteremsha kontena kwa wafanyabiashara Tanzania Bara umesababisha wafanyabiashara kuihama Bandari ya Zanzibar hivyo kusababisha uchumi wa Tanzania Zanzibar kushuka kwa kasi:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

(b) Je, kuna tofauti gani katika ulipaji Kodi wa *TRA* Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar wakati *TRA* ni moja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwapo na ongezeko la ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam kufuatia marekebisho yaliyofanywa katika uendeshaji wa bandari hiyo. Hata hivyo, mafanikio hayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na upunguaji wa idadi ya wafanyabiashara wanaotumia bandari ya Zanzibar. Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa uchumi wa Zanzibar unaendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.7 kuanzia mwaka 1992 hadi 2001.

Kufuatana na tafiti mbalimbali zilizokwishafanyika, sababu moja kuu iliyosababisha wafanyabiashara kupunguza kutumia Bandari ya Zanzibar ni kuwepo kwa uoanisha wa viwango vya kodi kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Utaratibu huo umepelekea wafanyabiashara kutoona umuhimu wa kupitishia

bidhaa zao nyingi Zanzibar baada ya kuona kuwa tofauti iliyokuwepo ya viwango vya kodi imeondolewa.

Awali viwango vya kodi vilikuwa vya chini kwa upande wa Tanzania Zanzibar ukilinganisha na Tanzania Bara. Hata hivyo, tafiti nyingine zimeainisha pia kuwepo kwa mapungufu katika huduma za usafirishaji na utoaji wa mizigo ikiwa ni sababu nyingine muhimu ya upunguaji wa mizigo katika Bandari ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haiamini kuwa uchumi wa Zanzibar unashuka katika miaka ya hivi karibuni kutokana na takwimu zifuatazo ambazo zinaonyesha ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kuanzia mwaka 1994 mpaka mwaka 2001. Mwaka 1994 uchumi ulikuwa unakua kwa asilimia 0.3 na ulikua kufikia kiwango kikubwa mwaka 1996 ambapo ukuaji ulikuwa asilimia 7.1, ulishuka mpaka asilimia 0.5 mwaka 1998. Lakini mwaka 2002 ulikua hadi kwa kiwango cha asilimia 5.6.

Mheshimiwa Spika, aidha, si kweli kwamba kuboreka kwa bandari za Tanzania Bara kumesababisha uchumi wa Tanzania Zanzibar kuzorota.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna tofauti yoyote ya viwango vya ushuru vinavyotumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar hivi sasa, isipokuwa ada ya ukaguzi wa mizigo *(Pre-shipment Inspection Fees)* ambayo hutozwa kwa bidhaa zinazoingizwa Tanzania Bara lakini haitozwi kwa bidhaa zinazoingizwa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hakuna tofauti yoyote katika ukusanyaji wa kodi unaofanywa na *TRA* kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa *TRA* inatumia kanuni na taratibu zinazofanana kwa pande zote za Muungano.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa uchumi wa Zanzibar unategeme sana zao moja tu la Karafu na Bandari. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi kuboresha shughuli za Zanzibar ili kuweza kukuza uchumi wake kwa hali yoyote ile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona ni kama swali jipya. Hilo ni swali jipya Mheshimiwa Naibu Waziri hana majibu yake sasa hivi.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri aliyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ameelezea kwamba *TRA* haina tofauti katika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Je, kwa nini hao wafanyabiashara wote sasa hivi wamehamia Bandari ya Tanga?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wana hiari ya kuchagua bandari yoyote wanayopenda. Kwa sababu Bandari ya Dar es Salaam kuna bidhaa nyingi zinazoingia, kwa hiyo, kuna wafanyabiashara wanachagua bandari ya Tanga ambayo haina bidhaa nyingi zaidi ukilinganisha na Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna wafanyabiashara wengine wanapitishia Bandari nyingine kama Mombasa. Kwa mfano, wafanyabiashara wa Mkoa wa Kagera, wanapitishia bidhaa zao Mombasa. Kwa hiyo, kinachoangaliwa hapa siyo kwamba labda kuna gharama kubwa katika Bandari ya Zanzibar ama katika Bandari ya Dar es Salaam ni *convenience* na matashi ya wafanyabiashara wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hatuna takwimu kwa sasa zinazoonyesha kwamba wafanyabiashara wote wa Zanzibar wamehamia katika Bandari ya Tanga.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, lakini haoni kwamba wafanyabiashara wanaopitishia bidhaa zao katika Bandari ya Tanga wanapata unafuu ndiyo maana wanafanya hivyo na kuna sababu kubwa wanaipata huko ndiyo maana Bandari ya Dar es Salaam inashindwa kuvuka yale malengo na Bandari ya Tanga inavuka malengo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba kuna njia fulani wanayoifuatia huko? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi taratibu na kanuni zinazotumika ziko sawa kwa Bandari zote. Kwa hiyo, kama wafanyabiashara wanakwenda Tanga siyo kwa kufuata kitu ambacho kiko Tanga, lakini katika Bandari ya Dar es Salaam hakipo. Sana sana ni upungufu wa bidhaa na uharaka wa mizigo na pengine wanateremshia mizigo yao katika Bandari ya Tanga kwa sababu ni karibu na Pemba na kwa hiyo inakuwa rahisi kusafirisha mizigo kuipeleka huko.

Na. 202

**Msongamano wa Mahabusu Magerezani**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa zaidi ya nusu ya watu walioko magerezani ni mahabusu ambao wanangojea kesi zao kusikilizwa; na kwa kuwa kuwepo kwao magerezani kwa muda mrefu kunafanya gharama za uendeshaji wa magereza kuwa kubwa sana.

Je, Serikali haiwezi kuangalia uwezekano wa kuweka muda maalum, mathalani miaka mitatu hadi minne ya mtu kukaa rumande na baada ya hapo kuachiliwa chini ya kifungu fulani cha sheria kitakachoiwezesha Serikali kumkamata tena endapo upelelezi utakapokuwa umekamilika kwa lengo la kupunguza

msongamano mkubwa wa mahabusu na gharama kubwa zisizo za lazima za uendeshaji wa magereza hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wapo mahabusu wengi magerezani wanaosuburi kesi zao kusikilizwa. Hata hivyo, idadi yao sio zaidi ya nusu ya waliopo magerezani kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, bali ni kiasi cha asilimia 40 ingawa nacho tunakiri kwamba bado ni kiwango kikubwa. Tatizo la kuchelewa kusikilizwa kwa kesi nyingi zilizopo Mahakamani kunatokana na sababu mbalimbali za msingi hasa ugumu wa kukamilisha haraka upelelezi wa makosa ya jinai hasa yale makosa ya mauaji, kukosekana kwa mashahidi, baadhi ya wahalifu washiriki kutokupatikana mapema kwa kujificha, na upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba yafanywe marekebisho ya sheria kwa nia ya kutoa muda maalum mathalani miaka mitatu au minne ya mtuhumiwa kukaa rumande na baada ya hapo aachiwe ili kupunguza msongamano magerezani, tumeupokea ushauri huo na utafanyiwa kazi na Wizara yangu kwa kushirikisha Wizara ya Sheria na Mambo Katiba na wadau wengine.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Serikali baada ya kukiri mlundikano huo wa mahabusu katika magereza yetu. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba wakati umefika Serikali ilazimishwe kuwepo kwa sheria ya kuwaweka mahabusu nje kwa dhamana isipokuwa kwa wale tu wanaohusika na makosa makubwa kama ya mauaji pamoja na uhaini?

(b) Kwa sababu inavyoonekana kule magerezani kuna mahabusu wamewekwa tu katika mchanganyiko na ni wengi kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri. Ili kupunguza mlundikano huo wa mahabusu kule magerezani. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba labda uwekwe utaratibu wa kuwakutanisha kila siku Mahakama, Magereza na Polisi ili waweza kujionea hali halisi ya mlundikano wa mahabusu kule Magerezani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali limeshaeleweka. Majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi tunakiri kwamba msongamano upo katika magereza yetu tena mkubwa. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria iwekwe

ili watu wapewe dhamana wa makosa mengine kasoro yale makosa makubwa, hiyo sheria ipo. Takribani makosa yote yana dhamana isipokuwa machache sana yakiwemo makosa ya mauaji yale hayana dhamana, makosa ya uhaini hayana dhamana na makosa ya ujambazi kwa kutumia silaha kwa wale wanaoua watu na kuiba, tukiondoa hayo makosa mazito mengine yote yana dhamana.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea nendeni magerezani mtaona wengi dhamana zipo wazi, lakini wanashindwa kuzitumia kwa kukosa mtu wa kumdhamini yaani mtu yuko gerezani kwa kosa ndogo tu, lakini mama yake hataki kumdhamini, baba hataki kumdhamini hata mjomba, kaka, shangazi hawataki kumdhamini hayo ndiyo yanayotokea huko katika magereza. Lakini sheria inatoa fursa ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwakutanisha Mahakimu, Polisi na Magereza huo utaratibu upo. Ipo Kamati inaitwa Kamati ya Kusukuma Kesi, hizi Kamati zipo katika ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati hizi Mahakimu ni wajumbe tena Mahakimu ndiyo Wenyeviti, Polisi ni wajumbe, Magereza ni Wajumbe ile Mikoa ambapo kuna Wanasheria wa Serikali ni Wajumbe na Kamati hizi kazi yao ndiyo hiyo kupitia katika magereza, kutazama kesi zinavyokwenda, hii kesi imekwama wapi ili kusukuma kesi ziende haraka.

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo kuna baadhi ya Mikoa na baadhi ya Wilaya Kamati hazikai kwa kiasi cha kutosha. Ningependa kutumia nafasi hii kutoa wito kwamba Kamati zote za kusukuma kesi za Mikoa na Wilaya zifanye kazi kama inavyotakiwa kusudi zisaidie kupunguza msongamano uliopo magerezani.

**SPIKA:** Naona Waheshimiwa Wabunge saba wanataka kuuliza maswali ya nyongeza. Lakini leo hii tunajadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hiyo, mliyonayo mtayasema wakati wa mjadala.

Na. 203

**Vyuo vya Elimu Rungwe**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Rungwe ina Vyuo vya Elimu viwili vya Tukuyu na Mpuguso, vinavyotoa elimu kwa ngazi ya cheti tu;

Je, Serikali haioni kuwa ni vyema Chuo kimojawapo katika hivyo kikabadilishwa ili kitoe mafunzo katika ngazi ya *Diploma* kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya walimu wa ngazi hiyo ya elimu yaliyotokana na wananchi kuitikia wito wa kujenga shule nyingi za sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali vikiwemo Vyuo 14 ambavyo vinatoa mafunzo ya Stashahada. Vyuo vya Ualimu binafsi vilivyosajiliwa ni 13, vikiwemo 8 vinatoa mafunzo ya Stashahada. Kati ya hivyo vinane, kimoja kipo Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Rungwe ina Vyuo viwili vya Tukuyu na Mpuguso vinavyotoa elimu kwa ngazi ya cheti. Vyuo hivi vinachukua wanachuo Kitaifa kwa kuzingatia mahitaji. Kwa sasa hivi Wizara yangu inaandaa mpango wa kupanua na kuboresha Elimu ya Sekondari nchini. Ni dhahiri katika kufanya hivyo itaangalia upya matumizi bora ya Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu vikiwemo Vyuo vya Ualimu vya Tukuyu na Mpuguso. Chuo cha Ualimu Tukuyu kina nafasi nzuri ya kuchukua majukumu mapya ya kuandaa walimu ngazi ya Stashahada.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa ushauri wake utapewa kipaumbele wakati Wizara yangu itakapoanza kutenga Vyuo vipya vya kutoa Stashahada.

Mheshimiwa Spika, Wizara inahitaji muda wa kufanya maandalizi yakiwemo ya wakufunzi wenye sifa, vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia. Aidha, Wizara yangu inakaribisha wadau wengine kufungua Vyuo vya Ualimu vya Stashahada ili kukidhi mahitaji ya Shule za Sekondari ambayo yataendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, siku mbili zilizopita tumemshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri alizofanya katika kupanua Elimu ya Msingi. Nilitegemea kwamba tunapopanua elimu ya msingi madarasa yanakuwa mazuri na wanafunzi wanakuwa wengi. Nilitegemea kwamba upanuzi wa Elimu ya Walimu pia ungekwenda sambamba. Lakini takwimu alizotupa hazisemi hivyo.

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba hii kwenye *development budget* ya asilimia 15 haoni kwamba Serikali haijaonyesha *seriousness* katika Elimu ya Walimu?

La pili, hivyo Vyuo nilivyovitaja viko katika hali mbaya sana kimajengo na sidhani kama ni Vyuo vya Ualimu vya Rungwe peke yake. Je, ni kazi ya nani kukarabati hayo majengo na kama ni ya Serikali hii shilingi milioni 10,000/= ambayo iko kwenye Bajeti itatosha? Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza katika kupanga Bajeti tunakwenda hatua kwa hatua. Napenda Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba tunatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Katika kutekeleza programu hiyo tuna *roll out* yaani katika kila hatua tunatoa mpango kwa ngazi stahili ya elimu.

Kwa hiyo, kwa makusudi kabisa tuliamua kwamba Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya miaka 5 utahusu ngazi ya *Primary School.* Mpango wa pili, utahusu ngazi ya Sekondari. Mpango wa tatu, utahusu ngazi ya Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutapata nafasi wakati wa *Teacher Education Development Plan (TEDP)* yaani kutoka *Secondary Education Development Plan(SEDP)* tutakwenda kwenye *Teacher Education Development Plan* ambapo tutayazama kwa undani matatizo yote yanayohusu Vyuo vyetu vya Mafunzo ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, pia amesema kwamba Bajeti tunayoweka ya asilimia 15 haitoshi. Napenda kumfahamisha kwamba kwa *resources* za ndani kama alimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha *percentage* inayokwenda kwenye Elimu sasa hivi iko kwenye asilimia 25 siyo asilimia 15, iko kwenye asilimia 25 na pia tunasaidiwa na misaada ya kutoka nje.

Sasa kuhusu hali mbaya ya Vyuo vya Mpuguso na Tukuyu napenda kumhakikishia kwamba wakati tunatayarisha hiyo *Teacher Education Development Plan* tutakuwa na *component* pia ya kuli-*habilitate* vyuo vyote vya Ualimu pamoja na kujenga vyuo vipya pale inapostahili na kuvipanua vingine vilivyopo.

Napenda pia nisahihishe kwamba *enrolment* yaani uandikishaji wa Walimu Tarajali katika vyuo vyetu. Miaka mitatu iliyopita vyuo vilikuwa na wanafunzi 3,000. Mwaka 2002 vilikuwa na wanafunzi karibu 9,000. Mwaka huu Vyuo vya Ualimu kama taarifa nilivyoitoa katika Bajeti zitakuwa na wanafunzi 15,000. Kwa hiyo, tumepanua sana *enrolment* katika Vyuo vya Ualimu ili tuwe na walimu wa kutosheleza mahitaji. *(Makofi)*

Na. 204

**Mpango wa Wizara Maji Safi na Salama**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu umepita tangu mwongozo wa Wizara ulipotolewa kuhusu mpango wake kuwapatia maji safi na salama wananchi wake na Taifa kwa ujumla ifikapo mwaka 2005.

Je, azma hiyo ya Serikali bado ipo au Serikali inatoa kauli gani tena?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa lengo la Serikali ilikuwa ni kuwapatia wananchi wote maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 ifikapo mwaka 2002. Hivi leo ni asilimia 53 ya watu waishio vijijini na asilimia 73 ya watu waishio mijini wanapata huduma ya maji safi na salama. Lengo la mwaka 2002 halikufikiwa kutokana na mahitaji makubwa ya raslimali inayohitajika ukilinganisha na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kwa kifupi hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Bara la Afrika. Inakadiriwa kwamba watu zaidi ya milioni 400 hawana huduma ya maji safi na salama Afrika na karibu ya watu milioni 330 ambao wanaishi vijijini hawana huduma ya maji safi na salama. Katika Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo Endelevu uliofanyika Johanesburg, Afrika ya Kusini, Jumuiya ya Kimataifa ilikubaliana kwamba ifikapo mwaka 2015 idadi ya watu wasio na huduma ya maji safi na salama iwe imepunguzwa kwa asilimia 50. Hii ina maana kwamba ili kufikia malengo haya katika upande wa Afrika inatakiwa kuongeza huduma ya maji safi na salama kwa zaidi ya watu milioni 19 kila mwaka.

Kwa upande wa Tanzania idadi ya watu wasio na huduma ya maji safi na salama wanatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 28.6 hadi milioni 41 waishio vijijini na kutoka milioni 10.4 hadi milioni 13.6 waishio mijini ifikapo mwaka 2015. Hivyo ili kufikia malengo ya milenia na makubaliano ya Mkutano wa Kimataifa ya Maendeleo Endelevu wananchi wapatao milioni 20.7 waishio vijijini na milioni 6.3 waishio mijini nchini wanatakiwa kupatiwa huduma ya maji safi na salama. Pia tunahitajika kuelekeza asilimia isiyopungua 15 ya Bajeti katika matumizi ya maji safi na salama.

Lengo la Serikali la kuwapatia wananchi wote maji safi na salama bado lipo. Juhudi za Serikali zilizopo katika kuwapatia wananchi wote maji safi na salama ni kuendelea kutekeleza programu mbalimbali za maji hapa nchini kwa kuzingatia malengo ya Jumuiya ya Kimataifa na kuwapatia maji safi na salama watu wote duniani.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, amekiri kwamba kweli azma hiyo ya Serikali ni vigumu kuikamilisha kwa mpango ulivyotolewa kwa mwaka 2002. Je, kwa sababu wananchi wanaelewa kwamba Serikali inafanya juhudi ya kutekeleza kupata mahitaji ya maji safi na salama wanaposhindwa Serikali hawaonyeshi kwamba wananchi wanakosa matumaini kama mwongozo inavyotamka kwamba watatekeleza kwa wananchi azma hiyo ya kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, jukumu la kuwapatia wananchi maji safi na salama sio la Serikali peke yake. Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa maeneo mbalimbali nchini ambao wanalielewa hili na wamechangia kwa kiwango kikubwa sana katika upatikanaji wa maji safi na salama kupitia juhudi zao katika kijiji na kupitia mtu mmoja mmoja.

Lakini pili, jukumu la kuwapatia maji safi na salama wananchi kama nilivyoeleza katika jibu la msingi linategemea sana uchumi wa Taifa au upatikanaji wa raslimali. Kwa sababu miradi ya maji inahitaji fedha nyingi na inahitaji nguvu nyingi kuelekezwa huko. Kwa maana hiyo ndiyo maana tulishindwa kufikia kiwango kilichotarajiwa mwaka 2002. Lakini kwa juhudi zilizopo sasa hivi za Serikali na Chama cha Mapinduzi pamoja na wananchi walivyoitikia wito wa kusaidiana nina hakika kwamba kiwango kilichotarajiwa sasa hivi kitaongezeka ili tuweze kukidhi mahitaji ya maji safi na salama hapa nchini.

Na. 205

**Uhaba wa Huduma ya Maji Vijiji na Miji ya Kongwa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa miundombinu ya maji katika Mji wa Kongwa na Miji midogo ya Mlali, Kibaigwa na Mkoka haitoshekezi kutokana na ongezeko kubwa la watu, mifugo na makazi; na kwa kuwa vijiji vingi Wilayani Kongwa vina uhaba mkubwa wa huduma ya maji:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuboresha huduma hiyo ya kusambaza maji katika Miji midogo ya Mlali, Mkoka, Kibaigwa na Kongwa?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kuboresha huduma hiyo ya ujenzi wa mabwawa katika vijiji vya Wilaya ya Kongwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna uhaba mkubwa wa maji katika Wilaya ya Kongwa. Hata hivyo Wilaya hiyo inayo ufadhili wa miradi miwili inayotekelezwa na Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ambayo ni moja Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Miji Midogo unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la *AFD.* Pili, Mradi wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira unaotekelezwa na Serikali kutumia fedha za mkopo nafuu wa Benki ya Dunia.

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika uchunguzi wa kina Serikali inatarajia kuwa Mji Mdogo au Kijiji cha Kibaigwa utakuwa katika miji itakayonufaika na

Mradi wa Miji Midogo unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa. Hivyo kutatua tatizo la maji hivi karibuni.

Kwa kuwa Mradi wa maji Vijijini na Usafi wa Mazingira unaotekelezwa na Serikali kwa mkopo nafuu wa Benki ya Dunia unahusisha miji midogo pia namshauri Mheshimiwa Mbunge kupeleka maombi kupatiwa maji Vijiji vya Mlali, Mkoka na Mamlaka ya Mji Mdogo ya Kongwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ili lijadiliwe na liweze kutekelezwa baada ya kutimiza masharti yanayohusika.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali Kongwa ni Wilaya mojawapo iliyo na bahati kubwa ya kuwa na Mradi wa Maji au Miradi ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira. Nina uhakika Mheshimiwa Mbunge alishiriki katika kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kilichochagua vijiji 10 ya kujiunga na mradi huo katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji. Vijiji vilivyochaguliwa ni Mautya, Kiteto, Manungu, Chamae, Tubugwe, Mbande, Iduo, Masinyeti na Pandambili, Hembahemba na Lenganga. Majina ya Kigogo hayo. *(Makofi)*

Ujenzi wa miradi ya Maji katika vijiji hivi 10 unatarajiwa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka huu 2003. Miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa mabwawa, visima virefu na vifupi katika vijiji nilivyovitaja kutegemea na uchunguzi wa kitaalam utakavyobainisha. Serikali itaendelea kutafuta fedha ndani na nje ya nchi kama ilivyofanya kuboresha huduma maji katika Wilaya ya Kongwa na Wilaya nyingine hapa nchini.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na shukrani kubwa sana za wananchi wa Kongwa kwa Serikali yao kwa jinsi inavyowatazama katika masuala ya maji. Lakini kwa kuwa bado kuna vijiji vingi vina matatizo makubwa sana ya maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Kongwa pamoja na nami ili kuweza kujionea mwenyewe hali ilivyo mbaya?

Swali la pili, kwa kuwa tunasikia ipo teknolojia kubwa ambayo imekuwa *developed* kwenye Wizara ya kuvuna maji ya mvua. Je, mnaweza mkatufikiria Wilaya yetu nayo ikaingia katika taratibu zenu za mradi kama huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa shukrani alizozitoa kwa niaba ya wananchi wake wa jimbo la Kongwa.

Pili, inawezekana Mheshimiwa Mbunge amesahau nilishatembelea Kongwa, nikaona baadhi ya miradi ya maji katika vijiji mbalimbali Wilayani Kongwa.

Tatu, kama nilivyoeleza Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa maji safi na salama sio Wilaya ya Kongwa peke yake lakini mahali pengi

hapa nchini. Hivyo pia namshauri Mheshimiwa Mbunge ajaribu kushawishi Wilaya yake ili waendelee kutenga fedha katika Bajeti za Halmashauri ili kutekeleza baadhi ya miradi midogo midogo ambayo imo ndani ya uwezo wa Wilaya. Sio Wilaya Kongwa tu lakini popote hapa nchini.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umenipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayoshughulikia Maji na Mifugo na kwa kuwa Serikali imepanga Mfuko wa Kuendeleza Mifugo Nchini je, Serikali inaweza ikaeleza ni majukumu gani yatafanywa na mfuko huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya kabisa halihusiani na maji Wilaya ya Kongwa.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nazungumzia Kongwa hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Kongwa na Miji Midogo iliyotajwa katika swali la msingi iko karibu sana na Dodoma; na kwa kuwa Dodoma sasa hivi ina maji mengi kuliko mahitaji kufuatana na matangazo ya *NUWA* katika Redio mpaka inabomoa mabomba. Je, Serikali haioni busara ya kuweka maji haya kuyapelekwa Kongwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli *supply* ya maji kwa Mji wa Dodoma sasa hivi inakidhi karibu asilimia 100 na yanabaki. Lakini Mji wa Kongwa uko zaidi ya kilomita 50 kutoka hapo. Zaidi ya kilomita 50 zinaweza kuwa hata 200 au 300.

Kwa hiyo, kusafirisha maji kutoka hapa kwenda Kongwa itahitaji fedha nyingi sana kitu ambacho kwa kuangalia kwa juu juu ina maana kwamba maji haya yanayopatikana sasa hivi hapa Dodoma yanaweza yasitoshe kwa vile Dodoma inapanuka. Kwa hiyo, italeta matatizo yaliyokuwepo hapo nyuma baada ya muda mfupi. *(Makofi)*

Na. 206

**Mradi wa Umwagiliaji - Kijiji cha Misozwe**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1970 Serikali kupitia uhisani wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China ilianza Ujenzi wa Bwawa kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji katika Kijiji cha Misozwe (kwa sasa Kata ya Misozwe) Jimboni Muheza; na kwa kuwa lengo la mradi huo ni kupunguza umaskini kwa wakazi wa kijiji hicho, lakini mradi

haukukamilika na vifaa vingi vimetekelezwa kwenye eneo la mradi na sasa vinaendelea kuoza:-

(a) Je, ni sababu gani zilizofanya ujenzi wa mradi huo kusitishwa hadi sasa?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha wakati huo kilitumika kutoka kwenye fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo na kiasi kilichobaki kilihifadhiwa wapi?

(c) Je, ni jitihada gani zimefanywa na Serikali kuwahamasisha wahisani wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, Japan au wahisani wengine za kuufufua na kuuendeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kumjibu Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Maji Mashambani la Misozwe uliofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, ulijengwa kati ya mwaka wa 1974 na 1975. Lengo la mradi kwa wakati huo lilikuwa kuendeleza eneo la hekta 60. Aidha, mradi huo ulisitishwa kutokana na upungufu wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, wahisani hawakutuachia hesabu ya fedha walizozitumia. Hata hivyo, mwaka wa 1974/1975, Serikali ilichangia katika kuendeleza mradi huo kwa kumpa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ya Muheza shilingi 357,950/= kwa ajili hiyo. Fedha hizi hazikutosha kuikamilisha mradi na kwa hiyo, hakuna fedha zilizobaki.

(c) Katika mwaka wa 2001/2002 mradi huu ulijumuishwa katika Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani na katika mwaka wa 2003/2004. Wizara inakusudia kuufanyia usanifu na kuandika andiko la kitaalam upya. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inashauriwa kujumuisha mradi huu katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ili utafutiwe fedha za kutekeleza.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa kuhusu swali hili. Lakini pamoja na hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mradi huu ulikwishaanza kutekelezwa na ukasitishwa na kwamba sasa hivi upo mpango wa Kitaifa wa Umwagiliaji maji. Je, ni kwa nini mpango huo usiingizwe katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa Kitaifa wa Umwagiliaji Maji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, huu mradi kamambe sasa hivi ndiyo unachambuliwa na kupewa *priority.* Lakini kwa

utaratibu huu nilioupendekeza wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya fedha zimo kwenye Bajeti. Kwa hivi ili kutatua tatizo hili ni bora wafanye kama nilivyoshauri.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niuliza swali moja la nyongeza.

Katika Mpango mzima wa Serikali kuhimiza Kilimo cha Umwagiliaji ni kwamba kwa vile Halmashauri za Wilaya hazina uwezo katika kutekeleza miradi kama hiyo. Je, iko mikakati ya Serikali kuweza kuzisaidia Halmashauri za Wilaya katika mipango mizima ya kufanyia *feasibility study* katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, wakati wa mwaka huu wa fedha Halmashauri zitakuwa na fedha za kuandaa mipango yao na kuiwasilisha kwenye Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo na hapo tutaweza kutekeleza suala hili kama nilivyoshauri kwa Halmashauri ya Muheza.

Pili, ni kuwa tunatambua kama Halmashauri hazina fedha ndiyo maana tulikaribisha maoni kuwa mlete mapendekezo kutoka huko kwenye Wilaya kusudi tuweze kuunganisha katika Mpango kabambe wa Taifa. *(Makofi)*

Na. 207

**Kuondoa Ruzuku Kwenye Pembejeo**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yaani Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ilikuwa maarufu kwa uzalishaji wa chakula hasa mahindi; na kwa kuwa uzalishaji huo mkubwa ulitokana na matumizi ya kutosha ya mbolea za chumvi chumvi zilizokuwa zikipatikana kwa bei nafuu kutokana na ruzuku ya Serikali kwenye bidhaa hiyo:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba nchi yetu imekuwa haina uhakika wa kujilisha baada ya kuondoa ruzuku katika pembejeo za kilimo?

(b) Je, Serikali inaelewa kuwa kuendelea kuamini kwamba yapo maeneo yasiyohitaji mbolea za kisasa katika kilimo cha kisasa ni kujidanganya?

(c) Je, Serikali iko tayari kupokea maombi ya wakulima wa mikoa hiyo ya kupunguza bei ya mbolea kwa zaidi ya nusu ya bei iliyopo sasa ili waweze kuongeza uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Si kweli kwamba nchi yetu imekuwa haina uhakika wa kujilisha baada ya kuondolewa kwa ruzuku kwenye pembejeo. Kati ya mwaka wa 1990/1991 na mwaka wa 2001/2002 nchi imejitosheleza kwa chakula kwa asilimia kati ya 92 na 102 ya mahitaji yake yote, bali ni kweli kwamba kuondolewa kwa ruzuku kwenye mbolea, kumesababisha kushuka kwa matumizi ya mbolea nchini kwa asilimia 33, kutoka wastani 124,000 kwa mwaka wa 1990/1991 hadi tani 83,000 kwa mwaka wa 1994/1995.

(b) Serikali haiamini kuwa yapo maeneo yasiyohitaji mbolea. Vituo karibu vyote vya utafiti wa udongo viko chini ya Serikali na Serikali inajua kwa uhakika kwamba maeneo mbalimbali ya nchi yanahitaji aina na viwango tofauti vya virutubisho. Mimea huchukua virutubisho kutoka kwenye udongo na baada ya muda husababisha upungufu wa virutubisho hivyo. Ili kilimo kiwe endelevu, inabidi kurudisha virutubisho hivyo kwenye ardhi kwa kutumia mbolea. Serikali ina habari za uhakika juu ya mahitaji ya virutubisho kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na haina sababu za kujidanganya juu ya suala hilo.

(c) Kadri uwezo wa Serikali utakavyoongezeka, ndivyo itakavyojitahidi kuwapatia wakulima mahitaji yao ya kilimo kwa bei nafuu. Hadi sasa Serikali imekwishaondoa kodi karibu zote kwenye pembejeo, zana za kilimo na mauzo ya mazao kwa lengo la kumwezesha mkulima kupata kipato kizuri zaidi. Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali italipa sehemu ya gharama za kusafirisha mbolea kwenda kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Huu ni mwanzo mzuri na kadri mapato ya Serikali yatakavyoongezeka ndivyo ruzuku kwa wakulima itakavyoongezwa.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na juhudi mbalimbali za Serikali na kupunguza kodi mbalimbali katika mbolea lakini katika kipindi cha miaka 10 mbolea imepanda zaidi ya mara ya 20. Sasa swali ni kwamba katika utaratibu huu ambao Serikali itatoa nafuu ya usafirishaji wa mbolea. Je, mkulima yule wa chini wa kijijini atarajie kwa utaratibu huu wa awali kabisa kwamba mbolea hiyo ipungue kwa asilimia ngapi, gharama hiyo ya mbolea ipunguzwe kwa asilimia ngapi?

La pili, kama tulivyosema kwamba mbolea ilikuwa ikipanda kwa kasi kubwa, je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mbolea kwa sababu ni kitu muhimu hakipandi kiholela ndani ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika suala la msingi ni kuwa mbolea kama inavyoagizwa kutoka nje hazisababishi gharama kupanda. Kinachopandisha gharama mara nyingi ni gharama za usafirishaji. Kwa sababu pembejeo zote na mbolea zote hazina kodi. Ndiyo maana

Serikali imechukua jukumu la kuhakikisha kama inasaidia sehemu ya kupunguza gharama za Usafirishaji na kwa kufanya hivyo inatakiwa bei ibakie pale pale au ipungue kwa kiasi kikubwa sana. Lakini tutakavyozidi kufanya kama nilivyosema kadri uwezo wa Serikali utakapokuwa unaongezeka ruzuku itafikiriwa upya.

Na. 208

**Biashara ya Nje**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa biashara ya nje ni ya Muungano:-

(a) Je, ni chombo gani cha Muungano kinachosimamia biashara ya nje?

(b) Je, muundo wake ukoje?

(c) Je, ni matatizo gani yanayokikabili chombo hicho katika kutekeleza kazi zake?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Chombo cha Muuungano kinachoshughulikia Biashara ya Nje ni Halmashauri ya Biashara ya Nje yaani *Board of External Trade (BET).*

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Biashara ya Nje *(BET)* ni Taasisi iliyoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na uendeshaji wa kila siku wa *BET* husimamiwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye husaidiwa na Kurugenzi tatu ambazo ni Idara ya Ukuzaji Masoko, Idara ya Utafiti na Mipango na Idara ya Fedha na Utawala. Usimamiaji wa jumla wa shughuli za *BET* hufanywa na Bodi ya Wakurugenzi. Kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya mwaka 1978 ambayo ndiyo iliyoianzisha *BET,* Bodi ya Wakurugenzi ilitakiwa kuwa na wajumbe 17.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa gharama za kuendesha Bodi ya Wakurugenzi na kutokana na mabadiliko katika miundo ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja na mabadiliko ya mifumo ya baadhi ya Mashirika yaliyotajwa ndani ya sheria; mwaka 1992, Serikali iliamua kupunguza ukubwa wa Bodi ya Wakurugenzi mpaka kufikia wajumbe 8 ambao ni Mwenyekiti

(mfanyabiashara) na wajumbe kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii Zanzibar, *Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA), Confederation of Tanzania Industries (CTI),* Ofisi ya Bunge, Benki ya Taifa ya Biashara na Mkurugenzi Mkuu wa *BET*.

(c) Mheshimiwa Spika, mbali na *BET* kupata mafanikio mengi tangu kuanzishwa kwake pia imekumbana na matatizo kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake. Vile vile tunakumbuka kuwa *BET* iliunguliwa Ofisi zake za Makao Makuu ambazo zilikuwa kwenye jengo la *NASACO* ambapo *BET* ilipoteza vitendea kazi vyake vyote pamoja na nyaraka zake zote muhimu ikiwemo taarifa muhimu kwa wafanyabiashara. Hali hii imeathiri utendaji kazi wa *BET* kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatathmini mapendekezo ya vyanzo vya mapato kwa *BET* na muundo mpya wa *BET* kwa lengo la kuiwezesha *BET* kutoa huduma bora zaidi kwa wafanyabiashara na kuwa chanzo cha ushauri fasaha kwa Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya sasa ya biashara ya ushindani Kimataifa katika mazingira ya utandawazi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Katiba katika mambo ya Muungano *item* 800 ni mambo ya mikopo na biashara za nje ni mambo ya Muungano. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba chombo hiki kinatakiwa kiwe na mfumo wa muundo wa Kimuungano haoni kwa kuishirikisha Wizara ya Biashara na Viwanda peke yake Zanzibar na ukachukua Taasisi nyingi kutoka Tanzania Bara, je, hiki chombo hakina sura ya Kimuungano halisi? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa madhumuni makubwa ya kuanzishwa biashara ya nje kuwa ya Muungano ni kwamba utaratibu wote wa kufanya biashara za nje ziwe za Muungano. Kwa kuwa wakulima wa Karafuu wananyimwa haki ya kusafirisha bidhaa zao kwenda nje na chombo hiki ndiyo kazi zake moja kusimamia. Je, hawaoni kwa kufanya hivyo wanavunja Katiba ya Nchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba Muundo wa Bodi hauelekei Kimuuungano. Kwa sababu tumeshirikisha kabisa na *TCCIA,* ambayo nina hakika kuna wajumbe kutoka Zanzibar, tumeshirikisha vile vile Wizara ya Viwanda, Biashara, Utalii ya Zanzibar ambayo ni Wizara inayohusika na sekta tatu.

Vile vile, ili kuhakikisha kwamba tunatimiza masharti vizuri na kuisaidia Zanzibar kibiashara, tumefungua ofisi ambayo inaitwa *Zanzibar Trade Center,* tumetenga Shilingi 40 milioni na tumechagua Bodi ambayo itakuwa na Wajumbe wote kutoka Zanzibar. Kwa sababu tumekwishawateua, siyo vizuri kuwataja Wajumbe hao hapa na tunasubiri jina la Mwenyekiti litoke kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba, kuanzia Julai 1, *Zanzibar Trade Center* na *BET* watashirikiana kikamilifu na kama kuna marekebisho yoyote ambayo mngependa tufanye, tuko tayari kufanya. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, kwa swali la pili, napenda kujibu kama ifuatavyo, wafanyabiashara wanaouza karafuu kutoka Zanzibar siamini kwamba wamebaguliwa na wameshindwa kupeleka viungo nje! Tulifanya utafiti mwezi wa Agosti, 2002 na tukachukua Wajumbe kutoka Zanzibar tukaenda nao Ujerumani na Amerika na tumepata masoko mengi na makubwa.

Mheshimiwa Spika, tumetembea nchi nyingi sana zikiwemo nchi za *United Arab Emirates, Europe,* Ujerumani, Amerika, Ufaransa na Uingereza, masoko tunayo na wafanyabiashara wa Zanzibar pia tunao. Inasikitisha kuona kwamba mpaka sasa hivi bado hatujaweza kukidhi matakwa ya wale *customers* wetu kutoka huko nje.

Namuomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane naye, labda baada ya *session* hii tutazame uwezekano wa kuhakikisha kwamba tunaweza kutumia hayo masoko ambayo tumekwishafanyia utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Na. 209

**Upungufu wa Mahakimu**

**MHE. RUTH. B. MSAFIRI** aliuliza: -

Kwa kuwa mojawapo ya matatizo makubwa ya Idara ya Mahakama ni upungufu mkubwa wa Mahakimu hasa Mahakama za Mwanzo na kwa kuwa takwimu zinaonyesha upungufu huo ni takriban karibu au sawa na 50% hivi: -

(a) Je, ni mwaka gani Serikali inatarajia inaweza kuondokana na tatizo hilo?

(b) Je, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo anastahili awe na sifa zipi?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo pikipiki kama ilivyofanya kwa Makatibu Tarafa ili kuwawezesha kumudu ipasavyo kazi hiyo ngumu inayowakabili?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Hadi sasa, idadi ya Mahakama za Mwanzo Tanzania Bara ni 1,105. Idadi halisi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanaohitajika ni 2,210. Mahakimu

waliopo ni 722 na kati yao 40 ni wa Mkataba wa miaka miwili. Pengo halisi la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni 1,488.

Mahakama za Mwanzo zinaweza kuondokana na tatizo la uhaba wa Mahakimu baada ya miaka 5 iwapo tutafanikiwa kukipanua Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na pia iwapo Vyuo vingine vya Elimu ya Juu vitaongeza idadi ya wanafunzi wanaochukua Stashahada ya Sheria watakaostahili kuajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

(b) Hapo awali sifa ya mtu kustahili kuajiriwa kama Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ilikuwa ni Cheti cha Sheria. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuimarisha utaalam katika utendaji, sifa hizi zimeboreshwa na hatimaye Mahakimu wote wa Mahakama za Mwanzo wanatakiwa wawe na Stashahada ya Sheria.

(c) Nakubaliana na Mheshimiwa Ruth Msafiri, kuhusu umuhimu wa kuwapa pikipiki Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Tatizo la kutekeleza wazo hilo limekuwa ni uhaba wa fedha. Kwa kuzingatia umuhimu wa vyombo hivyo kwa Mahakimu, Serikali inajitahidi kulipatia ufumbuzi suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Msafiri, swali moja la nyongeza.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kanuni inanipa maswali mawili, naomba niyaulize.

**SPIKA:** Lakini muda unakunyima maswali mawili.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza ulilonïruhusu kwa leo kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwamba baada ya miaka 5 ijayo Chuo cha Lushoto na Vyuo vingine ambavyo hakuvitaja vitakuwa vimeongeza idadi ya ufundishaji, je, ni nani anayetakiwa kuleta maombi hayo ama utaratibu wa kuwezesha Mahakimu hao kuelimishwa na je, katika bajeti hii ameleta maombi hayo?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu na kama nilivyozungumzia katika jibu langu la msingi, kutatua tatizo hili pia itachukua muda mrefu.

Kwanza tumekuwa na tatizo la kupata kibali kutoka Idara ya Utumishi, lakini Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Mary Nagu amenidokezea kwamba, kutokana na unyeti wa Wizara hii na hasa Mahakama, sasa tatizo hili litaondolewa. Kwa hiyo, tutalegezewa masharti ya kutokuajiri na hivyo tutaweza kuajiri Mahakimu wengi zaidi na hali kadhalika tunazungumza na watu mbalimbali, Wafadhili mbalimbali na Taasisi zetu hapa nchini ili kuweza kupanua Chuo hiki cha Lushoto kiweze kutupatia Mahakimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Ruth Msafiri, ana matatizo ya Mahakimu katika Jimbo lake, wapo wachache, lakini napenda kumhakikishia kwamba, waswahili wanasema: "Ajaae kisimani mbele hunywa maji maenge," kwa hiyo, karibu Mheshimiwa Ruth Msafiri. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika, lakini kuna Kamati mbili ambazo zimepanga kukutana leo. Kamati ya Fedha na Uchumi, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Lephy Gembe, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo kwamba, kikao kitakuwa saa 5.00 asubuhi hii katika chumba cha mikutano namba 81.

Kamati nyingine ni ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawatangazia Wajumbe wake wakutane leo saa 6.00 mchana chumba namba 50.

Pia, kuna tangazo moja la sherehe za uzinduzi wa ripoti moja ya *UNDP.* Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Ali Mohammed Shein atazindua rasmi taarifa inayoitwa *The 2003 UNDP Global Human Development Report* na wanaomba Waheshimiwa Wabunge washiriki katika uzinduzi huo na utafanyika katika viwanja vya mashujaa, si mbali kutoka hapa, ni mkabala na Ofisi ya Ujenzi. Muda wa uzinduzi ni baada ya Bunge, ratiba inasema Mheshimiwa Makamu wa Rais atafika kwenye viwanja hivyo saa 7.40. Kwa hiyo, tutakuwa tumekwishaahirisha shughuli zetu. Waheshimiwa Wabunge wale watakaokuwa na nafasi ya kuhudhuria wanakaribishwa.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

## Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
## Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo wa Majimbo 19 uliofanyika tarehe 18 Mei, 2003 pamoja na wenzetu waliorejea tena Bungeni baada ya kushinda kesi zao Mahakamani. Nampongeza pia Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini kwa kuchaguliwa na wenzake kuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Naipongeza pia timu yake ya Wasemaji Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuelezea hoja yangu, napenda kuwashukuru na kuwapa pongezi za dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wa

Fedha, na Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri walizotoa humu Bungeni zenye mwelekeo na dira ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha na miaka inayofuatia katika nyanja za uchumi na jamii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera. Kamati hii iliyapitia na kuyachambua makadirio hayo pamoja na masuala mbalimbali ya Wizara yetu na kuyatolea maoni na maelekezo. Maoni na maelekezo hayo yamenisaidia sana katika kuandaa maudhui ya hotuba hii na pia katika kuchukua hatua mbali mbali za kuongeza ufanisi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaahidi kuyazingatia kwa ujumla wake maelekezo yao yote kwa lengo la kuleta ufanisi na kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani maalum kwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Capt. John Zephania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kwa msaada na ushirikiano wake mkubwa ulionipunguzia muda wa kuielewa na kuizoea Wizara.

Nawashukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Ndugu Bernard Saidi Mchomvu, Inspekta Jenerali wa Polisi; Ndugu Omar Iddi Mahita, Kamishna Mkuu wa Magereza; Ndugu Nicas Banzi, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara zote pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano waliouonyesha katika utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa katika mwaka wa fedha wa 2002/2003. Nawashukuru wote pia kwa msaada wao katika maandalizi ya Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za dhati zimwendee pia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha kwa wakati uchapaji wa kitabu cha Hotuba yangu hata nikaweza kuiwasilisha leo hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina Idara Kuu tano ambazo ni: Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji na Huduma kwa Wakimbizi.

Idara hizi kuu zinasaidiwa na Idara za Utawala na Utumishi, Sera na Mipango na Vitengo vya Uhasibu na Usajili wa Vyama vya Kijamii. Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya iliyokuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hivi sasa imehamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi kabisa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni pamoja na kudumisha amani, utulivu, usalama wa raia na mali zao, hifadhi ya wafungwa na mahabusu (ikiwa ni pamoja na jukumu la kuwarekebisha wafungwa), hifadhi na udhibiti wa wakimbizi na shughuli za uhamiaji. Aidha, Wizara pia inasimamia utekelezaji wa Sera ya Zimamoto na Uokoaji nchini na kuzisimamia Sheria na Kanuni za Zimamoto na Uokoaji. Mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na majanga yatokanayo na moto nayo hutolewa na Wizara hii. Kwa kuzingatia uzito wa majukumu hayo, tunavyo

Vyombo kadhaa ambavyo kwa njia moja au nyingine hushirikiana na Wizara yetu kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia katika maudhui ya bajeti na shabaha na malengo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba nizungumzie angalau kwa ufupi hali ya usalama nchini. Mwaka 2002, yaliripotiwa nchini kote, jumla ya matukio 529,227 ya aina zote, makubwa na madogo. Jedwali Na. 1(a) – (f) zinachambua kwa kina matukio hayo kimkoa na kwa aina.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwelekeo wa uhalifu mkubwa wa jinai kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zinaonyesha kupungua kwa matukio ya uhalifu huo kutoka 82,532 mwaka 1998 hadi 67,371 mwaka 2002. Katika kipindi hicho, kilele cha uhalifu mkubwa kilikuwa mwaka 1999 ambapo yaliripotiwa jumla ya matukio 98,900. Jedwali Na. 2 linatoa uchambuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hali ni tofauti kwa uhalifu mkubwa wa jinai unaohusiana moja kwa moja na ujambazi. Uhalifu wa aina hiyo kama vile unyang'anyi wa kutumia silaha na mauaji unaonyesha mwelekeo wa kuongezeka katika baadhi ya Mikoa hususan Dar es Salaam, Kigoma, Kagera, Shinyanga, Arusha na Mwanza katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, unyang'anyi wa kutumia silaha uliongezeka kutoka matukio 786 mwaka 1998 hadi matukio 1,237 mwaka 2002, kama inavyoonekana katika Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, matukio ya mauaji yaliongezeka kutoka 1,846 mwaka 1998 hadi 2,612 mwaka 2002 kama inavyoonekana katika Jedwali Na.4. Matukio hayo ni pamoja na ujambazi, wizi wa kawaida, imani za uchawi, wivu, ulevi, ugoni, kugombea wanawake/wanaume, kugombea mashamba na kujinyonga.

Mheshimiwa Spika, matukio ya ujambazi huambatana na ukamataji wa silaha. Jedwali Na. 5 linaonyesha mwelekeo wa ukamataji wa silaha toka 1998 hadi 2002.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2002/2003, miongoni mwa matukio makubwa ya ujambazi yaliyoleta mshituko nchini ni wizi wa fedha za Benki ya *CRDB* na kuuawa kwa Askari Polisi watatu na mbwa wao waliokuwa katika doria.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15/ Novemba, 2002, majambazi ambao wote walibainika kuwa raia wa nchi jirani ya Kenya, walivamia Tawi la Azikiwe la Benki ya *CRDB* Mjini Dar es Salaam na kupora fedha jumla ya shilingi 3,147,974,054/=. Watuhumiwa hao wa ujambazi walikamatwa nchini Kenya kutokana na ushirikiano baina ya Polisi wa Kenya na Tanzania. Kwa mujibu wa mkataba wa ushirikiano wa kubadilishana watuhumiwa baina ya nchi zetu mbili, watuhumiwa hao wamerejeshwa nchini kujibu mashitaka yao, na tayari wamefikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25/05/2003 lilitokea tukio kubwa la uhalifu ambapo Askari wetu watatu wa Polisi na mbwa wao waliuawa na majambazi. Mashujaa hao ambao walikuwa katika doria ya kusaka majambazi walishitukizwa na majambazi waliokuwa wamejiandaa huko maeneo ya Kawe, Mjini Dar es Salaam. Tukio hilo la majambazi kuthubutu kuua Askari wengi kama hivyo lilikuwa la aina yake kutokea nchini mwetu na lilileta mshituko mkubwa nchini. Hata hivyo, faraja ilipatikana pale majambazi karibu wote waliohusika katika tukio hilo, ambao wote ni wageni kutoka nchi jirani, walipokamatwa ambapo watano kati yao waliuawa wakati wakijaribu kukataa au kukimbia kukamatwa huku wakiwashambulia Polisi.

Mheshimiwa Spika, ugaidi umekuwa tishio kubwa la Kimataifa la amani na usalama katika nchi zote ulimwenguni. Tukio la tarehe 11 Septemba, 2001 la kule Marekani ambapo magaidi waliyateketeza majengo ya Kituo cha Biashara cha Dunia kwa kutumia ndege za abiria, liliziunganisha nchi zote ulimwenguni, ikiwemo Tanzania katika vita dhidi ya ugaidi.

Ingawa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2002/2003 hakuna tukio la ugaidi lililotokea nchini mwetu, lakini Tanzania imeathirika kiuchumi kutokana na matangazo ya tahadhari yaliyotolewa na Serikali za Marekani na Uingereza mwezi Januari, 2003 kwamba eti kulikuwapo tishio la shambulio la kigaidi Zanzibar. Serikali hizo na nyingine za baadhi ya nchi za Ulaya ziliwashauri raia wa nchi zao kutokwenda Zanzibar. Ingawa ilidhihirika baadaye kwamba hakukuwa na tishio lolote la kweli la ugaidi, lakini Zanzibar na Tanzania kwa jumla tuliathirika kutokana na kushuka kwa biashara ya utalii. Kwa bahati mbaya tahadhari kama hizo zilitolewa tena na Marekani na Uingereza mwezi Mei, 2003 baada ya majirani zetu wa Kenya kutangaza kwamba walikuwa wanakabiliwa na tishio la shambulio la ugaidi. Matangazo ya tahadhari ya nchi hizo na nyingine za Ulaya kwa raia wao yalizihusisha pia, ingawa kwa mbali, nchi nyingine za Mashariki ya Afrika ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania imekuwa ikiuhakikishia Ulimwengu kwamba nchi yetu bado ni salama kwa raia na wageni. Napenda kuchukua fursa hii kusisitiza kauli yetu hiyo ambayo tunaitoa kwa uhakika kutokana na hatua mbali mbali za udhibiti wa kiusalama tunazochukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu matangazo ya tahadhari za ugaidi ya Januari, 2003, Jeshi la Polisi kwa ushirikiano na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, liliimarisha ulinzi katika viwanja vya ndege, bandari, mahoteli, ofisi za ubalozi na maeneo yote nyeti. Sambamba na hatua hizo, misako ya majambazi na wahamiaji haramu ilizidishwa hasa katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kagera, Kigoma, Mwanza na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, baada ya tahadhari za ugaidi zilizorejewa tena mwezi wa Mei, 2003 pamoja na kwamba hatukuwa na wasiwasi wowote wa shambulio la ugaidi hatukuipuuza hali hiyo, bali tulizidi kuimarisha ulinzi na kuzidisha ukali wa misako ya majambazi na wahamiaji haramu. Tukio la tarehe 25/05/2003 ambapo Askari wetu waliuawa lilikuja wakati ambapo kasi ya misako ilikwishaanza kuuma kwa majambazi. Itakumbukwa kuwa tarehe 19 na tarehe 20 Mei, 2003 siku tano tu kabla ya tukio hilo,

jumla ya majambazi sita waliuawa na Polisi Mjini Dar es Salaam katika matukio mawili tofauti ambapo katika kila tukio waliuawa majambazi watatu.

Aidha baada ya tukio la tarehe 25 Mei, 2003 kati ya tarehe 30 Mei na tarehe 4 Juni, 2003, jumla ya majambazi 5 waliuawa na Polisi Mjini Dar es Salaam na katika msitu kati ya Dodoma na Kibaigwa. Hatua hizo zimekwishaanza kuleta matokeo ya kutia moyo kutokana na majambazi kukamatwa kwa wingi pamoja na silaha zao ambapo wale wanaojaribu kuhatarisha maisha ya Askari wanawahiwa wao kwa mujibu wa Sheria za Kujihami kwa Askari.

Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2003, jumla ya wahamiaji haramu 110 wamerejeshwa makwao kwa nguvu kwa kutumia utaratibu wa wahamiaji wasiotakiwa *(PI)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kulipongeza kwa dhati Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri inayofanywa na Vyombo hivyo. Nawashukuru pia Wananchi ambao katika kipindi hiki, wanatoa ushirikiano wa hali ya juu kabisa kwa kutoa taarifa zinazosaidia kufichuliwa kwa wahalifu na wahamiaji haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misako sasa imeshika kasi nchi nzima na itaendelea hadi matatizo ya ujambazi na ugaidi yatakapomalizika. Natoa wito kwa Wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa Serikali katika kuwafichua wahalifu na wahamiaji haramu wakati tunaandaa utaratibu rasmi wa kuwashirikisha katika ulinzi na usalama wao na mali zao utakaojulikana kama Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine tulizochukua hasa katika kukabiliana na tishio la ugaidi ni Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria ya Ugaidi. Nimekwishatia saini Tangazo la Sheria linayoifanya Sheria hiyo ianze kutumika rasmi kuanzia tarehe 15 Juni, 2003. Aidha, tumeendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kubadilishana habari kuhusu mtandao wa ugaidi wa Kimataifa. Labda nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kurudia uhakikisho wetu ambao tumekuwa tukiutoa kila mara kwamba mapambano yetu dhidi ya ugaidi kamwe hayaelekezwi na kamwe hayatoelekezwa katika kuiandama dini yoyote au Chama chochote cha Siasa. Ombi langu kwa Watanzania wote ni kwamba tushirikiane wote kuhakikisha kwamba ugaidi hauingii nchini mwetu badala ya kuuachia uingie halafu tukalaumiana au kutuhumiana wakati Serikali ikichukua hatua za kukabiliana nao.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya ujambazi na ugaidi hayatoweza kufanikiwa bila ya kuliwezesha ipasavyo Jeshi la Polisi kwa kuliongezea Askari, kulipatia vitendea kazi na kuliimarisha kiutaalamu. Bajeti ninayoiwasilisha hivi sasa inajielekeza kwa kiasi kikubwa katika mwelekeo huo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 kuamkia tarehe 18 Novemba, 2002 lilitokea tukio baya na la kuhuzunisha ambapo mahabusu 17 walifariki mikononi mwa Polisi kwa kukosa hewa safi na wengine 16 kulazwa hospitali kwa matibabu. Tukio hilo lilitokea

katika chumba cha mahabusu cha Polisi cha Rujewa, Wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya. Kukosa hewa huko kulikosababisha maafa hayo kulitokana na mbanano mkubwa kupita kiasi katika kituo hicho cha Polisi. Uchunguzi tofauti uliofanywa na Jeshi la Polisi na Uongozi wa Mkoa wa Mbeya uligundua uzembe uliofanywa na Maofisa na Askari Polisi waliokuwa dhamana wakati wa tukio hilo. Lakini pia uchunguzi huo ulibaini mapungufu mengi kuhusiana na mazingira ya kazi, yakiwemo ukosefu wa gereza na Mahakimu wa kusikiliza kesi kila siku katika Wilaya ya Mbarali. Mrundikano wa kesi ulisababisha kuwapo kwa mahabusu wengi ambao walipaswa kupelekwa Gereza la Ruanda, lakini kutokana na kuharibika kwa gari la kusafirishia mahabusu, ilibidi mahabusu hao wawekwe katika chumba hicho kidogo cha mahabusu cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, Maofisa na Askari waliopatikana na hatia ya uzembe, walichukuliwa hatua za kinidhamu, lakini pia wamefunguliwa mashtaka mahakamani kujibu tuhuma za kusababisha vifo. Lakini pia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inachukua hatua za kuboresha mazingira ya kazi ili lisitokee tena tukio kama hilo. Miongoni mwa hatua hizo ni maandalizi ya kujenga gereza la Wilayani Mbarali, kununua magari ya kusafirishia mahabusu na vifaa vya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa tathmini ya utekelezaji wa shabaha na malengo yaliyopangiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kipindi cha mwaka wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipangiwa kukusanya mapato ya Serikali ya jumla ya shilingi 13,579,470,000/=. Hadi kufikia Aprili, 2003, zilikuwa zimekusanywa jumla ya shilingi 9,121,812,593/= sawa na 67.2% ya lengo la mwaka mzima kama inavyoonekana katika Jedwali Na.6. Tunatarajia kufikia lengo mahesabu ya mwaka 2002/2003 yatakapokamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 89,303,426,900/= kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha wa 2002/03. Kati ya fedha hizo, shilingi 40,667,152,900/= zilikuwa za mishahara na shilingi 48,636,274,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo, kama inavyoonekana katika Jedwali Na.7(a).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2003, Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 68,291,706,673/= za matumizi ya kawaida ambazo kati yake shilingi 34,085,057,269/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 34,206,649,404/= kwa matumizi mengineyo. Jedwali Na. 7(b) linatoa uchambuzi wa matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, matumizi hayo halisi hadi kufikia Aprili, 2003 ni 76.5% ya lengo la mwaka mzima kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 7(c). Inatarajiwa kwamba hadi kufungwa kwa mahesabu ya mwaka 2002/2003, lengo la matumizi litakuwa limekaribiwa au hata kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 6,200,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati

ya fedha hizo, shilingi 3,300,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya Jeshi la Polisi na shilingi 2,900,000,000/= kwa ajili ya Jeshi la Magereza.

Hadi Aprili, 2003, jumla ya shilingi 5,076,102,137/= zilikwishatumika zikiwa ni 81.9% ya lengo la mwaka mzima, kama inavyoonekana katika Jedwali Na.8. Jeshi la Polisi lilikwishatumia shilingi 2,789,666,367/= na Magereza shilingi 2,286,435,770/=. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka, inatarajiwa fedha zote zitakuwa zimetumika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi nilioutoa hapo awali unadhihirisha kwamba jumla ya shilingi 95,503,426,900/= ziliidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kipindi cha mwaka wa 2002/2003. Hadi kufikia Aprili 2003, jumla ya shilingi 73,367,808,810/= zilikwishatumika zikiwa ni sawa na 76.8% ya lengo, kama inavyoonekana katika Jedwali Na.9.

Mheshimiwa Spika, nimekwishaelezea kuhusu mwelekeo wa kuongezeka kwa uhalifu unaohusiana na ujambazi nchini mwetu. Zifuatazo ni miongoni mwa sababu mbali mbali zinazochangia ongezeko la wimbi la ujambazi na uhalifu mwingine humu nchini ni: -

Uchache wa askari. Uwiano wa askari na raia tulionao hivi sasa ni 1: 1500 wakati kigezo kinachopendekezwa Kimataifa ni baina ya 1: 400 na 1: 700.

Uchache wa vitendea kazi, hasa magari na vifaa vya mawasiliano kwa Jeshi la Polisi.

Kupanda kwa gharama za maisha.Ukosefu wa ajira, kufanya biashara na kuweka fedha nyingi majumbani/ofisini/sehemu za kazi, kubeba fedha katika mifuko ya rambo kienyeji na kutembea nazo na kula njama kwa wafanyakazi wa ndani wa Serikali au wa Makampuni kwa kushirikiana na wahalifu. Pia kuzagaa kwa silaha mikononi mwa watu kutokana na ujio wa wakimbizi na mmong'onyoko wa maadili kwa jamii na kukosekana kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya jumla ya sababu zote hizi ni kuibuka kwa wimbi kubwa la ujambazi nchini. Jeshi la Polisi halijakaa kimya likiangalia tu ongezeko hilo la ujambazi nchini. Limekuwa likichukua hatua katika kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo: -

Operesheni za pamoja za Polisi, JWTZ na Vyombo vingine vya Dola zimekuwa zikifanywa sehemu mbalimbali nchini kila ilipoonekana haja, hasa kwenye Mikoa ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, operesheni za Jeshi la Polisi za kusaka majambazi na silaha, mfano, Biharamulo – Ngara tarehe 26 Aprili mpaka 4 Mei, 2003, Tabora tarehe 18 Aprili mpaka 04 Mei, 2003, Ziwa Victoria mwezi Mei, 2003 na Kahama – Bukombe tarehe 30 Mei hadi 14 Juni, 2003 na hivi sasa ni nchi nzima.

Pia misako ya wahamiaji haramu kwa kushirikiana na Uhamiaji, kubadili uongozi na Askari kwa baadhi ya Mikoa na Wilaya, pameongezwa Askari wapya 2,000 ili kusaidia doria ya miguu hasa katika Miji mikubwa na wananchi wamekuwa wakishirikishwa katika ulinzi wa jadi kama vile Sungusungu na Mgambo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya Ukimwi juhudi za kupambana na janga hili ndani ya Jeshi la Polisi zimeendelea kwa mwaka uliopita. Tarehe 02 hadi 06 Februari, 2003 kulifanyika semina kwa Makamanda wote wa Mikoa na Vikosi na Maafisa wa Makao Makuu katika Chuo cha Polisi Moshi. Baadaye semina kama hizo zilielekezwa katika ngazi za chini tangu Mikoani, Vikosini hadi Wilayani na Vituoni na Ma-*RPC*, Wakuu wa Vikosi, hatimaye Ma-*OCD* na Wakuu wa Vituo. Shabaha ililenga katika kuufanya ujumbe uliopatikana katika Semina ya Kitaifa uwafikie walengwa ambao ni Askari wa vyeo vyote katika Jeshi la Polisi nchini. Ni matumaini yetu kuwa ujumbe umemfikia kila mlengwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 hadi 30 Januari, 2003 ilifanyika semina ya Makamanda wote nchini katika Chuo cha Polisi Moshi kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wataalamu waliobobea katika fani hii kwa siku mbili nzima waliwaeleza Makamanda ni yapi yanatakiwa kufanywa na yapi hayatakiwi kufanywa ili kudumisha Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mfano, ni Askari kutowapiga watuhumiwa, kutotumia nguvu kupita kiasi, Wananchi kupewa haki ya kutoa maelezo mbele ya mawakili wao na kadhalika. Mambo mengi yalielezwa kwa Makamanda ambao waliagizwa kuyazingatia vilivyo.

Semina kama hizo zimekuwa zikiendeshwa kikanda (Kanda za Kaskazini na Kati, Kanda ya Pwani, Kanda ya Ziwa na Kanda za Kusini na Nyanda za Juu) kati ya tarehe 17 na tarehe 2 Mei, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masuala haya kwa vitendo, zaidi ya kuteremsha ujumbe huo wa Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Askari wetu katika ngazi zote za chini hadi vituoni, Jeshi la Polisi lilitayarisha mabango yenye vidokezo vya maadili mema na yenye ujumbe wa kukataza Askari wetu wanaotumia madaraka vibaya. Aidha, kulitayarishwa vipeperushi na bango kubwa la haki za raia. Yote hayo yamesambazwa nchini kote katika kila Kituo cha Polisi ili Wananchi waweze kuyaona na kuyasoma ili ujumbe huo uwafikie walengwa.

Vita dhidi ya rushwa navyo vimeendelea kupiganwa ndani na nje ya Jeshi la Polisi. Tarehe 30 hadi 31 Januari, 2003 kulifanyika semina ya Makamanda wote nchini katika Chuo cha Polisi Moshi kuwaelimisha Makamanda kuhusiana na tatizo hili la rushwa ndani na nje ya Jeshi la Polisi. Lakini pia hatua za kinidhamu na kisheria zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya Askari, Maofisa wachache ambao wamekuwa wakijiingiza katika vitendo vya rushwa. Kati ya Januari 2000 na Mei 2003 Askari 66 walifukuzwa kazi kutokana na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hatua za utekelezaji kuhusu rushwa zilizofanywa na Jeshi la Polisi zilikuwa ni pamoja na kutayarisha mabango na vipeperushi na kusambaza nchi

nzima. Aidha, kulianzishwa kipindi maalum cha redio kiitwacho Usalama Wetu ambacho kilikuwa kinatangaza maadili mema, rushwa ni kitendo gani, kwa hiyo kuwaasa Polisi na jamii nzima dhidi ya vitendo vya rushwa. Ni matumaini yetu kwamba mabango hayo na kipindi hicho cha redio vitaleta mchango mkubwa katika kukabiliana na tatizo la rushwa nchini na kwa Askari wetu na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tarehe 05 hadi 07 Machi, 2003, Makamanda wa Jeshi la Polisi walihudhuria semina maalum huko Zanzibar kuhusu Muafaka wa kisiasa baina ya CCM na *CUF*. Kama Chombo cha Dola, walielezwa maana ya muafaka na mambo yaliyosababisha hali kufikia hapo. Maelezo mengi yalilenga katika kuwaelimisha Polisi wasipendelee upande wowote katika kutekeleza majukumu yao.

Miongoni mwa matunda ya semina hii ni jinsi Jeshi la Polisi lilivyoweza kulinda usalama wakati wa hatua zote za chaguzi ndogo zilizofanyika katika Majimbo yote 21 Tanzania Bara na Zanzibar (Pemba) kwa ufanisi mkubwa ambao wadau wote wa chaguzi hizo wanaukiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita wa fedha wa 2002/2003, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 3,300,000,000/= kwa ajili ya miradi mbali mbali ya maendeleo katika Jeshi la Polisi. Kiasi hiki kilikuwa kikubwa kuliko kiasi chochote kilichowahi kutolewa kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka mmoja. Hata hivyo kikilinganishwa na miradi inayosubiri utekelezaji kwa muda mrefu, kilikuwa ni kidogo sana. Fedha nyingi katika hizo ilibidi zitumike kulipia madeni au kugharimia viporo vya miradi ya huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fedha hizo za miradi, imewezekana kuendeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo ifuatayo:-

(a) Mradi wa ujenzi wa nyumba 48 za kuishi Maafisa na Askari katika kambi ya *FFU* Ukonga Dar es Salaam. Mradi huu ambao ulianza mwezi Mei 2000 sasa umekamilika. Nyumba hizo zilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Benjamin Mkapa; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 27/08/2002. Kukamilika kwa mradi huu kumewezesha Askari wote wa kikosi cha *FFU* Mkoa wa Dar es Salaam kurejea na kuishi kambini kulingana na azma ya Jeshi. *(Makofi)*

(b) Mradi wa ujenzi wa nyumba 53 za kuishi Askari katika kambi ya Mfikiwa, Chake Chake Pemba. Mradi huu ambao ulikwama kidogo kutokana na ukosefu wa fedha sasa umekamilika, ukiwa umebaki umeme tu ambao haujafikishwa katika eneo hilo. *(Makofi)*

(c) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Nkasi huko Mkoa wa Rukwa ambao ulikuwa umesimama kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha nao sasa unaendelea vizuri. *(Makofi)*

(d) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za kuishi Askari huko Mwanga katika Mkoa wa Kilimanjaro upo katika utekelezaji. *(Makofi)*

(e) Tumeendeleza ujenzi wa sehemu ya Hospitali Kuu ya Polisi *Kilwa Road. (Makofi)*

(f) Tumeunga mkono kwa kuchangia miradi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi inayoendeshwa na Wananchi huko Simanjiro, Kiteto, Same, Ipinda (Kyela), Kibaigwa (Dodoma), Kibakwe (Mpwapwa), Meatu na Muhukulu (Songea). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na dharura ya kulipa madeni ya nyuma, hatukuweza kununua magari ya Polisi tuliyotarajia. Aidha, matarajio yetu yafuatayo pia hayakuweza kufikiwa: -

(a) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi, Urambo.

(b) Kuanza ujenzi wa jengo la *RPC* Mkoa wa Tabora.

(c) Kukamilisha viporo vya ujenzi wa mabweni, ofisi na nyumba za Askari.

(d) Kuendeleza ujenzi wa kambi ya *FFU* ya Finya (Pemba).

(e) Kukarabati nyumba za Askari za Tunguu (Unguja).

(f) Kununua redio za mawasiliano.

(g) Kununua mashua za doria katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, ni azma yetu kuitekeleza miradi hiyo katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwani tunaamini kwamba mafanikio ya utekelezaji wa masuala ya usalama unategemea pia hali nzuri ya Askari na upatikanaji wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 10 Machi, 2003 Jeshi la Polisi lilipatiwa msaada wa magari matano mapya na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Magari hayo yameelekezwa katika shughuli mbalimbali za kupambana na uhalifu. Naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Watu wa China kupitia ubalozi wao hapa nchini kwa msaada huo ambao umetusaidia kiasi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali ya Marekani imetupatia Dola za Kimarekani 600,000 kwa ajili ya vifaa vya maabara ya upelelezi katika Kitengo cha Utambulisho, Makao Makuu ya Upelelezi. Fedha zimekwishapatikana na kazi ya uwekaji wa vifaa hivyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa ushirikiano na *TRA* na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, tumeweza pia kuanzisha Kituo cha Polisi katika bandari ya nchi kavu ya Isaka, Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumo katika hatua za ukarabati wa jengo tulilopatiwa na uongozi wa Mkoa mpya wa Manyara kwa ajili ya Ofisi ya muda ya *RPC* wa Mkoa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Jeshi la Polisi linategemea kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha uwezo wa Jeshi la Polisi katika kuwahudumia Wananchi kwa utekelezaji wa miradi ifuatayo: -

(i) Kukamilisha viporo vya mabweni, ofisi na nyumba za Askari.

(ii) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Urambo.

(iii) Kuanza ujenzi wa Jengo la Ofisi ya *RPC* Mkoa wa Tabora.

(iv) Kuendelea kushirikiana na Wananchi kujenga Vituo vya Polisi na nyumba za Askari.

(v) Kuendeleza ujenzi wa Kambi ya *FFU* ya Finya (Pemba).

(vi) Kukarabati nyumba za Askari za Tunguu (Unguja).

(vii) Ujenzi wa maabara mpya ya upelelezi.

(viii) Kuanza ukarabati wa Chuo cha Polisi, Moshi na kuboresha mazingira ya kazi katika Vyuo vya Polisi Dar es Salaam na Zanzibar.

(ix) Kununua na kufunga mtambo wa kisasa wa mawasiliano, Dar es Salaam.

(x) Kununua redio za mawasiliano.

(xi) Ununuzi wa magari ya doria, kubebea mahabusu, na ya Makamanda wa Mkoa na kadhalika.

(xii) Kuajiri Askari wapya 2000.

(xiii) Kufanya maandalizi ya ujenzi wa ofisi ya *RPC* wa Mkoa mpya wa Manyara.

(b) Kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya ujambazi na uhalifu mwingine na kuboresha maslahi na vitendea kazi kwa Polisi na kuanzisha utaratibu wa Polisi Jamii (*Community Policing*) kama mbinu mojawapo ya kushirikisha jamii katika kudhibiti uhalifu. Misako ya kutafuta majambazi na wahalifu wengine pamoja na silaha itaendelea nchi nzima kwa ari na kasi kubwa zaidi. Aidha, vita dhidi ya Ukimwi na rushwa navyo vitaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Jeshi la Magereza ni kuhifadhi wahalifu wa aina zote linaokabidhiwa pamoja na kurekebisha tabia za wale waliohukumiwa vifungo ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii. Hata hivyo jukumu hilo limeendelea kutekelezwa katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa bajeti ya kuendesha Chombo hiki muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, tumeweza kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani, lakini bila kuhatarisha usalama wa raia na mali zao. Hatua zifuatazo zimechukuliwa kukabiliana na tatizo la msongamano magerezani.

(i) Kufuatia Bunge lako Tukufu kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi za *Parole*, Sheria Na. 25/1994 kuwa Sheria Na. 5/2002, wafungwa wapatao 1500 waliotimiza masharti ya awali wanachambuliwa. Wale watakaotimiza masharti na kuidhinishwa na Bodi ya *Parole* ya Taifa wataanza kutumikia vifungo vyao chini ya utaratibu wa *Parole*. Zoezi litaendelea kuwa la kudumu.

(ii) Kuhusu utekelezaji wa Sheria Na. 6/2002 ya Huduma kwa Jamii *(Community Service)*, kazi iliyokwishafanyika ni uanzishaji wa ofisi (kitengo) ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hivi sasa taratibu zinazoendelea ni uteuzi wa Mratibu wa Kitaifa wa huduma hiyo pamoja na Watendaji wengine wa ofisi hiyo, watakaofanya pia shughuli za uhamasishaji wa Wananchi. Utekelezaji wa Huduma kwa Jamii unategemewa kuanza rasmi mwaka wa fedha wa 2003/2004 katika sehemu chache zitakazoteuliwa kwa majaribio.

(iii) Katika hatua nyingine ya Serikali, jumla ya wafungwa 2,900 waliachiliwa huru kwa msamaha uliotolewa na Mheshimiwa Rais katika kilele cha sherehe za miaka 41 ya Uhuru wa Tanzania Bara tarehe 9 Desemba, 2002. Msamaha huo ulipunguza msongamano kwa kiasi cha kuridhisha, japo hivi sasa idadi ya wahalifu inaendelea tena kuongezeka magerezani.

(iv) Hadi tarehe 1 Aprili, 2003 wafungwa wapatao 2,430 walikuwa wameachiliwa na kupewa kifungo cha nje kwa kutumia Sheria ya *Extra Mural Labour* ya mwaka 1967, hatua ambayo kwa kiasi fulani nayo imepunguza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 1 Aprili 2003 kulikuwepo wahalifu wapatao 43,557 magerezani. Kati yao 24,440 ni wafungwa waliohukumiwa na 19,117 ni mahabusu kama Majedwali Na.10 na Na.11 yanavyoonyesha. Idadi hii ni karibu mara mbili ya uwezo wa kisheria wa magereza yetu ambao ni 22,699 tu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopitawa 2002/2003, Jeshi la Magereza limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali. Askari wapya 418 walihitimu mafunzo ya awali katika Chuo cha Magereza, Kiwira na kuajiriwa rasmi kama askari. Aidha mafunzo mengine yaliyoanza katika chuo cha Magereza, Ukonga ni yale ya *Gazetted Officers* yenye wanafunzi 45 na *Advanced Course* yenye wanafunzi 157. Askari wengine 452 wameanza mafunzo ya *NCO's* kwenye Chuo cha Kiwira. .

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Jeshi la Magereza lilitekeleza miradi ifuatayo ya maendeleo ikiwemo kununua jengo kutoka Kampuni ya *SIMU 2000* kwa ajili ya Makao Makuu ya Jeshi la Magereza, kununua nyumba 57 za *ATC* kwa ajili ya Askari na Maofisa, kuendeleza ujenzi uliokuwa umekwama kwa muda mrefu katika Magereza ya Segerea, Songwe, Makete, Rombo, Handeni, Mkuza, Mpwapwa, Magu, Kibondo, Ukonga, Kiteto, Mbozi, Malya, Iringa, Kayanga, Bariadi, Shinyanga na Bunda, ukarabati na uboreshaji wa Magereza ya Isanga (kazi imekamilika), Butimba (kazi iko hatua za mwisho), Uyui, Maweni na Ukonga, kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka katika jumla ya magereza 33 na kununua matrekta 10 na zana zake pamoja na ununuzi wa mashine na malighafi kwa viwanda vya ushoni na sabuni (Ukonga), sabuni (Mbeya) na mkonge (Kihonda Morogoro).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Jeshi la Magereza litaendelea kuboresha huduma zake na kutekeleza miradi ifuatayo ya maendeleo ambayo ni kuendesha kozi ya mafunzo ya awali kwa wanafunzi 793, kukamilisha viporo vya ujenzi wa nyumba za Askari, kukamilisha ukarabati wa Magereza ya Butimba, Maweni, Uyui na Ukonga, kuendelea kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka magerezani, ununuzi wa magari, uimarishaji wa miradi ya kilimo na viwanda vidogo vidogo na kukamilisha baadhi ya miradi viporo ya ujenzi wa mabweni ya wafungwa na kuanza ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuhifadhi wahalifu 100 katika Gereza la Mahabusu la Mbarali na bweni moja Gereza la Kyela. *(Makofi)*

Pia, kumalizia viporo vya ujenzi kwenye Chuo cha Magereza Kiwira ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bweni la wanawake, kukarabati Chuo cha Magereza Ukonga na uhifadhi wa mazingira kwa kupanda miti kwa ushirikiano na *UNDP*.

Ni matumaini yangu kwamba hatua hizi na nyingine zitakazochukuliwa chini ya matumizi ya kawaida zitaendelea kuyafanya mazingira ya magereza kuwa bora zaidi na kupunguza msongamano ili kujiepusha na matukio ya kuhatarisha maisha ya wafungwa na mahabusu kama lile la Mbarali.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini lina jukumu kubwa la kuokoa maisha na mali kwenye ajali za moto na majanga mengine. Jukumu hilo hutekelezwa kwa ushirikiano wa vikosi vya Miji Mikubwa, Manispaa, Miji, Viwanja vya Ndege, Bandari, Makampuni Binafsi na Umma wa Watanzania kwa ujumla. Jeshi pia linasimamia Sera ya Zimamoto na Uokoaji na kutoa mafunzo. Majukumu mengine ya Jeshi la Zimamoto ni kuelimisha umma juu ya tahadhari ya moto na kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye majumba na maeneo mbalimbali yenye uwezekano wa kupatwa na majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/03, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilifanya ukaguzi wa tahadhari na kinga katika Taasisi na maeneo 16 mbali mbali kama inavyobainishwa katika Jedwali Na. 12.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mpango wa ununuzi wa gari moja la kuzimia moto lenye ngazi ndefu na jingine lenye uwezo wa kubeba shehena kubwa ya maji na madawa. Magari hayo yatakabidhiwa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Yatapopatikana magari hayo yale matatizo ya kushindwa kuzima moto kwenye majengo marefu na magari kuonekana yanafika kwenye matukio ya moto yakiwa na maji machache, yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi pia liliandaa mkutano wa wadau mbalimbali wa zimamoto na uokoaji uliofanyika Bagamoyo tarehe 5 hadi 7 Mei, 2003 ambao ulitafakari utekelezaji wa Sera ya Zimamoto na Uokoaji na ufanikishaji wa uratibu wa shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa kasi na ufanisi mkubwa zaidi. Miongoni mwa kazi mahsusi zitazofanywa ni pamoja na ufuatiliaji wa upatikanaji wa jengo litakalotumiwa kwa pamoja na Makao Makuu ya Jeshi hilo na Chuo cha Zimamoto na Uokoaji. Kazi nyingine ni kukamilisha Kanuni za Usalama wa Moto katika ujenzi wa majengo, kusimamia mafunzo ya askari wa Zimamoto, ukaguzi wa majengo, na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu tahadhari ya moto na namna ya kutumia zana ndogo ndogo za kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/03, Idara ya Uhamiaji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaazi wa wageni na raia nchini. Mwaka 2002, Idara iliwapokea na kuwahudumia jumla ya wageni 358,050. Jumla ya wageni 9,684 walipewa vibali vya ukaazi. Raia waliopatiwa pasipoti walikuwa 49,136. Takwimu zinazohusiana na majukumu hayo kwa mwaka 2002 kwa ulinganisho na 2001. Zinatolewa katika jedwali Na. 13.

Mheshimiwa Spika, Idara pia ilikusudia kutekeleza malengo mahsusi mbali mbali yakiwemo kukarabati na kujenga ofisi na nyumba kwa ajili ya makazi ya watumishi, kununua na kufunga mtambo wa kuchapishia hati za kusafiria *(passport)* katika Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar, kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Hati za Kusafiria na kununua hati za kusafiria zinazosomeka kwa kompyuta. Malengo yote hayo yalitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo hayo, mambo yafuatayo yamefanyika:-

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha ukarabati wa ofisi na nyumba katika vituo vya Horohoro, Kyela, Kasulu, Namanga na Ofisi za Mwanza. *(Makofi)*

Pia tumekamilisha ujenzi wa vituo vipya vya Kasumulu na Mutukula, tumenunua nyumba kwa ajili ya ofisi na makazi ya watumishi. Majengo hayo yamenunuliwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Tabora, Pwani, Shinyanga na Mtwara na tumenunua mtambo wa kuchapishia hati za kusafiria katika Ofisi ya Uhamiaji,Zanzibar, ambao umekwishaanza kutoa *Passport* za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mipango imekamilika ya kununua *Passport* mpya zinazosomeka kwenye kompyuta ambazo zitaanza kutumika mnamo mwezi wa Januari 2004. Imetungwa Sheria ya Hati za Kusafiria.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji imeweza pia kuajiri Maafisa Uhamiaji 300 wapya ambao hivi sasa tayari wanaendelea na mafunzo ya awali. Aidha, imeweza kutayarisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Uhamiaji na Uraia ambayo imekwishaanza kujadiliwa na wadau mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kufunga mtandao wa kompyuta kwa ajili ya kutunza taarifa mbali mbali limeanza kutekelezwa kwa awamu kutokana na ukubwa wa gharama. Hatua iliyokamilika ni utafiti wa namna mtandao huo utakavyofanya kazi kwa kuunganisha Makao Makuu, Dar es Salaam, Zanzibar, mikoa yote, Wilaya na vituo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Kitaifa, Serikali iliendelea na mazungumzo na mzabuni aliyetarajiwa kuendesha mradi huo kufuatia maelekezo ya Mahakama. Napenda sasa kuliarifu Bunge kwamba tumeamua kusitisha mazungumzo na mzabuni huyo baada ya kuridhika kwamba hakuna uwezekano wa kufikia muafaka naye. Hivi sasa tunashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Uchaguzi ya Taifa na wadau wengine kubuni utaratibu mwingine wa kupata vitambulisho hivyo haraka. Tunakusudia kubuni kitambulisho kitachokidhi mahitaji ya uraia, uhamiaji na daftari la kudumu la wapiga kura, kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji nchini ni miongoni mwa Idara na Asasi mbalimbali za Serikali zilizoathiriwa na matatizo ya Ukimwi na rushwa. Hivyo, Idara hiyo kwa kushirikiana na chombo cha kupambana na ukimwi majeshini *(Tanzania Civil Military Alliance)* inaendelea kupiga vita janga la ukimwi kwa kuendesha semina, na kutoa ushauri nasaha kwa watumishi bila kuwanyanyapaa wale waliokwishaathirika.

Aidha, inaendelea na hatua za kinidhamu kwa maafisa wake wanaotuhumiwa kujiingiza katika rushwa. Afisa mmoja alifukuzwa kazi na 10 wamesitishwa kazi kutokana na vitendo vya rushwa katika kipindi cha mwaka wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/04, Idara ya Uhamiaji inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

Kukarabati vituo vya Manyovu, Sirari, Tunduma na Ofisi za Mikoa ya Mara na Dar es Salaam, utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa kuweka mtandao wa mawasiliano ya kompyuta - Dar es Salaam, Zanzibar, mikoa, wilaya na vituo, kuajiri maofisa uhamiaji 370 wapya, ununuzi wa magari na kompyuta, kukamilisha taratibu za utungaji wa Sera ya Taifa ya Uhamiaji na Uraia, kuanza kutoa hati mpya za kusafiria zinazosomeka kwenye kompyuta, kulimaliza tatizo la kukwama kwa utoaji wa vitambulisho vya Kitaifa na kukamilisha utafiti wa mahali pa kuweka kituo cha mpakani na Msumbiji eneo la Wilaya ya Mbinga na kuanza maandalizi ya ujenzi katika eneo mwafaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 nchi yetu imeendelea kubeba mzigo wa kuhifadhi wakimbizi 716,847 toka nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda, Somalia na kwingineko, katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa, Tabora na Tanga. Aidha, zaidi ya idadi hiyo ya wakimbizi, inakadiriwa kuwa wapo raia wa kigeni wapatao 300,000 toka nchi za Burundi, Kongo, Msumbiji, Rwanda na kwingineko ambao waliingia nchini katika mazingira yanayofanana na ya ukimbizi lakini wanaishi kiholela katika maeneo mbalimbali ya nchi hususan katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ikishirikiana na Serikali za Burundi na Rwanda pamoja na Shirika la *UNHCR* inaendelea na zoezi la kuwarejesha wakimbizi wa nchi hizo makwao. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumefanikiwa kuwarejesha wakimbizi karibu wote wa Rwanda waliokuwa wanaishi hapa nchini, isipokuwa wale ambao ni watuhumiwa na wahalifu walioko mikononi mwa vyombo vya sheria ambao utaratibu maalumu wa kuwashughulikia unaandaliwa. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuzingatia hali ya amani ilivyo nchini Rwanda kwa sasa, Serikali ya Tanzania haipokei tena raia wa Rwanda wanaotaka hifadhi ya ukimbizi nchini. Wakimbizi wote wa Rwanda ambao hawakurejea kwao kwa hiari hadi ilipofika mwezi wa Machi, 2003, hatuwatambui kama wakimbizi na hivyo watarejeshwa kwao kwa kutumia sheria za Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wakimbizi wa Burundi, jitihada za kuwarejesha zinaendelea. Mpaka tarehe 16 Aprili, 2003 jumla ya wakimbizi 43,000 kati ya wakimbizi 124,000 waliojiandikisha kutaka kurejea makwao walikuwa wamerejea kwao. Wengi wanaendelea kurejea kwao kwa hiari hata kwa kujitegemea pale ambapo *UNHCR* haitoi msaada.

Hata hivyo, kukosekana kwa usalama katika baadhi ya maeneo ya nchi ya Burundi kumekuwa kikwazo kikubwa kinachokwamisha kutekelezwa kikamilifu kwa zoezi la kuwarejesha wakimbizi katika nchi yao ya asili. Kwa hali hiyo, nchi yetu itaendelea kushiriki katika juhudi za kikanda za kuleta amani zinazoongozwa na Mwakilishi wa Msuluhishi wa mgogoro wa Burundi, Makamu wa Rais wa Afrika Kusini, Mheshimiwa Jacob Zuma, kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinapatikana Burundi kuwezesha wakimbizi wa nchi hiyo kurejea kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wakimbizi wanaotoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, idadi yao imeendelea kuongezeka kutokana na vurugu za vita zinazoendelea nchini mwao hususan katika mkoa wa Kivu Kusini unaopakana na nchi yetu upande wa pili wa Ziwa Tanganyika. Bado tuna matumaini kwamba jitihada za kuleta amani nchini humo zitaleta matunda na kuwezesha wakimbizi hao kuanza kurejea makwao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakimbizi wa Kisomali wenye asili ya Kibantu na hasa wa Kizigua, Shirika la *UNHCR* limekamilisha ujenzi wa kambi yao mpya ya Chogo. Tayari wakimbizi hao wamekwishahamishiwa katika kambi hiyo kutoka kambi yao ya zamani ya Mkuyu. Maandalizi yanafanywa ya kukabidhi majengo na vifaa mbalimbali vya kambi ya zamani ya Mkuyu kwa uongozi wa Mkoa wa Tanga kwa ajili ya matumizi watakayoamua wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Sera ya Wakimbizi sasa iko tayari. Aidha, Wizara yangu inafanya mapitio ya Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998 kwa lengo la kuirekebisha ili ilingane na Sera na pia kuandaa kanuni za Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni, misaada ambayo Jumuiya ya Kimataifa inatoa kusaidia nchi yetu kuhudumia wakimbizi imekuwa ikipungua na kusababisha ugumu wa kuwahudumia na pia kuathiri jitihada za kukarabati maeneo yaliyoathirika kutokana na kuwepo kwa wakimbizi. Mfano wa wazi wa upungufu huo unajidhihirisha kwa kupungua kwa chakula cha nafaka kinachotolewa na *WFP* kwa wakimbizi hadi asilimia 50 kuanzia Januari, 2003. Kuhusiana na upungufu wa chakula, Serikali iliziomba nchi mbalimbali hisani kutoa msaada wa chakula kwa wakimbizi. Napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru nchi zilizoitikia wito wa Serikali kwa kutoa msaada unaohitajika. Baadhi ya nchi hizo ni Marekani, Jumuiya ya Ulaya kupitia *ECHO,* Ubelgiji, Uswisi na Sweden. Kwa kuzingatia misaada hiyo, kiwango cha chakula kinachogawiwa wakimbizi kinatarajiwa kuongezeka kuanzia mwezi huu wa Julai, 2003.

Napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyingine tena kutoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa, kuendelea kusaidia nchi yetu kuhudumia wakimbizi na pia kutusaidia kuanzisha miradi ya kupunguza athari mbalimbali zilizojitokeza kwa sababu ya kuwepo kwa idadi kubwa ya wakimbizi nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Idara ya Kuhudumia Wakimbizi itaendelea na majukumu yake hasa kuanza utekelezaji wa Sera ya Wakimbizi na kuongeza kasi ya kuwarejesha makwao wakimbizi wa Burundi na Kongo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Jamii inaendelea na kazi ya kuchambua na kuandikisha Asasi zisizokuwa za Serikali *(AZISE* au *NGOs).* Idadi ya asasi hizo imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na kwa sasa tunazo jumla ya asasi 11,925. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asasi zisizokuwa za Serikali zimeendelea kuwa chachu kwa miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii. Zipo asasi ambazo zimekuwa mfano mzuri na daima zipo bega kwa bega na Serikali kuendeleza miradi katika fani za afya, elimu, ufundi, mazingira pamoja na fani nyingine ndani ya nchi. Wananchi wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wa mambo mazuri yanayofanywa na asasi hizi. Serikali itaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano kwa asasi zote zile zinazochangia kufanya maisha ya wananchi wetu kuwa bora na kukua kwa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zipo pia baadhi ya asasi ambazo si makini na hata kuwepo kwake kunatiliwa mashaka. Baadhi yake zinajihusisha na mambo yaliyo nje ya malengo na madhumuni yake, na hata kuwa kero kwa wananchi. Asasi za aina hii tutaendelea kuzishughulikia na kuzichukulia hatua kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuzifuta zile zinazoelekea kutorekebishika.

Aidha, lengo la Wizara kwa mwaka wa 2003/2004 ni kuendelea kufanya tathmini ya asasi zote, ili kutambua uhai wake kwa lengo la kuweka kumbukumbu sahihi. Ni matumaini ya Wizara yangu kuwa baada ya zoezi hili kukamilika tutaondokana na *NGOs* uchwara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya iliendelea na utekelezaji wa jukumu lake la kuratibu udhibiti wa utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya. Iliandaa vikao mbali mbali na wadau wakuu katika vita dhidi ya dawa za kulevya. Ilishiriki pia katika mikutano ya kimataifa na kushirikiana kwa njia mbalimbali na Jumuiya ya Kimataifa katika jukumu hili zito. Tume pia iliendelea kutumia kila fursa iliyoipata kuelimisha umma juu ya madhara ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza awali, Tume hii hivi sasa imehamia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda katika hatua hii kumshukuru Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kwa msaada na ushirikiano wake mkubwa ulionipunguzia muda wa kuielewa na kuizoea Wizara. Nashukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ndugu Benard Mchomvu, Mkuu wa Jeshi la Polisi *(IGP),* Omar Mahita, Kamishina Mkuu wa Magereza Nikasi Banzi, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara zote pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa ushirikiano walionyesha katika utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa mwaka 2002/2003. Nashukuru pia kwa maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Shukrani zangu pia kwa wananchi wote kwa mchango wao mkubwa wanaotoa katika kuisaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hasa katika kufichua wahalifu. Pia natoa shukrani za dhati kwa Jeshi la Mgambo, Polisi Wasaidizi *(Auxiliary Police),* Vikundi vya Sungusungu na Makampuni binafsi ya ulinzi kwa kusaidiana na Wizara yangu katika kuimarisha ulinzi na usalama nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama nitamaliza hotuba yangu bila ya kuwataja wahisani mbalimbali waliotusaidia. Nchi wahisani ambazo zimekuwa zikitusaidia ni pamoja na China, Marekani, Japan na Uingereza. Nawashukuru wote kwa misaada yao ya hali na mali. Napenda pia niyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya *UNHCR, INTERPOL, SAFER AFRICA, WFP, UNDP* na *EU* kwa ushirikiano, ushauri na misaada yao, bila kusahau Jumuiya zetu za Ushirikiano wa Kikanda za *SADC* na *EAC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia wananchi na wahisani kwamba Serikali imekwishaamua rasmi kuyaingiza masuala ya usalama wa raia na mali zao katika vipaumbele vya kibajeti kitaifa. Ushahidi ni kwamba bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ninayoiwasilisha hivi sasa imeongezeka kwa 27.1% ikilinganishwa na ile ya mwaka wa 2002/2003 ambayo yenyewe nayo ilikuwa na ongezeko la 34.7% juu ya ile ya 2001/2002, kama inavyoonekana katika Majedwali Na. 16(a) hadi (d). Katika uongezekaji huo wa 2003/04, bajeti ya Jeshi la Polisi imeongezeka kwa 29.3% na ile ya Magereza kwa 30.5%. Hiki ni kielelezo cha jinsi Serikali ilivyopania kukabiliana na matatizo ya uhalifu nchini na kuifanya hali ya maisha ya wafungwa na mahabusu magerezani kuwa bora zaidi.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepangiwa kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 12,916,353,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004. Kama inavyochambuliwa katika jedwali Na. 15.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya jumla ya shilingi 121,414,739,000/= kwa mwaka wa 2003/2004. Kama inavyoonekana katika jedwali Na. 19

Kati ya fedha hizo, shilingi 113,214,739,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:-

Fungu 28: Polisi: shilingi 65,486,361,200/=;
Fungu 29: Magereza: shilingi 38,060,371,900/= ;
Fungu 51: Utawala: shilingi 9,668,005,900/= uchambuzi zaidi
unapatikana katika Jedwali Na. 17

Mheshimiwa Spika, shilingi 8,200,000,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo Jeshi la Polisi limetengewa shilingi 5,300,000,000/= na Magereza shilingi 2,900,000,000/= kama inavyoonekana katika Jedwali 18.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa uvumilivu.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA (k.n.y. MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2003/2004

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kwa mujibu wa Kanuni ya 81 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo za mwezi Mei, 2003. Aidha nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambao kwa kutumia uzoefu wao kuhusiana na masuala mbalimbali ya Ulinzi na Usalama walijadili kwa kina masuala hayo pamoja na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2003/2004.

Wajumbe wa Kamati hii ni Mheshimiwa John Malecela, Mwenyekiti, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Omari Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. Naishukuru pia Sekretariati ya Kamati hii chini ya usimamizi wa Makatibu Ndugu Mathew Kitundu na Ndugu Angumbwike Ng'wavi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Katibu Mkuu na Wataalam wengine wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa za Utekelezaji wa ahadi za Wizara zilizotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu, ushauri wa Kamati ya Kisekta ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa Wizara uliotolewa wakati wa kupitisha makadirio ya Wizara hii kwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 na 3 Juni, 2003, Kamati ilizijadili na kuzichambua taarifa hizo pamoja na kujadili Makadirio ya Matumizi ya Jeshi la Polisi, Fungu 28 Magereza, Fungu 29 na Wizara (Utawala) Fungu 51 kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati ya Kisekta ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na wa malengo ya wizara ya mwaka 2002/2003

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati ya Kisekta ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na wa malengo ya Wizara ya Mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizijadili taarifa hizo kwa kina na kuipongeza Wizara kwa kufanya kazi zake katika mazingira magumu ya upungufu wa vitendea kazi. Kuhusu mambo ambayo utekelezaji wake ni wa kuendelea, Kamati ilielekeza kuwa yaendelee kutekelezwa lakini kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004. Kamati ilijadili mipango ya Wizara ya mwaka 2003/2004 ya kuboresha mazingira ya kazi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelezwa na Waziri katika hotuba yake. Hotuba ya Waziri inatilia mkazo malengo yafuatayo:

Kwanza, kukamilisha ujenzi na ukarabati wa nyumba na Ofisi za Jeshi la Polisi, Magereza na Idara ya Uhamiaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kulipia majengo yaliyonunuliwa kwa ajili ya kuishi askari na Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Magereza.

Pili, kuboresha na kununua vitendea kazi, kama vile vifaa vya mawasiliano; magari kwa ajili ya Vituo vya Polisi, doria na ya kubebea mahabusu na kompyuta. Aidha, kuimarisha huduma za umeme, mifumo ya maji safi na maji taka magerezani na maeneo mengine ya kufanyia kazi.

Tatu, kuendelea na jitihada za kuboresha maslahi ya askari ikiwa ni pamoja na kuajiri askari wapya.

Nne, kuongeza uwezo wa askari katika kushughulikia kesi kwa kuwapa mafunzo zaidi kuhusu kazi zao pamoja na vitendea kazi.

Tano, kuimarisha vikosi vya zimamoto ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa askari wa zimamoto, kutoa elimu kwa umma, kuajiri askari wapya na kukamilisha kanuni za usalama wa moto katika ujenzi wa majengo.

Sita, kuendelea na zoezi la kuwarejesha makwao Wakimbizi wa Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)*.

Saba, kuendeleza vita dhidi ya Ukimwi kwa wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na wafungwa.

Nane, kuimarisha utaratibu wa kushirikiana na raia wema *(Community Policing)* na kuimarisha ulinzi wa jadi kama mbinu ya kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Spika, tisa, kukamilisha kutengeneza Sera ya Taifa ya Uhamiaji na Uraia ili iwe dira ya shughuli za uhamiaji na kumi, kuanza utekelezaji wa Sera ya Wakimbizi na kufanya mabadiliko ya Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998 na kuandaa kanuni za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo kwa mwaka 2003/2004 Wizara iliomba fedha kwa mafungu yake kama ifuatavyo:-

Jeshi la Polisi: Fungu 28 Matumizi ya Kawaida shilingi 65,486,361,200/=, Mipango ya Maendeleo shilingi 5,300,000,000/=;

Jeshi la Magereza: Fungu 29 matumizi ya kawaida shilingi 38,060,371,900/=, mipango ya maendeleo shilingi 2,900,000,000/=; na

Utawala: Fungu 51 shilingi 9,668,005,900/=.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara, awali ya yote Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kuwakamata majambazi walioua askari polisi watatu na mbwa wa Polisi mmoja siku ya tarehe 25 Mei, 2003. Aidha, inashauri kuwa juhudi hizo ziendelee ili kudhibiti wimbi la ujambazi linaloongezeka siku hadi siku. *(Makofi)*

Pili, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hususan Jeshi la Polisi, kutoka shilingi milioni 55,178 kwa mwaka uliopita hadi shilingi milioni 70,780 kwa mwaka 2003/2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, Kamati inashauri kwamba kwanza, Jeshi la Polisi liongeze juhudi katika kukabiliana na tatizo la ujambazi kwa kuendesha msako wa nyumba hadi nyumba. Aidha, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, zifanywe operesheni za kupambana na uhalifu nchini.

Pili, mitaala ya mafunzo ya polisi iboreshwe, mafunzo ya upelelezi, sheria na mbinu za kivita yaende na wakati ikiwa ni pamoja na kutumia zana za kisasa na tatu, Serikali ikarabati majengo ya Chuo cha Polisi Moshi ambacho ndicho Chuo pekee cha mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi hapa nchini na kinachopokea wanachuo kutoka nchi za nje. Aidha, tanki la kuhifadhia maji la Chuo ambalo limechakaa lijengwe upya na nne, Serikali ianzishe Chuo cha Upelelezi na iboreshe mafunzo kwa askari polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali itoe muda maalum kwa watu wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kusalimisha silaha hizo. Watu wote wasio raia wanaoishi nchini bila kibali, vile vile wajisalimishe na Kamati za ngazi zote za ulinzi na usalama nchini zihakikishe kuwa hakuna watu wanaohifadhi majambazi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Sita, Serikali iangalie upya hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari polisi waliohusika na tukio la vifo vya mahabusu vilivyotokea mwezi Novemba mwaka 2002 huko Mbarali, Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Saba, Serikali ifanye juhudi ya kuhakikisha kuwa askari polisi wanaishi kwenye makambi badala ya kuishi uraiani ili kudumisha nidhamu katika utendaji kazi wa askari polisi. *(Makofi)*

Nane, Serikali ibuni njia imara za kudhibiti wizi wa magari, uhamishaji na uingizaji wa magari ya wizi nchini na kwa kushirikiana na nchi jirani, kukamata magari ya wizi. *(Makofi)*

Tisa, Serikali ihakikishe kuwa wanaokwenda kuchukua mafunzo ya Polisi wawe wamehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Uhamiaji, kwanza Serikali iweke mpango maalum na wa kudumu wa kuwataka wasio raia hapa nchini kujitokeza ili hatua zifaazo ziweze kuchukuliwa na pili, Serikali iangalie upya utoaji wa uraia wa Tanzania ili wanaopewa wawe ni wale tu ambao watakuwa na manufaa kwa taifa hili. Aidha, Serikali iwe makini katika kutoa vibali vya kufanyakazi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali itekeleze kwa haraka ahadi yake ya kutengeneza vitambulisho vya uraia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iendelee na juhudi za kuishawishi Jumuiya ya Kimataifa ili wakimbizi kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo watengewe maeneo salama *(safe zones)* ndani ya nchi zao badala ya kuendelea kuishi nchini mwetu. *(Makofi)*

Tano, Wasomali wa asili ya Kizigua waliorudi Handeni wafikiriwe kupewa uraia kwa kuwa asili yao ni Watanzania. Aidha, wakimbizi wa Ulyankulu, Mshamo na Katumba wasiendelee kuhudumiwa na Serikali kwa kuwa wanao uwezo wa kujitegemea kwa kilimo. *(Makofi)*

Sita, Serikali iongeze vituo vya uhamiaji mipakani kwa kuwa vilivyopo ni vichache sana na kuwe na mpango maalum wa kutathmini mahitaji na upungufu uliopo ili kuchukua hatua zinazofaa za kuboresha huduma katika vituo hivyo. Kwa mfano, Kituo cha Namanga hakuna umeme na vifaa vya teknolojia ya kisasa. Aidha, Kituo cha Uhamiaji kianzishwe Olmorok, Mkoani Arusha kwa kuwa wageni wengi wanapitia pale. Hatua hiyo itaimarisha usalama wa nchi na kuiongezea Serikali mapato. *(Makofi)*

Saba, Vituo vya mipakani viwe na mashine za kutambua pasi na noti bandia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara ya Magereza. Ili kuboresha shughuli za Jeshi la Magereza na kupunguza tatizo la mlundikano wa Mahabusu Magerezani, Kamati inashauri tena kwamba moja, Serikali iwe na mpango wa dharura wa kufundisha na kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, pili, Serikali iweke muda maalum wa kukamilisha upelelezi na kusikiliza kesi hasa za muda mrefu na iweke muda maalum wa watu kukaa mahabusu, tatu, Sheria ya Huduma kwa jamii *(community service)* itekelezwe kwa ukamilifu na nne, Serikali iboreshe huduma za wafungwa magerezani, na iangalie uwezekano wa kupanua magereza nchini.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali itenge fungu maalum la fedha kwa ajili ya kuwapatia vifaa wafungwa wanapomaliza vifungo vyao ili kuwawezesha kujiajiri na sita, Serikali iendelee kufufua miradi ya magereza ili wafungwa waweze kuitumia kwa mafunzo na kwa kuzalisha mali kwa matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Zimamoto. Ili kutatua tatizo la majanga ya moto Kamati inashauri kuwa moja, Serikali isimamie kuona kuwa tahadhari ya kuzuia majanga ya moto inachukuliwa na wawekezaji wote. Aidha, Serikali itunge sheria ya kuipa Idara ya Zimamoto mamlaka ya kufanya ukaguzi katika majengo mbalimbali ya Serikali na ya watu binafsi.

Pili, Mamlaka zinazohusika na utoaji vibali vya ujenzi zihakikishe kuwa majengo husika yameweka vyombo vya kuzimia moto. Aidha, kila mwenye nyumba awajibike kuweka tahadhari ya moto katika nyumba yake.

Tatu Serikali iweke sera maalum itakayofuatwa na taasisi zote zinazohusika na uzimaji moto. Serikali ihakikishe kuwa vifaa vya kuzimia moto vinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Tano, Serikali itoe mafunzo kwa wananchi ya kuepusha milipuko ya mioto na kutumia vifaa mbali mbali vya kuzimia moto na ya uokoaji.

Wizara ifanyie kazi mpango wake wa miaka kumi ujulikanao kama *Project Profiles for Strengthening Capacities in the Police Force, Prison Force, Immigration and Fire and Rescue Services,* kuhakikisha kuwa mpango huo unatengewa fedha katika bajeti ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kutumia tena fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati hii kwa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2003/2004.

Pili, Kamati inasisitiza tena kuwa Hazina iwe inatoa kibali ili *retention* inayotokana na mapato yanayokusanywa na Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji, yatumike kama nyongeza katika bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi ambacho Bajeti haikidhi mahitaji muhimu ya vyombo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Ili kukidhi mahitaji ya Wizara, fedha iliyotengwa kwa mwaka huu wa bajeti isitumike kwa kulipia madeni ya nyuma na nne na mwisho nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kuandaa taarifa hii na kunipa heshima hii ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kutamka mbele ya Bunge lako tukufu, kuwa Kamati yangu imepitisha bila marekebisho Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyoonyeshwa katika Fungu 28, Fungu 29 na Fungu 51 yenye jumla ya shilingi 121,414,739,000/=.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGOBA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika,

napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa Niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c).

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo zilizopita na wale wote ambao wako ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipigia kelele Serikali na angalau mwaka huu pesa imeongezeka mara dufu kuhahakisha Jeshi letu linapata hela ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Msaidizi wake Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu na timu ya wataalam waliosaidiana nao katika kuandaa Hotuba na Bajeti hii ambayo kwa kiwango kikubwa inaridhisha kama itatekelezwa vizuri. Pamoja na pongezi hizo, Kambi ya Upinzani inadhani kuna maeneo ambayo yanahitaji ufafanuzi wa kina kwa manaufaa ya Bunge lako Tukufu na wananchi kwa Ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kurejea kwa kina Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kuitafakari ni kwa kiasi gani yaliyosemwa na Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake iliyokuwa nzuri na ya kutia matumaini kwa utekelezaji. Kambi ya Upinzani inadhani bila kuanzisha utamaduni huu, tutakuwa na tabia ya kusifia hotuba, lakini utekelezaji unakuwa siyo mzuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Makamanda wa Polisi wa Mikoa katika Mabaraza yao na askari wameelekezwa kusisitiza umuhimu wa *Police Trafic* kuingia ndani ya mabasi na kuacha kuongea faragha na Madreva au Makondakta nyuma ya mabasi.

Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya wananchi, naomba uwaambie abiria kwamba askari anapoongea faragha na dreva au kondakta nyuma ya gari au mafichoni abiria wafanye nini? Kwa sababu askari hao hao wanasema mabosi wetu ndiyo wamewatuma kufanya kazi ya usalama barabarani na wasiporudi na kitu kidogo mara nyingi huwa hawapangwi katika kazi za u-*trafic* barabarani jioni.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi kuongezeka hapa nchini sio siri, hali ni mbaya sana. Ni hivi majuzi tu, askari wetu waliuwawa na majambazi Dar es salaam eneo la Kawe. Kwa kweli hakuna Mtanzania mwenye akili timamu anayeweza kufurahia hilo. Kambi ya Upinzani inatoa pole kwa hao marehemu pamoja na wafiwa wote.

Pamoja na kwamba hali hii kwa sasa hata polisi wanauwawa bado lawama ipo upande wa Polisi. Kambi ya Upinzani inauliza wananchi wangapi wameuwawa na Majambazi au kuvamiwa? Je, ni jinsi gani Polisi wamekuwa wakifuatilia mambo ya raia? Ni kiasi gani raia wanapovamiwa na majambazi hata akipiga simu Polisi, huchukua zaidi

ya saa tatu kupata msaada? Na ni kwa nini hata watuhumiwa wakipatikana, huachiwa katika mazingira ya kutatanisha?

Haya maswali yanatokana na Polisi waliouwawa na majambazi eneo la Kawe na *operation* iliyofuata mpaka sasa ilikuwa ni ya kipekee kwani majambazi wengi walipatikana au kuuawa. Hii inaonyesha wazi kwamba kuna uhusiano mkubwa kwa baadhi ya majambazi na polisi. Kwani majambazi wengine, walikuwa wanafuatwa sehemu za makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuficha mara nyingi mtu anapofanya vizuri lazima asifiwe. Kambi ya Upinzani haibudi kumpongeza *RPC* Dodoma kwa kazi yake nzuri anayoifanya pamoja na vijana wake. Amefanya kazi kuhakikisha majambazi wote waliotoka Dar es Salaam kukimbila kwenda nchi za nje ameyadhibiti na ya hawakuvuka hapa. Lazima tumpongeze kijana huyu anavyofanya kazi yake vizuri. Naiomba Serikali imwangalie kwa makini kijana huyu na vijana wake ili angalau baadaye uwe mfano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Askari waliopelekwa Pemba kwa ajili ya *operation* kutokana na machafuko ya kisiasa hadi leo bado wako huko na wanaendelea kupata posho na huduma zingine muhimu, je, askari hao waliopo huko kwa muda waote wanafanya nini? Je, hayo sio matumizi mabaya ya fedha za umma? Tunao uhaba mkubwa wa askari sasa walioko huku na kwingineko kazi iliyowapeleka kama imekwisha warudi maeneo yao ili sehemu zilizo na uhaba wa askari waje wasaidiane ulinzi wa Taifa kutokana na kwamba sasa hivi ujambazi umepamba moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001 huko Pemba. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Benjamin William Mkapa, aliunda Tume ya kuchunguza matukio ya huko Pemba na Mheshimiwa Hashim Mbita, alikuwa Mwenyekiti wa Tume hiyo, baada ya mahojiano na watu kadhaa bara na Visiwani Kamati ya Mheshimiwa Hashim Mbita, ilishauri kuwa wengi walioathirika walipwe fidia, lakini tangu wakati huo hadi leo hawajalipwa je, Serikali ina sema nini juu ya ukimya huu? Tulidhani baada ya Muafaka Serikali ingetekeleza ahadi zake kwa waathirika wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazo nzuri tu tena sana kuanzishwa kwa Polisi jamii katika makazi ya wananchi. Bila shaka wananchi wamekuwa katika hiyo polisi jamii kwa muda mrefu kwa kutoa taarifa za uhalifu sehemu mbali mbali hususan katika vituo vya polisi bila mafaniko.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu zaidi, mtu anayetuhumiwa mara nyingi ndiyo rafiki mkubwa wa baadhi ya Polisi sasa hata ukitoa taarifa, yule mtuhumiwa hashughulikiwi na matokeo yake, anapewa taarifa kwamba yote fulani ndiye aliyeleta taarifa hapa Kituoni. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi hili suala la kufufua polisi jamii utekelezaji wake ukoje? Ni budi ukawalezea wananchi ili waisaidie kwenye Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuanzisha kitengo maalum ndani ya Jeshi la Polisi cha kushughulikia na kuziba mianya ya hujuma katika taasisi za fedha na taasisi nyingine za Serikali. Pamoja na pongezi hizi, bado Kambi ya Upinzani inakutahadharisha Mheshimiwa Waziri kwamba Kitengo hicho kisiwe cha kuendeleza ubadhirifu kama ilivyo katika vitengo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuelewa madhara ya kutumia Madawa ya Kulevya na hivyo tunaona amelivalia njuga barabara. Na Mheshimiwa Waziri ameleeza nia ya Serikali kutumia njia za Kisasa kugundua maficho ya madawa ya kulevya.

Kambi ya Upinzani inapenda kuliweka wazi suala hili kuwa Madawa ya kulevya yanayotuathiri yanatoka nje ya nchi na wanaosafirisha ni baadhi ya viongozi na wafanya biashara wakubwa. Wananchi zaidi ya asilimia 98 ni walala hoi ambao hawawezi hata kupanda ndege kwani ni fukara sana. Tunachokisema, Viongozi na baadhi ya wafanyabiashara wakubwa waache biashara hii ili Taifa letu lisiangamie.

Mheshimiwa Spika, mlalahoi hawezi kuwa na *diplomatic passport* wala hawezi kupitia *VIP* kwa taarifa tulizonazo ni kwamba hawa watu wa madawa ya kulevya hawakaguliwi wala kuulizwa wanakokwenda na wala wanakotoka kwa sababu ushirikiano walionao na baadhi ya wakubwa wakiwemo polisi. Ndiyo maana utasikia madawa ya kulevya yamekatwa, mitambo ya kutengeneza madawa imekamatwa lakini masuala haya yanakoishia wanajua polisi na Viongozi wa ngazi za juu. Hii ni kashifa kwa Taifa kama Tanzania lenye ustaarabu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mtambo wa kutengenezea madawa ya kulevya ulikamatwa Dar es Salaam na vyombo vya habari ziliripoti kwa muda mrefu sana lakini mpaka sasa hivi hatujajua hatima ya kesi hiyo imefikia wapi. Kwa hiyo, tungeomba Kambi ya Upinzani ipate maelezo ya kutosha juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Waziri kueleza umuhimu wa vyombo vya dola kama Polisi na Mahakama kushirikiana ili kesi za madawa ya kulevya ziishe mapema, Kambi ya Upinzani inauliza ushirikiano huu maana yake nini? Ushirikiano ndiyo umesababisha madawa kuingia ndani ya nchi. Sisi tunasema kila kitengo kifanye kazi yake kwa muda unaotakiwa kwa usahihi umakini na mianya ya biashara hii, huenda ikapungua. Ushirikiano kwenye madawa ya kulevya maana yake ni rushwa.

Mheshimiwa Spika, tunatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kununua jengo liliko Dar es Salaam ili liwe Makao Makuu ya Jeshi la Magereza, Ujenzi wa nyumba 47 za Askari wa Vyeo vya chini, na nyumba 10 za Maaofisa zilizonunuliwa kutoka *ATC* ya zamani.

Kwa upande wa Jeshi la Polisi, nyumba 48 za *FFU* Ukonga, 53 *FFU* Chake Chake Pemba na Ujenzi wa nyumba za Askari Mwanga na Nkasi ukiwa unaendelea.

Tunaomba ari hiyo iendelee zaidi. Pamoja na pongezi hizo, nyumba zenyewe ziwe za kudumu na sio baada ya miaka miwili, ukaanza kutuletea taarifa kuwa nyumba hizo ambazo tunazisifia leo zikawa magofu kama sio za muda.

Vile vile, tunatoa pongezi kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama za Mikoa kwa kuwa karibu na raia mipakani katika jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao. Tunaomba zoezi hili liendelea haswa Mikoa ya Kigoma, Kagera ambako hali si swari sana. Vile vile tunatoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutoa ajira kwa vijana na kama ilivyo katika maelezo yake, anatarajia kuajiri vijana wapatao 2,000. Lakini uajiri huu mara nyingi huwa sio wa wazi kwa wanachi. Hivyo basi, tunategemea kuwa utaliweka wazi suala hili ili wananchi wasio na ndugu za wakubwa wapate angalau nafasi ya kujiunga na Jeshi hilo la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ukaguzi wa wawekezaji kutoka nje, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba hivi sasa Serikali inatambua kuwa kuna wawekezaji uchwala. Pamoja na kusema kwamba kuna Watumishi kutoka vyombo vya Ulinzi na Usalam katika Balozi zetu wanawachunguza hawa wawekezaji, hatuamini kama kweli ni wafuatiliaji hasa wawekezaji barabara. Tusije kuwa na wawekezaji uchwala. Kwa mfano, kuna mwekezaji aliyeingia hapa nchini zaidi ya miaka 6 iliyopita kuanzisha Kiwanda cha *Fumigation.* Mpaka sasa hivi hakuna cha Kiwanda wala Kampuni ya *Fumigation* wala kampuni hiyo na sasa hivi biashara yake ni ya kuuza Urembo.

Sasa je, mtu kama huyu utampaje *working permit Grade A* na je, kweli Balozi zetu zinafanya uchunguzi wa hawa wawekezaji? Suala hili, tuwaachie wananchi kwa kuisadia Serikali kwa kutoa taarifa pale watakapo bainisha kwamba mwekezaji ni mhuni taarifa iandikwe magazetini na isipite miezi miwili kabla Serikali haijatoa tamko kuhusu hili suala tangu litolewe magazetini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna wanausalama katika Wizara mbalimbali. Lakini sio kweli kwamba hawa wanausalama wanafanya kazi katika Wizara mbali mbali. Utasikia kila kukicha, fedha za Serikali zimepotea na karibu kila Wizara imeisha kumbwa na wimbi hili au wanafanya nini? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba ni ubadhirifu gani hawa wanausalama wanasaidia katika Wizara. Tunashauri Jeshi la Polisi katika zoezi hili liwaajiri wataalam ili wafichue siri na sio uhalifu tu bali pia na ubadhirifu katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kuna zoezi la kupiga kura kwa Siri kubaini majambazi, bado tunaona kazi haijafanyika. Mara nyingi tunasikia zoezi hili na wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba hata wakipiga kura, utekelezaji wake ni wa hafifu sana na ndiyo unaosababisha wananchi kuchukua uamuzi mikononi wa kupiga na hata kuuwa wahalifu na majambazi. Hii inaonyesha kwamba zoezi hili halitekelezwi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, cha msingi Mheshimiwa Waziri, angalau baada ya miezi sita, kura zipigwe katika jamii na utekelezaji ufahamike kwa wananchi. Wananchi wengi sasa hivi wamepoteza imani na Polisi kwani matukio ya uhalifu mara nyingi

yanawahusishwa na baadhi ya polisi na wakati mwingine utakuta gofu ambalo tunategemea ndiyo inafanya *patrol* inasindikiza mali za wizi. Je, wananchi wafanye nini katika hili mara linapojitokeza?

Mheshimiwa Spika, kila binadamu anayo haki ya kuishi na tunapenda kuunga mkono hili zoezi la kupiga marufuku watu wanao uwawa kwa imani za uchawi au ushirikiana. Suala hili sasa hivi lisipoangaliwa na kufanyiwa utafiti wa kina, huenda tukauwawa kama mchwa siku za usoni. Tunaomba mbinu zote zitumike sio tu viongozi wa siasa bali Wakuu wa madhebu mbalimbali, viongozi wa Serikali, na hata viongozi wa kimila.

Mheshimiwa Spika, lengo liwe la kutokomeza imani hii ya kishirikina. Vile vile, tunatoa pongezi kwa Mikoa ya Kusini kwa kupunguza ajali barabarani baada ya kuanzisha zoezi la kuweka askari ndani ya mabasi ya abiria isipokuwa, naomba Mheshimiwa Waziri achunguze vyanzo vya ajali hizo. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri barabara zetu zinakuwa mbaya, inawezekana kabisa kwamba anaweza akafanya kosa kutokana na kwamba kule mbele anakuwa haoni kutokana na hali barabara ilivyo.

Pia kuwe na uchunguzi wa makini kuhusu madreva wanaotumiwa na wapelekwe shule pia ili kuhakikisha kwamba madreva hao wanakuwa na uzoefu wa kutosha na tabia ya kumweka dreva mmoja kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza iachwe mara kwa sababu hiyo ndiyo pengine inachangia kuleta ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba Mahakama zetu zina upungufu wa Mahakimu lakini sio sahihi kwamba Mahakimu ndiyo wanaochelewesha kesi. Mara nyingi sababu zinazotolewa ni kwamba upelelezi bado haujakamilika. Wakati huo huo, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba upelelezi unakwama kutokana na mazingira na shauri lililohusika na wala sio mwelekeo wa rushwa. Ni ukweli usiofichika kwamba wapelelezi wanapata shida sana kupata habari na hii pia inachangia kwamba jeshi la Polisi lina wapelelezi ambao hawatoshi. Ningeshauri kwamba suala la Chuo kilichokuwa kinategemewa kujengwa hapa Dodoma siku za nyuma nadhani kifufuliwe, matumaini ya kujengwa Chuo hiki kuongeza vijana wa upelelezi ili kazi za upelelezi zifanyike haraka kuliko kuweka kesi kwa muda mrefu bila sababu.

Mheshimiwa Spika, tunatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kuwa na nia ya kununua *Speed Boats* kwa ajili ya doria majini na juhudi zake za kufanya mawasiliano ya jinsi wanavyoweza kuwa na mfumo wa pamoja kutumia shughuli za Jeshi la Ulinzi, *TRA* na Maliasili ili kuziba pengo kwa sasa ambapo fedha bado hazijapatikana.

Mheshimiwa Spika, tunashauri kwamba Serikali ajaribu kutafuta wafadhili na pengine tatizo hilo laweza kutatuliwa. Vile vile tunapongeza utekelezaji kwa awamu uboreshaji wa mazingira mazuri ya kazi ili vyombo vya Ulinzi na Usalama vikabiliane na tishio la ujambazi. Pamoja na pongezi hizo, kwa awamu zilizopita Mheshimiwa Waziri namwomba ajitahidi kuongeza bidii zaidi ili angalau mwakani tuje tusikie jambo jipya katika hilo.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, tunafurahi sana kwamba ameelewa baada ya kufanya utafiti wa kina chanzo cha uhalifu nchini. Hii inaonyesha picha nzuri tu katika Jamii lakini hakueleza jinsi ya kupunguza makali ya vyanzo hivyo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aeleze angalau jinsi ya kutatua vyanzo hivyo vya uhalifu kwa sababu tafiti zote lazima ziendane na ufumbuzi au mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka 2002/2003, Serikali ilichukua hatua kwa kutenga shilingi milioni 389,580,000 kwa ajili ya kilimo Magereza. Fedha hizi zimeagizia matrekta 10 pamoja na zana zake muhimu kama majembe, *haro* na *trailer*.

Vile vile viwanda vilipata shilingi milioni 90,000,000 ili kuboresha na kufufua viwanda vya Ushonaji kutengeneza Sabuni sehemu mbali mbali hapa nchini katika Jeshi la Magereza. Tunadhani Waziri amefanya kazi nzuri na ya kimaendeleo kwani Magereza si sehemu ya kulisha na kulazwa tu watu bila kazi bali pawe ni sehemu ya uzalishaji ili iongeze Pato la Taifa. Pamoja na hayo, tuligetemea Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba kwa mwaka uliopita Magereza ilizalisha tani ngapi za mahindi, mchele na maharage ili angalau tungeweza kutafuta soko nje kwa ajili ya kuongeza pato katika Jeshi la Magereza na nchi nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na uboreshaji wa Magereza, tunatoa pongezi sana kwani Mheshimiwa Waziri ameeleza viwango mbali mbali vilimofikia na mpaka sasa hivi zoezi hilo linaendelea Vizuri. Bila shaka yale mabomba ya zamani yaliyooza na hivyo kuvujisha maji machache tuliyonayo yarekebishwe, pia vyoo na bafu vinahitaji kufanyiwa marekebisho. Vile vile, tunatoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwasitiri wafungwa ili wasiadhirike kwa kutoa sare, virago, mablanketi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kwamba kuwa mfungwa sio kumnyiwa haki za binadamu. Pamoja na pongezi hizo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya hivyo bila kusita.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi, kuna wingu kubwa sana la kutoa uraia Watanzania kwa watu mbali mbali wanoomba uraia Tanzania. Tunaomba hili suala lisiachiwe mtu mmoja ambaye ni Waziri bali pawepo na kamati maalum ya kupitisha uamuzi huo baada ya uchunguzi wa kina. Pamoja na hayo, kuna watu wanaitwa wataalam wa kigeni ambao wanapewa vibali vya kuishi na kufanya kazi nchini. Watu hawa si wataalam wote tunavyojua sisi tunapotembelea sehemu mbalimbali haswa haya makampuni ya Kigeni. Hali hii inapelekea Watanzania wengi kukosa ajira bila sababu.

Pamoja na kwamba vibali vinatolewa baada ya *TIC* kutoa taarifa, hii ina maana kuwa *TIC* haina wataalam wa kuchunguza hawa wageni au haifanyi utafiti wa kutosha. Nimewahi kuona Kampuni ya Kigeni imemuajiri mgeni kama Mkurugenzi wa Fedha. Hivi ni kweli hatuna Watanzania wanaoweza kazi hii? Tunachosema ni kwamba tuwape wananchi au wafanyakazi nafasi kwanza pale patakapotokea mgeni asiyeweza kufanya kazi yake kama ilivyoainishwa katika kibali chake cha kufanya kazi, taarifa itolewe

magazetini na Uhamiaji wafuatilie suala hili kwa muda angalau siku 60 na taarifa iwe imetolewa kwa muda huo na siyo vinginevyo. Hii inatokana na *TIC* na Wizara ya kazi kutofanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la rushwa katika Idara hii ya Uhamiaji. Tunaeleza kwamba kuna mikakati imewekwa kwa ajili ya kukomesha tatizo hilo. Lakini, Mikakati hiyo haitafanikiwa iwapo watendaji hao hawatapewa elimu na kuwafahamisha madhara ya rushwa. Rushwa hiyo ndiyo inayofanya watumishi wa Idara ya Uahamiaji kutoa *passport* hata kwa watu wasiofaa kuingia nchini. Hivi karibuni, tumejionea wenyewe majambazi waliowauwa askari polisi wetu. Watu hawa (majambazi) inawezekana kabisa wameingia nchini wakiwa na *passport* za Tanzania, idara hiyo ifuatilie kwa makini wapi walizipata *passport* hizo na nani aliruhusu kutoa *passport* hizo? Na iwapo itabainika ni nani hatua za kinidhamu zichukuliwe mara moja na riporti hiyo itolewe haraka sana.

Mheshimiwa Spika, tunatoa pongezi kwa kuwarejesha baadhi ya wakimbizi kama wa Rwanda na Burundi makwao lakini bado juhudi zinahitajika ili Tanzania isiwe na wakaimbizi wengi. Tunaomba Marais wa Bara la Afrika husuan Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Kongo na Burundi waongeze kasi ya mazungumzo ili mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yakomeshwe mara moja. Kwa sababu hilo ndilo tatizo kubwa linalosababisha kuendelea kuwa na wakimbizi katika nchi hizi sasa hivi, Tanzania. tatizo hilo ndilo linalosababisha kukua kwa ujambazi wenye kutumia silaha kali kama *SMG* na bastola.

Mheshimiwa Spika, wakimbizi wanaoingia nchini kwa ajili ya hifadhi, wadhibitiwe wasitoke ovyo kwenye Makambi yao. Watokapo, wasachiwe na waingiapo pia wafanyiwe hivyo hivyo. Ni heri ya lawama kuliko fedheha tunayoipata sasa hivi. Serikali sasa hivi ijaribu kuwadhibiti kwa nguvu wakimbizi hao wakorofi. Aidha, ushawishi wa kuwarudisha wakimbizi makwao uimarishwe zaidi ili warudi makwao kwa hiari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Polisi na mafunzo ya awali ni kimoja Tanzania nzima, jambo hilo linatia shaka kama kweli tunaweza kupata askari wengi kwa kutegemea chuo kimoja, kwa maana hiyo tunashauri kuwa kijengwe chuo kingine na ikiwezekana vipatikane vyuo vingine viwili ili kukidhi mahitaji ya askari polisi nchini. Kwa mfano, wananchi walihamasishwa kujenga vituo vya polisi *(Police Post),* lakini vimekosa askari wa kukaa hapo kituoni kisa ni kukosa askari.

Mheshimiwa Spika, jambo hili inawezekana limewakatisha tamaa wanachi wengi waliokuwa wako tayari kuchangia ujenzi wa vituo hivyo hasa nyakati za usiku aidha kama askari atakuwa kwenye vituo hivyo, basi wawili yaani mmoja mchana na mmoja mwingine usiku. Hata hivyo, askari kama binadamu huwa wanajifungia ndani ya vituo hivyo kwa kuhofia maisha yao kwani wanalinda wakati mwingine bila hata silaha. Hii, inawakatisha tamaa hata walinzi wa sungusungu ambao hupenda kuongozana na askari. Ukizingatia kuwa wezi wa siku hizi huja na silaha kali kali kama vile wapo vitani. Kwa maana hiyo, kuongezeka kwa vyuo nchini kutasaidia upatikanaji wa askari wengi na

ulinzi wa maeneo mbali mbali utafanikisha hali hii iendane na upatikanaji wa silaha za kutosha wa kutumia askari wetu watakaopangwa vituo vya Polisi, *Police Post.*

Mheshimiwa Spika, hatua za kinidhamu na kisheria zinazochukuliwa dhidi ya askari wachache ambao kwa namna moja au nyingine wamejihusisha na makosa mbali mbali hairidhishi na inatia shaka au walakini sana. Pamoja na kwamba hiyo imeelezwa kama kuweka jeshi la polisi kama Chuo safi cha Serikali Je, hatua za kinidhamu zinazochukuliwa ndiyo hii ya kuhamisha askari anapoharibu hapa na kumpeleka sehemu nyingine akaharibu? Au hatua hizo kwa sababu askari wa cheo cha chini, tunaona wanaachishwa kazi na sio wakubwa. Hivyo tunaomba tuanzie kwa wakubwa ndipo nidhamu itatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 makadirio ya maduhuli ilikuwa ni shilingi milioni 485,509,804 na hadi kufikia mwezi Aprili, 2003 uliweza kukusanya jumla yashilingi bilioni 3,531,098,300 ambayo ni takriban asilimia 81. Hii ni dalili nzuri, tujiulize asilimia 19 ambazo hazikuweza kupatikana, ilikuwa ni kwa sababu gani? Kwa hiyo, tunamshauri Mheshimiwa Waziri afanye utafiti wa kutosha ili angalau kipindi hiki kinachokuja kipatikane angalau 100% ziweze zipatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waipitishe Bajeti hii kwa sababu hata mimi kama Waziri Kivuli imenifurahisha, ili iweze kufanikisha mambo yote. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu ni ule ule kwamba wale ambao hawajachangia hata mara moja ndio wanapewa nafasi ya mwanzo, kuwatendea haki. Wengine waliacha Wizara nyingine wakisubiri hii. Kwa hiyo, wanapewa nafasi mwanzo na wapo 17. Kwa hiyo, siku ya leo yote ni wale ambao hawajachangia hata mara moja. Aliyekwisha kuchangia asitegemee kuitwa. Mchangiaji wa kwanza leo ni Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa George Lubeleje, hao ndiyo wanne wa mwanzo. *(Makofi)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nitoe mawazo yangu katika hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Mkutano huu wa kumi na mbili. Naomba nami niungane na wenzangu walionitangulia kuwapongeza Wabunge wote waliofanikiwa kupita katika tanuri la uchaguzi wa hivi karibuni na kufaulu kuitwa Waheshimiwa Wabunge. Wote kwa ujumla wao nawapa hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri na yenye kutia matumaini. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali tuliyo nayo ya usalama wa raia na mali zao ni ngumu. Sidhani mtu yoyote atasita kuelezea hali ilivyo sasa kuwa uhalifu katika jamii umefikia

kiwango cha kutisha. Wizi wa kutumia silaha yaani ujambazi, wizi wa fedha, upakaji na mauwaji yamekuwa ni mambo ya kila sika. Wahalifu wanachekelea na kusherehekea jinsi wanavyotumia kila mbinu kuwapiku askari polisi. Kwa mfano, Dar es Salaam sio Bandari Salaam siku hizi. Watu roho ziko mkononi, mategemeo yao ni kuwa hatua kamambe zilizoelezewa katika hotuba kwamba zimeanza kuchuuliwa zitaleta matunda ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Jeshi letu la Polisi kwa jinsi linavyokabiliana na uhalifu na majambazi wakiwa wao wenyewe wanahatarisha maisha yao. Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hawana vitendea kazi vya kutosha na maslahi yao ni duni. Lazima juhudi za ziada zielekezwe kuboresha uwezo wao wa kazi, wapatiwe vitendea kazi vya kutosha na maslahi yao yaboreshwe kwa kiwango kikubwa. Wanahitaji utaalam wa kisasa kudhibiti uhalifu kwani wahalifu wamekuwa wanabuni mbinu mpya kila wakati. Uwezo wao wa upelelezi na kuendesha mashtaka lazima nao uimarike. *(Makofi)*

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2000 ilitamka wazi kuwa jukumu la ulinzi na usalama wa wananchi ni wananchi wenyewe. Kwa maana hiyo ulinzi na usalama si jukumu la majeshi ya Ulinzi na Usalama peke yao lazima majeshi yapewe ushirikiano wa kutosha na wa dhati kabisa kutoka kwa wananchi nalitegemea Jeshi la Polisi kuwa ni rafiki na kimbilio la raia wema na kiboko kwa wahalifu. *(Makofi)*

Lakini urafiki huo wakati mwingine unapotoshwa kuwa urafiki wa binafsi na wa kulindana badala ya kuwa urafiki kwa jamii nzima. Urafiki huo binafsi unatumiwa vibaya na baadhi ya watu kuwatishia wenzao katika jamii na mbaya zaidi baadhi yao wanaruhusiwa kumiliki silaha ambazo wanazitumia kutishia raia na kutamba kwamba hakuna litakalowapata kwani wanalindwa na wakubwa katika jeshi la polisi. *(Makofi)*

Hali hiyo imetokea katika Jimbo langu la uchaguzi Gairo. Kuna mhusika ambaye viongozi katika jeshi la polisi wanamfahamu. Amekuwa anatumia urafiki au tuseme kufahamika kwake kwa viongozi wa polisi vibaya. Lakini baya zaidi malalamiko dhidi yake yalipofikishwa kwa viongozi wa Serikali yalipuuzwa na kuonekana kuwa ni uzushi, majungu na kumvunjia hadhi.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha zaidi, baadhi ya askari polisi wanashirikiana na wahalifu, wanawafahamu na wakati mwingine unaweza kujenga hisia kwamba wanapata mgao wa mali iliyoporwa na wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walioruhusiwa kumiliki silaha wakigundulika wanazitumia vibaya, kuwatishia wenzao au kwa uhalifu wa aina yoyote, wanyang'anywe silaha hizo mara moja na kamwe wasiruhusiwe kumiliki silaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umma wa Watanzania umekuwa unaelimishwa ili uzidi kushiriki katika ulinzi na usalama wa umma na wao wenyewe kujisaidia, vikundi vya ulinzi wa umma kama sungu sungu, wasalama, mgambo, vimekuwa vinatakiwa kushirikiana na vyombo vya dola. Lakini la muhimu kabisa ni kuwepo kwa mwongozo

ulio wazi na usimamizi imara juu ya jinsi vikundi vya ulinzi hivyo vitakavyoshirikiana na vyombo vya dola bila ya hivyo kitakachotokea ni vurugu na wahalifu watajiingiza katika vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilikabiliwa na kijana ambaye yumo katika kikundi kinachojiita *Chawamata Public Security and Environment Committee* kilichoko Kinondoni Dar es Salaam, akanitaka niingie nao mkataba wa kunilindia nyumba yangu ya kuishi Dar es Salaam kwa malipo ya shilingi 60,000/= kwa mwezi. Nilistuka, je, hivyo ndivyo vikundi vilivyoundwa kuitikia wito wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam? Wa huduma za ulinzi wa jamii Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe ufafanuzi juu ya uhalali wa vikundi kama hivi kama siyo vikundi vya wezi.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika jeshi la Polisi ni kero kwa wananchi. Kinachokatisha tamaa ni kwamba ushirikiano uliopo kati ya wananchi ambao ndiyo wanaowajua wala rushwa wakati mwingine ni geresha tu. Kuna kulindana kwingi na hasa kwenye *Grand Corruption,* baadhi ya watoa habari za kweli yaani wanaoitwa *Genuine Whistle Blowers* hawalindwi bali husakamwa na hata kushukiwa kwamba ni wapika majungu tu wanaotaka kuwakomoa watendaji bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii inakatisha tamaa kama kweli Serikali imedhamiria kupiga vita rushwa na mimi naamini imedhamiria, basi tuone kwa vitendo kuwa utambuzi wa wala rushwa unaimarika na hatua za haraka zinachukuliwa kuwadhibiti. Lazima imani ijengeke kati ya wananchi na vyombo vya dola vinavyopambana na rushwa. Tukumbuke imani huzaa imani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magereza, nina moja tu. Mbanano wa mahabusu katika magereza yetu kama ilivyo katika gereza la Keko na Gereza la Butimba, Mwanza na magereza mengine ni tishio la afya ya mahabusu.

Mheshimiwa Spika, Ukimwi unaenezwa kwa kasi sana katika mazingira hiyo. Kwa nini wahalifu wadogo wadogo wasiwekewe utaratibu mwingine badala ya kulundikwa mahabusu? Kwa nini, wafungwa wasitumiwe katika kazi za kupanua majengo ya magereza na kuongeza majengo ya magereza. Maana majengo ya magereza mengine yako vile vile tangu wakati wa ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie kidogo wafanyakazi wa Uhamiaji. Nao warekebishe kasoro zilizojitokeza. Wageni wengi wameingia nchini na kuishi nchini kinyume cha sheria kama ilivyothibitika hivi karibuni jinsi majambazi na washirika wao kutoka nchi za kigeni walivyowaua askari polisi wetu mashujaa na mbwa wao Koplo. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Wema wetu umetuponza. Majambazi hayastahili hata kidogo kulindwa utu wao.

Mheshimiwa Spika, wema ukizidi ni ujinga. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kusema machache kidogo kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza labda niseme kwamba napenda nitumie fursa hii kutoa shukrani nyingi kwa wananchi wa Jimbo la Gando, ambao wamenichagua kwa kura nyingi tu kuja tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliochaguliwa hivi karibuni, wote kwa pamoja hasa hili kundi la Wazungu 15 tuliokuja kutoka Pemba kwa sababu tuliambiwa kule Pemba Waafrika hawatakiwi, inaonekana hawa ni Wazungu waliokuja hapa. Kwa kweli napenda kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa utangulizi huo sasa napenda niende moja kwa moja kwenye mchango wa Wizara hii. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo baada ya kuipitia inaonekana kama itatekelezwa inaweza ikakidhi haja ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niseme yafuatayo, kwanza, napenda nianze na suala la vitambulisho. Sheria ya Vitambulisho ilipitishwa na Bunge hili mwaka 1987 na inasikitisha kuona kuanzia hapo mpaka hivi leo ni *doldrum,* tunakwenda tu mara huyu, mara huyu, lakini bado vitambulisho havijatengenezwa. Sasa wakati muafaka wa vitambulisho umefika kwa sababu hiki kitendo cha majambazi kuwa wanaingia na kuweza kuwauwa vijana wetu ovyo ovyo, inaonyesha ipo haja sasa ya kuwa na vitambulisho tena kwa haraka sana. Hawa askari waliokufa hivi karibuni mmoja katika askari wale ni kijana wangu, mtoto wangu hasa wa Jimbo langu. Napenda kutumia fursa hii kutoa mkono wa pole kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando, kwa Mheshimiwa Waziri kutokana na vifo vya maaskari wote hawa.

Mheshimiwa Spika, napenda nije katika *agenda* ya pili niliyokusudia kuizungumza, nalo ni suala la *passport.* Inaonekana labda kuwa *passport* katika nchi yetu sijui ni *privilege* ambayo anaweza akaipata mtu fulani tu, kuna ugumu kidogo wa watu kupata *passport,* sisemi hawapewi lakini kuna ugumu. Kama Mheshimiwa Waziri atatoa takwimu hapa za Watanzania waliopata *passport* ukilinganisha na idadi ya Watanzania milioni 36, basi mimi nafikiri itakuwa ni watu kidogo sana walioweza kumiliki passport mpaka hivi sasa. Sasa hii inaonekana kuna ugumu na kuna ugumu kweli kwa sababu unaweza kwenda kujaza fomu ya *passport* vizuri tu lakini hivyo vikwazo utakavyopewa kwamba wewe unataka kwenda wapi? Au hebu tuletee *copy* ya tiketi unakotaka kwenda, kwa nini yawe yote haya? Nchi kama za Asia mtoto akizaliwa tu basi anaandikiwa *passport* yake kwa sababu ile ni haki yake. Sasa mimi nashangaa inafika wakati unasumbuka kwa jambo ambalo ni haki yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala la wafungwa na msongamano wa wafungwa. Kwenye Magereza yetu idadi kubwa ya watu wanaosongamana ni wale

ambao wanasubiri kesi.  Kwa bahati mbaya askari polisi hapa nchini ndio wao ambao wanashtaki, sasa inawezekana ikawa ni kesi ndogo tu lakini askari kwa sababu wao ndio wanaoendesha mashtaka wanamwomba Hakimu mrudishe mshtakiwa ndani kwa sababu upelelezi haujakamilika, tena inachukua muda mrefu sana upelelezi huu kukamilika. Sasa hii ni kama *contradiction* kwa sababu upelelezi ni kweli unachukua muda wote huo? Mtu mwenye kufanya kosa hasa inakuwaje askari wanapelelezi muda mwingi hivyo mpaka inapelekea mahabusu wanakusanyika ndani, wanasumbuka halafu inapelekea mpaka wanakufa.

Sasa mimi ningependelea nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba aandae namna ya askari hawa ambao ndio wanashtaki, waweze kuzimaliza hizi kesi kwa haraka ili yule anayefungwa afungwe na ambaye bado kesi yake haijakamilika basi apewe dhamana, awekwe nje ili isiwe ni mzigo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nije kwenye suala la askari.  Askari kidogo wana malalamiko sana na kwa sababu ni vijana wetu na tunakaa nao ndani ya mitaa tunawasikia wakilalamika.  Kule kwetu Zanzibar au labda niseme Pemba na Unguja, vijana hawa ambao ni askari huwa wanaoa mke zaidi ya mmoja, sasa kama akipata uhamisho wa kwenda sehemu nyingine basi Jeshi la Polisi linamhudumia mke mmoja tu na watoto lakini mke mwingine na watoto wanakuwa ni mzigo wake mwenyewe.  Mimi nafikiri ni vizuri Wizara ikaangalia juu ya jambo hili kwa sababu inaweza ikawasaidia hawa askari ili kuweza kupunguza matatizo kidogo.  *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili, kuna ile *ten percent* ambayo askari wanapewa kwa ajili ya *house rent.*  Hii ilianza mwaka 1988 na ilikwenda vizuri mpaka mwaka 1994, kwa mfano labda askari katika mshahara wake unampatia tuseme ten percent ya shilingi 1,500/= ilikwenda vizuri mpaka mwaka 1994 lakini kuanzia hapo imebakia *fixed* haiongezeki, japo mshahara unaongezeka lakini ile haiongezeki.  Hii labda pengine ni kutokuwa na fedha au ni vipi lakini naona Mheshimiwa Waziri amepewa fungu kubwa kiasi hiki basi ni vizuri akayatazama mambo haya ambayo yatawasaidia vijana wetu katika kupunguza malalamiko.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ninachotaka kukizungumzia hapa ni suala la mishahara.  Vijana wanaopelekwa kozi, wanakwenda kozi wanarudi lakini wakirudi ile mishahara yao mipya baada ya kupata mafunzo inachelewa kidogo na hii inaleta malalamiko.  Pengine si nia ya Mheshimiwa Waziri au ya Wizara kuwasumbua lakini labda urasimu unachukua muda mwingi.  Kwa ulimwengu wa leo ambao unaweza ukakusanya habari za nchi nzima katika *computer* moja tu, ni vizuri ukafanya kazi hii haraka ili askari anaporudi asisumbuke.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nizungumzie juu ya suala la hayo marekebisho yenyewe.  Marekebisho yenyewe ni kazi nyepesi tu, askari anaporudi kutoka kwenye kozi inajulikana askari wamerudi kutoka kwenye kozi mwezi gani, yanakusanywa majina yao yanapelekwa Hazina, sasa inakuwaje wanachelewesha mpaka wengine wanakufa?  Wanakufa kabisa hawajapata mishahara yao.  Sasa hii kidogo inasikitisha, anaona amekwenda kusoma lakini haoni faida ya ile elimu aliyoipata.

Mheshimiwa Spika, halafu ningependa nizungumzie kidogo kuhusu hawa askari pale anapokufa. Katika Wizara nyingine kwa mfano labda kule kwetu kama tulivyozoea sisi, mfanyakazi mwingine wa Wizara nyingine anapokufa basi yule kizuka aliyemwacha na watoto wanahudumiwa kwa muda kidogo mpaka pale ambapo kizuka anatoka pengine baada ya miezi minne ndiyo analipwa mafao yake na yanaweza kuwasaidia. Lakini kwenye uaskari si hivyo, akifa kama kipo chake kinaweza kutayarishwa akapewa lakini haionekani kuwa labda kuna fungu maalum la kuwasaidia hawa vizuka na watoto ili waweze kuendesha maisha katika kile kipindi kigumu cha msiba.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na kusema hayo napenda niruke hapo nije kwa askari ambao kwa bahati mbaya hivi karibuni waliuana kule Pemba. Wale askari walipelekwa kule Pemba na wako toka zamani, sasa mimi kidogo nina mashaka, sijui dhamira ni ipi kwa sababu kama ni uhamisho wa kawaida, kwa nini askari wale wote wamewekwa katika vituo viwili tu, Pemba kuna vituo vya maaskari, Basira kuna Kituo cha Maaskari, Micheweni, Konde, Kengeja na Mkoani lakini kwa nini wako Wete tu na Chake Chake?

Sasa ukifanya hivyo unawafanya askari iwe ni rahisi kugenge kama wanakusudia kufanya ubaya na matokeo yake ndiyo yale inafikia kuwa ni aibu kubwa kwamba askari wanapigana risasi wenyewe kwa wenyewe. Nipengenda kumwomba kaka yangu Mheshimiwa Waziri kwamba alitazame hili. Kama ni uhamisho wa kawaida basi *okay* awatawanye ili upungue uwezekano wa kugenge na kufanya vitendo vya ajabu ajabu. Juzi wameuana wao kesho kutwa pengine watakuja kumpiga Kamanda ije kuwa ni matatizo makubwa. Kama labda wanafanya hivi kuwa wamechoka basi wahamishwe, kwa nini wakae, wahamishwe tu warudi kwao ili waje waendelee na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nije kwenye sehemu ya muafaka. Katika muafaka Mheshimiwa Waziri kwa bahati nzuri yeye ni miongoni mwa wanakamati na yeye ni Mwenyekiti Mwenza, napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu nimpongeze kwa juhudi zake kubwa sana za kuhakikisha kuwa muafaka unatekelezwa.

Kwa kweli askari kule Zanzibar wamejitahidi sana kujirekebisha mpaka sasa katika hali mpya hii ya muafaka. Tumeliona hili katika nyakati za uchaguzi tokea kujiandikisha mpaka upigaji wa kura, sasa sijui kuwa ni kwa sababu huu ni uchaguzi mdogo au vipi, *you call spade a spade,* wamefanya vizuri kwa wakati huu, ni lazima tuwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini inaonekana Bara bado kidogo. Nyakati za kampeni kuna baadhi ya viongozi kwa vyama vingine wengine walikaribia hata kwenda ndani kwa kukamatwa na polisi.

Sasa mimi nafikiri tuwe *sober* kidogo kwa sababu wakati huu sio kuwa muafaka umefanywa Zanzibar tu, kweli muafaka umefanywa Zanzibar baina ya *CUF* na CCM lakini hata hivyo *CUF* na CCM wako nchi nzima na vyama vingine viko katika nchi nzima.

Sasa lile zuri ambalo linafanywa Zanzibar sioni tatizo kwangu mimi kuwa lisifanywe katika sehemu nyingine ya Jamhuri ya Muungano. Hii twasira ya kuwa askari wanakuwa *harsh* kwa upande mmoja na wanakuwa wazuri kwa upande mwingine inaleta sura mbaya kidogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nije katika sehemu ya uajiri wa askari. Napenda nitoe malalamiko kwa Mheshimiwa Waziri kuwa hasa kule kwetu visiwani *particularly* Pemba suala hili la uajiri bado halijawa na uwazi. Sijui kwa nini inakuwa hivyo kwa sababu *okay* inawezakana labda katika Wizara kuna watu wenye sifa fulani wanatakiwa lakini *why not* usifanye wazi?

Mheshimiwa Spika, Kenya wanapowataka askari wanatangaza kabisa redioni kwamba tunawataka vijana waliomaliza darasa la kumi na mbili wenye urefu fulani na wafike mahali fulani basi wanafanyiwa *interview.*

Sasa kule kwetu inaonekana kuna ugumu kidogo na watu wanalilalamikia sana suala hili. Pengine si agizo la Wizara lakini ni tatizo la watendaji na baya zaidi ni kuwa wanatumia baadhi ya askari wakubwa kuwaingiza jamaa zao zaidi na ndio ambao wanaofanya kiuvungu uvungu. Mengine ni aibu kuyasema sana hapa lakini mimi ningependa kumwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri, alitazame hili ili aweze kuyaondoa manung'uniko yasiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda niseme kuwa umekuwa ukijitahidi sana kutuelimisha sisi Waheshimiwa Wabunge hapa kwa namna mbalimbali, umetuandikia makala nyingi na pia umetupeleka wengine katika *institution* mbalimbali ili tujifunze kuwa Wabunge wazuri na wasemaji wazuri ndani ya nyumba hii. Inasikitisha sana mtu anaposema walimu au wafanyakazi wa *TES* walipwe, linakuwa ni kosa kubwa, anakuja mtu anatukana ndani ya Bunge hili na analindwa na wakubwa wa Bunge, mimi nafikiri tunaharibu heshima ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukalijengea heshima Bunge letu ili wananchi wanaotusikia wakaona kweli sisi ni watu wazima, *matured* na tumekuja hapa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wenyewe siyo kutukanana maneno ya ovyo, yanaangusha sana hadhi ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na mimi mwenyewe, tushirikiane katika kuipitisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ili haya aliyoyataka apewe na aweze kufanya kazi yake vizuri. Ahsante sana. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Napenda nikumbushe tu kwamba kanuni za Bunge zinamruhusu Mheshimiwa Mbunge yeyote siyo Spika peke yake, yeyote akiona mwenzake ametumia lugha isiyotakiwa, anasimama kuhusu utaratibu. Na wewe fanya hivyo safari ijayo. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Wawi, napenda kutoa shukrani kubwa sana kwako kwa kuniruhusu kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kukupongeza kwa kazi nzuri ambayo unaifanya ya kuliongoza Bunge hili bila kuchoka na uvumilivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii naomba ama napenda kumkumbuka Marehemu Dr. Omar Ali Juma, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi kwa sababu nakumbuka mwezi kama huu ndio ambao alifariki dunia. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kuchangia katika hotuba hii napenda sana kuipongeza Serikali ama kuipongeza Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, kwa kazi yake nzuri ambapo anaiongoza Wizara hii na vile vile Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati, kwa ushirikiano mzuri na Mheshimiwa Waziri na viongozi mbalimbali wa Wizara hii wakiwemo Makamanda, Makamishna, wataalam na vile vile askari. Napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika nchi yetu hii bila kuchoka usiku na mchana. Kwa hiyo, napenda kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nirudi kidogo kwa wenzangu wa upande wa upinzani. Toka tuanze kuchangia mimi sijawahi kuchangia ndiyo mara yangu ya kwanza.

Kwanza, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioingia katika Bunge hili katika huu uchaguzi mdogo hasa wa Waheshimiwa Wabunge wa Chama chetu cha Mapinduzi, napenda kuwapongeza sana.

Vile vile napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Upinzani katika kuingia humu kwa sababu ni demokrasia. Lakini napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Upinzani ambao wameingia humu kwamba, humu si sehemu ya kueleza maneno ambayo mtu anapenda kwa binafsi yake kusema tu, humu ni sehemu ya kushirikiana na kutoa maoni ya kuwasaidia wanachama wetu huko tunakotoka au wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimewaona viongozi wengi hapa wa Chama cha Upinzani wana midomo mirefu, wanapenda kuongea ongea mambo ya kukashifu kashifu, kwa hiyo mimi napenda kuwaonya kwamba siyo vizuri kuzungumza lugha zilizokuwa siyo rasmi katika Bunge. Kazi iliyotuleta ni kushirikiana, kusaidiana, kuheshimiana na kuiongoza vizuri nchi hii bila kuleta matatizo. Hivi sasa ni muafaka! Napenda kuwakumbusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kusema kwamba Pemba ni sehemu ya upinzani wala CCM hatuwezi kuongoza, mimi mwenyewe ni CCM nimeingia humu.

Napenda kuwaambia ya kwamba mwaka 2005 tutarudi sisi tuliokuja humu yaani Chama Tawala tutarudi sisi na wengine nyuma yetu wa Chama cha CCM tutarudi humu na ninyi mtabakia huko. Napenda kusema kwamba Pemba siyo Kambi ya upinzani, Pemba ni Kisiwa ambacho kinaongozwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Changia hoja, changia hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea napenda sana kuipongeza Wizara hii kwa kuzisikiliza hoja zetu za kuwapigania askari wa Zanzibar na askari wote wa Tanzania...

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuatana na Kanuni ya 50, *item* 8(a) inayosema: "Mheshimiwa Mbunge asitumie lugha ya kuudhi." Tunaomba Mheshimiwa Mbunge angefuta lile neno kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge hapa wana midomo mirefu. Midomo mirefu ni kwamba hatuna kipimo hicho hapa ndani ya Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Aah, lakini midomo mirefu ni neno la kawaida la kiswahili. Endelea Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea napenda kuipongeza Wizara hii kwa kusikiliza vilio vyetu sisi Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na askari hasa kule Pemba. Askari wa Pemba walikuwa hawana sehemu ya kukaa, askari wengi walikuwa wakikaa hata kwenye mahema, tukawa tunachangia hapa Bungeni kipindi kilichopita, Mheshimiwa Waziri ama Wizara ikaona kwamba ni kweli kwa hiyo wakawajengea nyumba 53 katika Kijiji cha Mfikiwa katika Jimbo langu la Wawi. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Wizara hii kwa ufuatiliaji wake wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kile Mheshimiwa Waziri alikuwa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, pia napenda kumpongeza kwa kuianza hiyo kazi na Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na wengine kwa kufuatilia. Napenda kuipongeza sana Wizara kwa kujali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumsifia Kamishna wetu wa Polisi Zanzibar kwa kazi yake nzuri ambayo anaifuatilia, mimi mwenyewe nilimwona kwa macho yangu akija kule Mfikiwa kuzitazama na kuzichunguza nyumba zile na kutupa moyo kwamba tayari sasa askari wetu watakaa sehemu ile kwa salama na amani. Tunapenda kuwapongeza sana kwa juhudi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kusema kwamba kuna mambo ambayo yameishafikishwa pale kama maji, napenda kulipongeza hilo. Lakini kitu kimoja ni

kwamba umeme bado haujafika. Napenda kuiomba sana Serikali kuwa ifuatilie kwa karibu sana kupeleka umeme pale kwa sababu huwezi kuwaweka askari kwenye giza.

Naomba sana umeme ufanyiwe haraka ili askari wetu wakati wakikaa wajisikie raha. Vile vile kuwe na miundombinu mbalimbali kama barabara, viwanja vya michezo, mambo ya vituo vya afya na pia *school* kwa sababu kile kitakuwa ni Kijiji. Kwa hiyo, napenda kuiomba sana Serikali ilifuatilie hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuhusiana na nyumba. Napenda kuzungumzia kidogo kuhusiana na nyumba hizi za *FFU* za Finya. Kwa kweli zile nyumba haziko katika hali nzuri kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba zitaendelezwa kujengwa. Lakini na mimi napenda kusisitiza kwamba zile nyumba zijengwe na kama kuna matatizo pale ya kujenga zile nyumba, basi waje waziendeleze kule kule Mfikiwa ili kuwe ni Kijiji, iwe ni Kambi ya Mapolisi kama tulivyozungumza kwamba askari si vizuri kukaa uraiani, akae kambini, basi wakiwa pamoja pale watakuwa ni ndugu na watafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuiomba Wizara au kumwomba Mheshimiwa Waziri kuhusiana na nyumba za Ma-*RPC* wetu wa kule Pemba. Ma-*RPC* wetu wanakaa nyumba ambazo si nzuri kwa kweli. Naomba sana na wao watengewe sehemu au wajengewe nyumba ambazo na wao waweze kujiona kwamba nao ni viongozi wa maaskari wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimalizia hapo naomba vile vile kuiomba Serikali kwamba zile nyumba zilizopo pale Madungu Chake Chake, zile ambazo ni za zamani toka enzi ya ukoloni, zifanyiwe ukarabati au napenda kuuliza tu kwamba wale waliopo pale ndio watakaoondoka kwenda kule kwa sababu naona askari ni wengi? Naamini sio wale na kama ni wale watakuwepo na wengine; je, zile nyumba zitafanywa nini? Kama ikiwa watabakia pale askari basi naomba nyumba zile zifanyiwe ukarabati, kwa kweli haziko katika hali nzuri pamoja na Ofisi Kuu, Ofisi ya Makao Mkuu ya Polisi Chake Chake.

Kwa kweli inafikia hatua mpaka mvua zikinyesha ile ofisi inavuja, basi itengenezwe. Kama kuna uwezekano kule nyuma iko sehemu nzuri ijengwe nyumba nyingine kubwa pale, basi mambo yatakuwa mazuri. Lakini utakuta Ofisi moja ina Maafisa hata watatu wanafanya kazi kwenye Ofisi moja, hiyo siyo nzuri. Kwa hiyo, naomba kama kuna uwezekano ikarabatiwe vizuri ile ofisi na vile vile iongezwe sehemu kubwa, liongezwe jengo pale Ofisi Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiondoka kwenye nyumba za askari napenda kuchangia kuhusiana na mishahara ya askari wetu. Kwa kweli askari wetu si watu ambao labda wanakaa tu yaani wako peke yao, wanakuwa na watoto na wake au waume zao. Kwa hiyo, wanategemewa, sasa mishahara yao ni midogo. Naomba sana mishahara ya polisi iongezwe kulingana na maisha. Maisha ya Tanzania kama tunavyoyajua, mtu anakuwa pengine ndiyo kama hivyo anakodi nyumba, anawasomesha watoto, matatizo ya maradhi lakini unakuta mshahara ukifika mwisho wa mwezi anakuwa hana chochote. Tunaomba sana mishahara ya askari iongezwe kutokana na jitihada zao ambazo wanazifanya na

kuilinda nchi ikawa ni nchi ya amani. Kwa kufanya hivyo tutawapa askari wetu moyo mzuri wa utendaji wa kazi na kuondoa rushwa. Wataondokana na rushwa kwa sababu mtu kama hana atakwenda kutafuta lakini kama anapata mshahara mzuri, ana chakula, anavaa vizuri na familia yake, basi atafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo napenda vile vile kuchangia kwenye sehemu hii ya matatizo ya kuwafunga vijana ama watoto magerezani na watu wazima. Kwa kweli naomba sana suala hili liondolewe, mtoto huwezi kumfunga pamoja na mtu mzima, mtoto ana pumzi zake na mtu mzima ana pumzi zake. Matatizo ya maradhi, watu wakiwa kule magerezani akili zao zinakuwa mbaya, akimwona mtoto anaweza akambadilikia, watoto wetu wanaathirika. Tunaomba sana kama mtoto amefanya kosa wawekewe magereza yao special, tunapenda kuiomba sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo naomba sana kuchangia kuhusu mambo ya ajira kwa vijana katika Jeshi la Polisi hasa kule kwetu Zanzibar kama Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kusema kabla ya mimi alivyozungumza. Mimi napenda kuchangia kwamba ajira kwa kule Zanzibar kwa kweli katika Majeshi haya ya polisi zipo, lakini kwa kweli kulingana na ukosefu wa ajira kwa vijana wetu, kwa kweli ni kidogo sana. Tunaomba vijana wetu wapatiwe ajira. Pengine kijana ana elimu yake lakini akifika anaambiwa mara ana matege au mara sijui ana kitu hiki. Kwa kweli hizi Sheria nyingine za askari ziondolewe, japo anakuwa siyo mtaalam lakini anaweza kulinda. Tunaomba sana hizi Sheria nyingine zipunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kusema kwamba hawa vijana ambao wataajiriwa, wawe ni vijana ambao ni wazalendo wanaoipenda nchi yao siyo kwenda kumchukua kijana ambaye si mzalendo, anaweza kuja akafanya mambo mengine baadaye. Kwa hiyo, tunawaomba vijana wetu wazalendo ambao wanaipenda nchi yao na wanajulikana, tunawajua katika Majimbo yetu wajiunge. Kwa hiyo, naomba sana hilo suala lifuatiliwe, hatutaki kuja kuuziwa nchi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuchangia kuhusu suala la ndoa kwa askari. Hawa askari wakiishamaliza mafunzo yao kama ni wanawake au wanaume, kwa kweli sisi ndio tunaotunga sheria lakini napenda kuiomba sana Serikali ilifuatilia hili, mtu anaweza akakaa miaka sita hajaolewa au hajaoa. Sasa kutokana na maradhi haya ya Ukimwi mtu hatakuwa hawezi kustahimili, hii Sheria ibadilishwe, mtu akiishamaliza kozi aolewe ama aoe, haina haja mtu akae miaka sita hajaoa au hajaolewa. Kwa hiyo, suala hili linadhalilisha sana. Twendeni na wakati tuachane na zile sheria za kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile, napenda kuzungumza kwamba kutokana na kazi nzuri ambazo wanazifanya askari wetu, naomba sana Mheshimiwa Waziri alifuatilie hili la kutoa mikopo kwa askari kwa sababu mtu inawezekana akakaa hana nyumba mpaka anastaafu lakini ikitolewa mikopo ya ujenzi anaweza akajenga nyumba yake wenyewe akajitegemea, akiishastaafu anakwenda kwenye nyumba yake kwa sababu zile nyumba za askari ukiishastaafu inakuwa si nyumba yako tena. Naomba sana mikopo kwa askari itolewe.

Vile vile na vifaa vya usafiri kama kule kwetu watu wanakaa mbali sana, mtu anakwenda kazini kwa baiskeli, askari anakwenda kwa baiskeli, anadhalilika au anapanda magari ya abiria, anadhalilika, mara anashushwa, mara hivi, inaonekana kwamba askari wetu wanadhalilika sana. Naomba sana mikopo tofauti itolewe kwa askari wetu ili kujijengea hatma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema hapa kwamba, askari waliopelekwa Pemba kwa ajili ya *operation* kutokana na machafuko ya kisiasa mpaka leo wako huko wanafanya nini? Mimi nakataa kwa sababu mimi pia ni Mpemba. Sisi tunafahamu kwamba Tanzania ni hii moja na hii Wizara ni ya Muungano askari anaweza kufanya kazi popote, sasa nashangaa mtu kusema kwamba askari huko wanafanya nini?

Mimi napenda kuwaambia kwamba askari wa Pemba wanafanya kazi, mimi ndiyo napenda kuwaambia hivyo na wanalinda amani ya nchi hii kwa sababu mambo yaliyopita waliyaweka wao sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba sana kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechaguliwa, tunawakaribisha sana katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi nzuri na hapa tulipo polisi ndio wanaotulinda. Kwa hiyo, pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri lakini bado wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, nami napenda niishukuru Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu mwaka 2002 ilikuwa shilingi bilioni 55 na sasa ni shilingi bilioni 70. Kwa hiyo, nina hakika wataboresha utendaji wao kwa sababu Bajeti imeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nianze na hili la usafiri katika vituo vyetu vya polisi. Pamoja na kufanya kazi nzuri lakini kama kituo cha polisi hakina gari askari wanafanyaje kazi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba nilimwandikia barua kwamba gari la Kituo cha Polisi Mpwapwa ni mbovu. Napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana *RPC* ambaye amefanya juu chini ili kuhakikisha kwamba gari hilo analitengeneza na sasa linafanya kazi. Lakini gari lile haliwezi kupanda milima, ni

mbovu kwa sababu Wilaya yetu ya Mpwapwa Vijiji vingi viko milimani. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alimwandikia barua *IGP* kwamba apeleke gari jipya Mpwapwa lakini gari hilo sijalipata mpaka sasa. Sasa naomba majibu kwamba kwa nini hili halikutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu magari katika Vituo vya Polisi maana gari linahitaji mafuta na matengenezo. Huwezi kumpatia *OCD* gari lakini hakuna fedha za matengenezo wala mafuta hata kama linatokea tukio la mauaji inabidi wananchi wachangie mafuta.

Mheshimiwa Spika, hivi ma-*OCD* kwa nini wasipelekewe mafungu yao Wilayani pale pale mbona Idara nyingine wanapeleka na hili ni agizo la Serikali kwamba fedha zote ziende Wilayani sasa ma-*OCD* kwa nini wasitengewe mafungu yao. *RPC* atakuwa anasimamia matumizi lakini ma-*OCD* wapate fungu kwa ajili ya matengenezo ya gari na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni nyumba za askari. Tangu nimeingia kwenye Ubunge mwaka 1990 wakati ule tunafanyia vikao *Karimjee Hall* suala hili limekuwa linazungumziwa kila mwaka Serikali ina mikakati, Serikali ina mipango, Serikali iko mbioni. Sasa ufike wakati suala hili litekelezwe. Hapa tumeona fedha za maendeleo karibu shilingi bilioni tano tujenge nyumba za askari. Ndugu zangu askari wanaishi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri ukipata nafasi utembelee nyumba wanazoishi Askari hapa Dodoma hasa zile za mabati *(full suit)* ni chumba kimoja *partition* unaweka pazia katikati. Kwa hiyo, ni vizuri tuweke mkakati wa kujenga nyumba za Askari na ni vizuri wakakaa mahali pamoja. Sasa Askari anakaa Makole, mwingine anakaa Chang'ombe utawapataje kama inatokea tatizo? Kwa hiyo, ni vizuri nyumba hizi zitengenezwe ili Askari wote wakae mahali pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini vitendea kazi ni muhimu hususani mawasiliano katika Vituo vya Polisi. Tunalishukuru sana Jeshi la Polisi kwa kusaidia vifaa vya kukamilisha jengo la Kituo cha Polisi cha Kibakwe na nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini kituo kile hakina simu ni vizuri basi kipate mawasiliano ya simu pamoja na Kituo cha Polisi cha Mtera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati kwamba iko haja ya kuanzisha Chuo cha Upelelezi. Mheshimiwa Waziri napenda nipate maelezo kwa sababu kulikuwa na mpango wa kujenga Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma, je, mpango huo umefikia wapi na kwa nini Chuo hicho hakijaanza kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna mlundikano wa mahabusu katika Magereza na suala la upelelezi ni taaluma huwezi kumchukua mtu yeyote tu kwenda kupeleleza kesi.

Kwa hiyo, Chuo hiki kitasaidia sana kuwaendeleza kitaaluma wapelelezi hawa. Naomba nipate maelezo kwamba Chuo hicho ambacho kitajengwa hapa Dodoma kitaanza lini na ni sababu zipi ambazo zimefanya Chuo hicho kisianze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni upande wa Magereza. Namshukuru na nampongeza sana Kamishna Mkuu wa Magereza amefanya kazi nzuri. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani nimeona kwamba ujenzi wa Gereza la Mpwapwa unaendelee. Gereza lile ni jipya kulikuwa na matatizo mengi sana hivi sasa wana mawasiliano ya simu, Kamishna Mkuu nakupongeza sana kwa hilo, lina usafiri wa kuaminika lakini bado tuna tatizo kubwa la umeme. Jana nilikuwa na Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Mpwapwa alinihakikishia kwamba mna mpango wa kupeleka umeme pale, nakushukuru sana kwa hilo.

Hivi sasa wafungwa wanatumia taa za mkono ambazo huwa zinatoa moshi na kusababisha air *pollution* kwa hiyo badala ya wafugwa kuvuta oxygen wanavuta carbon monoxide ambayo ina madhara makubwa sana kwa afya zao. Kwa hiyo, Kamishna Mkuu naomba suala hilo litekelezwe ili tuweze kupata umeme katika Gereza letu la Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu ni haya, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mussati, ohoo, amekwenda Mtera? Aah, yupo. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Nimesimama.

**SPIKA:** Ameshapanda ngazi, sasa namwona. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuongea machache.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wakazi wa Jimbo la Kasulu Mashariki, naomba kuwapongeza Wabunge wote wapya wa CCM na *CUF* ambao wamejiunga nasi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee juu ya Vituo vya Polisi ambavyo viko mpakani hasa katika Jimbo langu la Kasulu Mashariki kuna Kituo cha Heru Ushingo ambacho kiko karibu kabisa na mpaka wa Burundi lakini kina askari watatu au wanne tu, kina *radio* ya mwaka 47.

Pamoja na kwamba kiko mpakani ili kuwe na mawasiliano na Kasulu au na Kituo cha karibu inabidi Mkuu wa Kituo atembee kama maili tatu akapande kilima halafu pale juu ya kilima apande juu ya mti ndio aweze kuwasiliana.

Mheshimiwa Spika, nilimkuta mzee mmoja ambaye ndiyo Mkuu wa Kituo ana miaka kama 50 hivi kwa kweli alikuwa analalamika sana na hana hata baiskeli. Sasa inapotokea dharura mnaweza kuelewa inafanyikaje sasa kwanza umri mkubwa halafu inabidi atembee kama kilomita tatu au nne kwenda kutafuta mawasiliano kwa kupanda mti na umri mkubwa hivyo, ni mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Kituo hicho sehemu ya karibu ni kituo kikubwa cha Makere pana umbali kama kilomita 50 na njia hiyo ndio njia wanatumia Ninja. Ninja ni hawa watu wanaofanya ujambazi na hasa katika nchi ya Burundi.

Sasa kutembea katika eneo la namna hiyo ni hatari kubwa sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie kituo hiki kwanza tupate redio ya kisasa vile vile tupate usafiri kama inawezekana tukapata gari tutashukuru sana lakini endapo itashindikana kupatikana gari basi hata pikipiki.

Vile vile tunaomba tuongezewe Askari, kituo ambacho kiko karibu na mpakani wakimbizi wengi wa kutoka Burundi wanaingilia pale na vitu wanavyovijua ikiwa ni pamoja na silaha lakini wanaoweza kuwakagua ni askari 3 ambao hawatoshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeshukuru kama Mheshimiwa Waziri angeangalia uwezekano wa kuwapa posho maalum askari wanaokaa maeneo ya namna hii. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na ya hatari. Madaktari wanapewa posho inayoitwa *Risk Allowance* askari hawa wanaokaa maeneo hayo magumu ya kupambana na majambazi na wakimbizi wanastahili kupewa hiyo *Risk Allowance.* Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hali ya wakimbizi Mkoani Kigoma. Suala hili ni suala zito sana. Naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba *ration* ya wakimbizi kuanzia mwaka jana katikati imepunguzwa kwa kiasi cha nusu na Mkoa wa Kigoma mwaka huu kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka mingi tumepata matatizo ya mvua kwa hiyo, tuna upungufu wa chakula.

Kama *ratio* ya wakimbizi imepungua na chakula cha wananchi kimepungua nina uhakika mwaka huu tutapata matatizo makubwa. Wakimbizi hasa wa Burundi ni rahisi kuchanganyika na Waha kwa sababu tunaongea lugha moja na watavamia chakula cha wananchi na hivyo tutapata matatizo makubwa sana.

Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kusaidia kuwarudisha makwao wakimbizi hawa. Kutegemea wakimbizi hawa watarudi kwao wao wenyewe sio rahisi kwa kweli tunaomba warudishwe kwao haraka iwezekanavyo na bila masharti yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu bidhaa zinazoingizwa mipakani kutokea nchi za nje. Sisi upande wa Kigoma tunapata vitenge kutoka Kongo na Burundi lakini vile vile zinaingizwa bidhaa kama sigara ambazo zina nembo ya *Sportsmen* lakini sio *Sportsmen* na kuuzwa hapa nchini kwetu na pia konyagi. Mali hii ni ile ambayo ina

ubora duni na inaingia kinyemela bila kulipiwa kodi inashindana na mali inayozalishwa hapa nchini na ushindani ambao sio halali. Kwa hiyo, tunaomba Jeshi la Polisi lisimamie sana hasa hasa mipakani mali hizi zisiingizwe kiholela na kuja kuua biashara ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la nne, mara kwa mara ninaposikiliza vyombo vya habari nashangaa kusikia Polisi wanatangaza kwamba wamekamata bangi au madawa ya kulevya na wanatoa thamani kwamba ni bangi ya shilingi kadhaa, madawa ya kulevya ya shilingi kadhaa inakuwa kama vile Jeshi la Polisi linafanya kazi ya *promotion. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani si vema kutangaza thamani ni vema kusema tu kwamba Polisi wamekamata kilo kadhaa za bangi, wamekamata madebe kadhaa ya gongo sasa ukisema kwamba wamekamata dramu kumi za gongo zenye thamani hii wananchi wanasema alaa kumbe kitu hiki kina thamani. Nadhani ni vizuri tuishie kusema kwamba tumekamata madebe kadhaa, tumekamataa kilo kadhaa basi tusitangaze thamani ili hata mtu aliyekuwa amelala asiamke na kujua kwamba kuna biashara inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, napenda kuongelea juu ya vitambulisho vya uraia. Kama nilivyokwishasema sisi Waha na Warundi tunaongea lugha moja. Mrundi aki-*cross* tu mpaka akaingia Kigoma kijiji chochote kile unamchukulia kama Muha. Sasa ni tatizo kubwa hasa ikizingatiwa kwamba hatuna vitambulisho vya uraia hata sisi, kwa kweli inasikitisha hata kusema, wakati mwingine mambo yakiwa magumu ndani ya nyumba unakwenda kwenye kambi ya wakimbizi unajiandikisha kama Mrundi na unaweza kupewa posho kama vile unga na maharage kwa sababu unachohitajika ni kusema mimi ni mkimbizi na lugha inayotumika ni Kirundi na unaongea Kirundi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba imekuwa tatizo kupata hivi vitambulisho vya uraia lakini tungeomba walau sisi tulioko mipakani tupewe kipaumbele ili tupewe hivyo vitambulisho vitusaidie. Vile vile suala hili litasaidia kiusalama akiingia Mrundi kama hana kitambulisho cha uraia tunajua huyo ni Mrundi na sio Muha lakini kwa sasa hivi ni Mrundi tu akiwa Burundi akivuka mpaka anakuwa Muha na hivyo ni Mtanzania. Ni tatizo kubwa sana namwomba Waziri aliangalie suala hili ili lipewe kipaumbele haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja na nawapongeza Wabunge wote wapya waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo na nawakaribisha ndani ya Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu pamoja na wataalam wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa amani na utulivu uliokuwepo nchini na hii inatokana na juhudi za wananchi wenyewe *the security of the people by the people for the people. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Mji Mkongwe, Jimbo ambalo ni moyo wa Zanzibar, uchumi wote uko pale. Kwa bahati mbaya mwaka 2002 nilizungumzia kuhusu Kituo cha Polisi cha Malindi kiko katika hali mbaya kinahitaji ukarabati, lakini nafikiri kutokana na ufinyu wa Bajeti mpaka leo ukarabati huo haujafanyika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akumbuke jambo hili na alikarabati jengo lile kwa sababu watalii, wafanyabiashara na viongozi wa nchi mbalimbali lazima wapite sehemu ile.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu *passport* za Kidiplomasia Zanzibar. Nimemwombea mke wangu nimeambiwa bado sheria haijafika hapa na Mheshimiwa Waziri alisema mke mmoja tu apewe na mimi mke wangu ni mmoja tu, lakini hakupewa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aipeleke sheria hiyo Zanzibar ili mke wangu maskini apate *passport. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu wizi wa Mabenki uliotokea mara mbili, tatu hapa Tanzania. Nashauri wenye Mabenki waimarishe ulinzi wao wasitegemee Polisi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifanye zoezi kama walivyofanya nchi za nje kwa mfano Marekani *Surrender the illegal weapon* ambapo watu wana-*surrender* silaha ambazo sio za halali. Wizara itoe changamoto hiyo kwa wananchi wote waliokuwa na silaha isivyokuwa halali wazirudishe bila kuulizwa swali lolote, nafikiri itasaidia kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifanye semina za Makamanda mara kwa mara za kuwaelimisha utawala bora na haki za binadamu. Naipongeza Wizara, Polisi waliosimamia uchaguzi mdogo wa Pemba japokuwa kulikuwa na fujo lakini walidhibiti uchaguzi ulikwenda kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ugaidi, gazeti la Rai la leo linasema: “Wafadhili Wakuu wa Waislam Wanafungisha Virago Dar es Salaam.” Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu hotuba yake imeelezea wazi kwamba suala la ugaidi halihusiani na dini yoyote, inatufurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu wengi wanafikiria kwamba ugaidi unaletwa na Waislam tu jambo hilo sio kweli, nalipinga. Sasa hivi Waislam wanaogopa hata kujenga misikiti kwa kuhofia kuonekana wao magaidi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake imeelezea vizuri kwa hiyo naomba ieleweke kwamba suala la ugaidi sio la Waislam mtu yeyote anaweza kuwa gaidi. Kwa mfano kule Marekani kuna watu wamelipua majumba ya wananchi wa kawaida na wamekamatwa ni Wamerekani wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza sana ulinzi uliopo hapa nchini na hasa Zanzibar na Tanzania ni nchi ambayo inakubalika Kimataifa kwa kuwekeza na hii inatokana na

juhudi za Jeshi la Polisi japokuwa wana vifaa vichache, wana matatizo mengi. Nampongeza sana Kamishana wa Polisi wa Zanzibar, Ndugu Khalid, mwaka jana nilimpongeza na haki yake mwaka huu nimpongeze kwa sababu anafanya kazi nzito. Vile vile nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwakamata wale majambazi walioua Polisi watatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi isipokuwa naunga mkono asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kama ambavyo wenzangu wameanza kusema naomba niungane nao kuwapongeza Wabunge wapya walioingia Bungeni baada ya kuchaguliwa katika chaguzi ndogo nikianza na wale wa Chama cha Mapinduzi, hongereni sana lakini pia wale wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa hotuba yao nzuri. Hotuba hii inatupa matumaini kutokana na jinsi ufafanuzi wake ulivyo unaonyesha bayana kwamba suala la utulivu na amani katika Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi linatiliwa mkazo na kwa hiyo kupitia utekelezwaji wa Bajeti hii linaweza likafanyika vizuri zaidi. Nawatakia kila la kheri na tutajitahidi kushirikiana nao kuona kwamba mambo yao au shughuli hizi zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kabisa ambalo nafikiri ni vizuri niliseme katika kuboresha hotuba ya Wizara hii, naomba nianze na suala la namna ya upatikanaji wa Askari. Wenzangu kadhaa wameshalizungumzia lakini naomba niliseme kwa maneno yangu kama ifuatavyo. Ni dhahiri kwamba vipo vigezo ambavyo vinaelezwa vya namna ya vijana kujiunga katika Jeshi la Polisi, wametaja elimu, vimo, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sina ubishi juu ya taratibu hizo nasisitiza tu kwamba zizingatiwe lakini nafikiri ule utaratibu wa namna ya kuanza kuwapata vijana hawa usianzie katika ngazi ya Wilaya uanzie chini kwa sababu nina hakika kama vijana hawa watachujwa au wanaotahiniwa kwa ajili ya nafasi hiyo wakichujwa kuanzia kwenye ngazi za chini kabisa kwenye mitaa au vijiji vyao itasaidia sana kufahamu au kuelewa nyendo, historia za maisha yao miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka katika miaka ya nyuma viongozi wetu mliotutangulia mlikuwa na msemo mnasema moyo kabla ya silaha. Kinachojitokeza ni kwamba inawezekana tunawaingiza vijana hawa kwa kuangalia kigezo ama hivyo nilivyovitaja au elimu peke yake matokeo yake sasa wanapoingia kwenye Jeshi hili na tunawapa mafunzo baadaye kwa sababu hatuna hakina na tabia zao ndio hao ambao tunasikia sasa matukio mengine mabaya yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, askari anatoka Amary kwa hasira zake anageuzia bunduki hiyo Askari wenzake na anawapiga risasi anawaua. Hiyo inaonyesha kiasi gani mtu huyu hakuwa mkamilifu ambaye anajitolea kweli kufanya kazi ya ulinzi na usalama wa raia na mali zake na kwamba tumeingiza mtu ambaye hatukuwa na uhakika naye juu ya mienendo yake. Lakini nafikiri kama kweli tutakuwa tumeanzisha kwa kupitia mahali anapoishi watu wale watakuwa wanajua wazazi wake, mwenendo wake akiwa shuleni mpaka umri huo ambao anahitaji sasa kujiunga na chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu chombo hiki ni chombo nyeti na shughuli hii tunayotaka kumpa Askari huyu ni shughuli nyeti. Kwa hiyo isingependekeza kama tutamwingiza kwa utaratibu ambao pengine unakuwa na kasoro matokeo yake anaingiza dosari nzima katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, uko ushahidi thabiti kwamba kwa kutofuatilia historia hizi wako watu wakati mwingine kwa kutumia nafasi wanajiunga sasa kwa kupitia watu wenye nafasi katika chombo chenyewe. Mathalani mtu anajiunga na Jeshi la Polisi kutoka Ruvuma kwa mfano lakini anakuja anajiunga Shinyanga. Anayemvuta pale unaweza kugundua kwamba ni mtu ambaye yuko tayari kwenye taasisi hii na kwa hiyo ameombwa na mtu wake au rafiki yake kwamba nisaidie kijana wangu huyu apate ajira. Hilo nalo linachangia sana katika kudhoofisha ufanisi mzuri wa kupata askari wazuri wa Jeshi hili. Hilo nafikiri ni jambo la msingi la kuanza kuchuja kuanzia ngazi ya chini zaidi kwa watu wanaowania nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka kuchangia ni suala la mafunzo. Nashukuru sana Waziri ameshalitaja na hata Kamati imeshatoa ushauri. Lakini mimi nataka kushauri kama ifuatavyo. Nashauri kwamba muda wa mafunzo ni mdogo sana miezi sita kwa kumfundisha askari ili awe mahiri nadhani hautoshi. Mapendekezo yangu ni kwamba askari hao wangefundishwa mwaka mmoja na nusu ingeweza kuwasaidia sana. Miezi sita ile ni ya kuondoa uraia, mwaka mmoja ule atazamia sasa katika fani mbalimbali za kisheria, upepelezi na mambo mengine ambayo yatamfanya kazi yake aifanye vizuri hata suala la kujihami yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, sisi wote tunaishi na wapiganaji na tunawafahamu na wakati mwingine tunaona jinsi wanavyolemewa na shughuli hii kwa sababu kuna mapungufu katika maandalizi yao. Kwa mfano, nieleze tukio la kusikitisha lakini ni vizuri tu nitoe mfano kwa nini kuna umuhimu wa mafunzo zaidi.

Sisi pale Shinyanga alitokea kijana mmoja tu sina hakika kama alivuta bangi au alilewa amechukua jambia amefuata watu wanakunywa kahawa mahali watu wale wametawanyika, amekwenda kwenye mji mwingine wa pili wamekimbia wametoa taarifa Polisi.

Mheshimiwa Spika, polisi watatu wamekuja pale na wana silaha *SMG* na *SAR* lakini kilichotokea ni kwamba baada ya huyu kijana kuwatishia na kuwafuata akiwa na lile jambia askari wale pamoja na bunduki zao walikimbia na walikimbia kiasi kwamba

hawakuonekana. Askari mmoja ambaye hakuwa na silaha alifuatwa na yule kijana na baada ya kuanguka akachomwa kisu kwenye bega lake la kushoto. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yule kijana akawa huru kufanya lolote analofanya na kwa bahati mbaya zaidi yule labda ameshamjeruhi vya kutosha akamwendea raia mwingine akamchoma kisu na ni kiongozi wetu nasikitika kueleza hili kwamba kiongzi wetu wa Chama cha Mapinduzi aliuawa na kijana huyo kwa kuchomwa kisu hicho jambo ambalo kwa kweli lilitusonenesha sana.

Napenda nieleze kwa masikitiko makubwa kwamba hii inatuonyesha kwamba askari wetu wakati mwingine wasipofundishwa kwa kiwango kizuri ambacho kinaweza kuwasaidia hata wao wenyewe kujihami basi matokeo yake ndio hayo ana silaha lakini anamkimbia mtu ambaye amebeba sime ambaye anamtishia.

Mheshimiwa Spika, tukio hili sisi lilitufanya tusielewe kwamba kweli kama kweli Askari hawa wangekuwa wamefundishwa kikamilifu wakaweza kutumia mbinu zao hata kama ni za *karate, akido, kungfu* wangeweza hata wasihitaji *SMG* kumkabili mtu huyo. Baada ya kumuua kiongozi wetu mtu huyu alikwenda kujisalimisha mwenyewe Polisi ajabu alipoingia Kituoni hata Polisi pale Kituoni wakakimbia kwanza mpaka baadaye ndio wakarejea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kueleza haya ili kuonyesha juu ya umuhimu wa mafunzo kwamba ni vizuri Askari wetu wakapata muda wa kutosha wakaimarishwa sio tu katika suala hili la ukakamavu lakini pia katika maeneo mengine ambayo sikuyataja. Nimetoa mfano huo ambao kwetu sisi ulitusonenesha kumpoteza kiongozi wetu labda niseme tu kwamba Mungu amweke mahali pema pema peponi Ndugu yetu Mshandete.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo nataka nizungumzie ni eneo la mawasiliano na mahusiano kati ya Jeshi letu la Polisi na vyombo vingine vya Ulinzi. Nina hakika wote tunajua kwamba Serikali yetu na vyombo vyake vinatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ukisoma Ilani yetu ya CCM juu ya ulinzi na usalama inaeleza kama ifuatavyo naomba ninukuu: "Sera za CCM kuhusu ulinzi na usalama zitaendelea kulenga kwenye mambo yafuatayo hasa katika Jeshi la Polisi, ni kujenga Jeshi la usalama wa raia dogo na lenye utaalam wa kisasa wa kudhibiti machafuko katika jamii, mbinu za kisasa za upelelezi na umahiri katika kuendesha mashtaka, Jeshi ambalo ni rafiki wa raia wema na tishio kwa wahalifu, Jeshi lenye uzalendo na uadilifu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, mimi ambacho ninakiona juu ya mahusiano ambayo yanatajwa katika sera hii ni kwamba hayapo. Ukienda Vijijini utasikitika kuona kwamba kwa mfano, tuna utekelezaji wa suala la ulinzi wa umma. Majeshi haya kama ya Sungusungu au Jeshi la Jadi, viongozi wao uhusiano walio nao kati yao na Polisi ni uhusiano wa kiuhasama, ni uhusiano ambao ni kama wa chui na paka. Hakuna ushirikiano ambao unaweza kuwasaidia kufanya hii kazi yao vizuri zaidi. Jambo hili linafifisha azma nzima ya kuleta mtangamano wa amani na utulivu katika nchi yetu kama ambavyo chombo hiki kinakusudiwa kifanye.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba suala hili la kuhusisha majeshi haya ya jadi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametaja katika hotuba yake yatazamwe vizuri ili nao waweze kushirikiana na Jeshi hili la Polisi vizuri zaidi ili suala la amani na utulivu liweze kuchukua nafasi yake katika nchi yetu tofauti na ilivyo sasa. Kwa mfano, katika maeneo yetu inapotokea bahati mbaya mtu kazidiwa labda na pombe au kifo kilivyo kimemkuta, wanaofuatwa pale ni viongozi wa Sungusungu. Wanakamatwa na kwa kutishiwa na kwa sababu hawajui sheria wanaambiwa sasa ninyi kesi hii ni ya mauaji lazima mhakikishe mnachanga laki nne mlete mapema kabla faili lenu halijakwenda kwenye Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linajenga mahusiano mabaya, mahusiano ambayo hayalengi lengo moja la kudumisha amani na utulivu na pia yanatoa mwanya wa rushwa kwa sababu kama kiongozi katika Jeshi anaomba chochote au anaomba fedha hizo kwa ajili ya kutokumpeleka huyu mtu kutoa maelezo ya namna gani wamemshuhudia huyo mtu amekufa, basi hali hii inasababisha uvunjaji wa amani.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu bali pia lengo zima la kuhakikisha kwamba hawa nao wanatoa mchango wao wa ulinzi na usalama katika nchi yetu linakuwa halipo. Kwa hiyo, suala la mahusiano ni suala ambalo nafikiri linahitaji kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la mwisho, ni suala la nyenzo za kazi za stadi kama ambavyo wenzangu wamekwishasema kwamba ni dhahiri kabisa, tunawaona askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, vifaa duni lakini wanajitahidi kadri inavyowezekana na mimi naungana nao kuwapongeza.

Nawapongeza pia viongozi wa Jeshi la Polisi waliopo katika Wilaya yangu ya Shinyanga Vijijini. Lakini tatizo ambalo nimeliona ni kwamba wakati mwingine katika mgawo huu wa fedha kwa ajili ya mafuta wakati mwingine hautoshi, maana unamkuta askari anafuatwa kwa ajili ya tukio lililojitokeza kilomita mia moja kutoka kwenye kituo chake anakwambia sina mafuta. Sasa inabidi huyu mtu ambaye anahitaji msaada atie mafuta kwenye gari ili gari hilo liende kutoa huduma.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri katika mgawo wa fedha za matumizi ya askari katika Wilaya uzingatie pia ukubwa wa Wilaya yenyewe. Haitopendeza kama askari wanapewa kiasi kidogo ambacho hawawezi kufanya kazi zao kama ilivyokusudiwa. Kwa hiyo, naomba wapate magari mapya na vifaa vingine vizuri na magari hayo yasiwe mapya tu bali pia wapate na mafuta ambayo yanaweza kusaidia katika kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba nitumie nafasi hii kutamka bayana kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa mchana huu na mimi kuwa miongoni mwa watu wa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kwanza tofauti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia ningependa mimi kuelekeza pongezi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli wameonyesha kwamba ni Wabunge. Pia na-*reserve* pongezi zangu kwa wale Wabunge ambao bado hawajaweza kujirekebisha na kuweza kwenda sambamba na shughuli za Kibunge. Baada ya hapo napenda nichukue fursa hii kuipongeza kwa dhati hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni hotuba yake ya kwanza tokea kupewa nafasi hii ya kuwa Waziri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wakuu wakiwemo Kamishna wa Polisi wa Tanzania Bara pamoja na Kamishna wa Polisi wa Zanzibar kwa ushirikiano wao waliotoa katika kufanikisha shughuli nzima ya utendaji wa Jeshi hili la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo mimi nilikuwa na mambo machache ambayo ningependa kuchangia kwa mchana huu wa leo. Kwanza, ni kuipongeza Wizara hii kutokana na juhudi na malalamiko au maombi tuliyoyapitisha katika bajeti iliyopita ya kukarabati ofisi kuu ya Jeshi la Polisi, Zanzibar pamoja na baadhi ya vituo vya Polisi vilivyojengwa kule Pemba.

Naipongeza sana Wizara nikitegemea kwamba katika Bajeti hii yale ambayo tuliyalalamikia katika bajeti iliyopita na hayakupata nafasi basi mara hii yatazingatiwa zaidi hasa tukizingatia pamoja na nyumba za Polisi zilizokuwemo Makao Makuu au eneo la Makao Makuu ya Polisi Ziwani pale Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kwamba hivi karibuni nilisikia katika vyombo vya habari kwamba kuna kesi za madawa ya kulevya zipatazo 400 zimefutwa kutoka Mahakama ya Zanzibar kwa kukosa ushahidi. Vitu hivi vimekamatwa, Polisi wamechukua juhudi ya kuzipeleka kesi hizi, sasa cha kushangaza ni kwamba tunapata taarifa kwamba kesi zile zimefutwa au watu wale wameachiwa huru kwa sababu ya kukosa ushahidi.

Sasa hapa inavyoonyesha ni kwamba askari hawaelewi madawa ya kulevya au kuna utaratibu gani ambao unaofanywa mpaka Polisi ambao ndiyo wadhamini wa kesi hizi zinapokwenda Mahakamani wanaambiwa watu hawa wanaachiwa kwa sababu hakuna ushahidi uliokamilika na badala yake hatuelewi ni nini ambacho kinajitokeza?

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, lakini hatuelewi nini hatima ya hayo madawa au mambo ambayo yanahusika na kesi hizo yaliyochukuliwa kama vielelezo huwa yanaishia wapi? Wanarejeshewa wenyewe watuhumiwa au yanakwenda wapi? Tunasema hivyo kwa sababu tunaona kwamba bado uasi unazidi, watoto wetu, wajukuu zetu bado wanaathirika na madawa ya kulevya. Lakini tunapokwenda Polisi tunaambiwa hakuna ushahidi.

Kwa hiyo, naomba sana suala hili lizingatiwe kikamilifu, la sivyo tutafika mahali pabaya kwa sababu hali ya madawa ya kulevya inaongezeka na matokeo yake wananchi tunalalamika hatujui yanaishia namna gani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia katika hotuba hii ni suala la Ukimwi. Hali ya Ukimwi inazidi kuongezeka. Kama tunavyoelewa haubagui, hauangalii askari, Mbunge, Waziri wala mtu yeyote, atakayezubaa ndiyo yule yule ambaye atakumbana nao. Sasa kama alivyozungumza Mheshimiwa mwenzangu hapa kuna hii sheria ambayo imewekwa kwamba kijana wa Polisi anapoingia kwenye Jeshi asiolewe au asioe mpaka afike umri fulani wa Jeshi. Ningesisitiza na kuweza kuunga mkono wenzangu kwamba kipengele hiki tunahitaji kukitazama kwa sababu kinaweza kwa upande mwingine kutupatia vishawishi vya kuweza kufikia mahali ambapo hatukupategemea na kikatuweka pabaya. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake waiangalie upya sheria hii ili kuweza kuwapunguzia nafuu na afadhali kufuatana na hali ya nchi inavyokwenda hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa pia kulizungumzia ni kwamba kuna agizo au kuna utaratibu wa wananchi kujijengea Vituo vya Polisi kutokana na mahitaji ya kuwa karibu na usalama. Lakini cha kusikitisha ni kwamba wengi ambao wanachukua jukumu la kujenga huzingatia tu kuwa na Kituo cha Polisi lakini hawazingatii kwamba Polisi anapokwenda pale anahitajika kukaa. Kwa hiyo, ningetoa wito kwa wale ambao watachukua jukumu la kujenga Vituo vya Polisi ikiwa ni wananchi wao wenyewe kujenga basi vile vile wazingatie kujenga pamoja na nyumba za Polisi ili wawape fursa wale Polisi watakaokaa pale kuweza kufanya kazi kuliko kuuachia mzigo Serikali kufuatana na hali ya bajeti iliyokuwepo na bajeti hii iweze kufanya mambo mengine ili kuweza kufanikisha utendaji wa shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ili nimpatie nafasi mwenzangu ni kuhusu suala la nyenzo za ndugu zetu wa Polisi. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba ndugu zetu Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hivi karibuni nilipokuwa katika Wilaya yangu kulikuwa na tukio moja ambalo tukio hilo nadhani wengi wamelisikia kulipokuwa na ugomvi wa mipaka kati ya Kijiji na Kijiji na ilipotokea kwamba wananchi wa Kijiji fulani wanataka kwenda kulipiza kisasi Kijiji kingine jambo la kushangaza au kusikitisha ni kuona au kusikia kwamba Polisi wanashindwa kupata usafiri wa kwenda kulishughulikia suala lile na matokeo yake yakajitokeza mambo makubwa ambayo hayakuweza kuzuilika. Jambo ambalo kama wangekuwa wamepewa nyenzo za usafiri natumai wangepata fursa ya kuweza kulizuia suala lile kutokea.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuiomba sana Wizara kuwatafutia usafiri pamoja na mafuta Polisi ili waweze kupata uwezo na fursa ya kuyashughulikia mambo ipasavyo na kuweza kuepukana na lawama ambazo zitakuwa hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo naomba niiunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuitayarisha hotuba hii. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wote waliochaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuipongeza Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa juhudi kubwa ya Jeshi la Polisi linavyojitahidi kupambana na majambazi na kujitolea nafsi zao kwa kulinda amani, usalama, mali na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kupitia kwako nawapa pole kwa vifo vya askari wetu ambao wameuawa wakati wakipambana na majambazi na wahalifu wengine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Mambo ya Ndani itupie macho kitengo cha *Police Marine* cha Zanzibar kwa kuwapatia nyenzo za kisasa za kazi kama vile boti za doria za kisasa na mitambo ya mawasiliano ya uhakika ili ziweze kufanya kazi zake za ulinzi baharini na mwambao mwa visiwa vya Zanzibar maana ulinzi wa pwani ni muhimu sana hasa wakati huu ambapo sekta ya utalii inakua kwa kasi huko Zanzibar na maeneo ya visiwa vidogo vidogo vinavyoizunguka Zanzibar. Kwa sababu kumekuwa na harakati nyingi za utalii kwenye visiwa hivyo, wakipatiwa vifaa hivyo wataweza kulinda usalama na hata ajali za baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Uhamiaji. Naiomba Wizara kuifanyia matengenezo Ofisi ya Uhamiaji iliyopo Bandarini Zanzibar ili iwe na hadhi na sura nzuri kwa wageni wetu wanaokuja kutembelea Zanzibar kama inavyojulikana uhamiaji ni sura na uso wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa kwa Wizara hii jinsi ya maamuzi ya chombo kikuu hiki cha Bunge lenye dhamana ya kupitisha sheria kwamba mnamo tarehe 4 Novemba, 2002 tumepitisha sheria hiyo ya *The Tanzania Passport and Travel Document Bill, 2002.* Sijui nani mwenye mamlaka ya kubadilisha vipengele vya sheria hiyo baada ya Bunge kupitisha, maana tarehe 1 Novemba, 2002 Kamati ya Ulinzi na Usalama ilitoa maoni yake kuhusu kifungu namba 13 kinachozungumzia watu ambao wanaweza kuunganishwa katika hati ya usafirishaji kiongezwe kifungu kitakachomruhusu mke au mume mmoja, yaani kiwepo kifungu kinachofafanua kuwa mume au mke anastahili kuwa na *diplomatic passport,* anaweza kupatiwa vile vile mke au mume mmoja haki ya kuwa na *diplomatic passport.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati wa kuchangia hoja hiyo Mheshimiwa Parseko Kone, alikuwa anatoa maoni yake naomba nimnukuu: “Mheshimiwa Spika, hili ni suala la Wabunge kupata *passport* ya diplomasia pamoja na Mheshimiwa Waziri kueleza lakini hii ikishapita hivi bila kutolewa kwenye maandishi japo itakuwa kwenye *Hansard* itapelekwa kwa Mwandishi wa Sheria ataandika hivyo hivyo. Kwa hiyo, nashauri iletwe *schedule of amendment* nyingine ambayo ipo inayomtaka Mbunge apate *diplomatic passport.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri ya tarehe 4 Novemba, 2002 alisema hivi, naomba ninukuu: “Mheshimiwa Spika, mwisho, Wabunge

wengi walitaka tubainishe waziwazi katika waraka wetu huu kwamba pia Wabunge wote wana hadhi ya kuwa na *Passport* za Kibalozi na napenda kuwaarifu kwamba katika majumuisho haya pia Wabunge wote watapata *Passport* za Kibalozi wao na wake zao au wao na waume zao." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda Ofisi ya Uhamiaji kutaka *diplomatic passport* za wake zao au za waume zao watendaji wa Ofisi za Uhamiaji huwa wanajibu hakuna sheria hiyo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atupe maelezo ya ufasaha kuhusu sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali ya Muungano kufikiria kuwa na Ofisi ndogo ya Wizara ya Mambo ya Ndani Zanzibar kama ile ofisi ndogo ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iliyopo Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia usumbufu wa bure wanaoupata wananchi wa Zanzibar kwenye *road block,* zipo saa 24. Utaona magari yanasimama kungoja gari ya mbele iruhusiwe kwa maana tangu zamani utaratibu huo upo, magari ya abiria lazima yasimame kituoni yaangaliwe na magari ya *private* hayasimami. Hivi sasa kumejazwa mapipa na magongo ili gari isipite kwenda wala kurudi, ziwe zinapita upande mmoja tu.

Kwa hiyo, kunakuwa na msururu mrefu kusubiri magari ya mbele yaruhusiwe. Naomba vizuizi hivyo viwekwe nyakati za usiku na siyo mchana labda kuwe na dharura maalum inayobidi kuwepo na *road block.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na napenda kuunga mkono Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kikao cha asubuhi. Wasemaji wa kwanza wawili wa jioni watakuwa ni Mheshimiwa Mohammed Abdully Ally na Mheshimiwa Ali Machano Mussa. Kwa hiyo, wasichelewe kufika. Baada ya hapo sasa nasitisaha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kidogo katika hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kwanza, sinabudi kwa heshima zote kulishukuru Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri inayofanya. Pili, mimi binafsi namshukuru Mkuu wa Jeshi la Polisi, Ndugu Omari Mahita kwa ushujaa na ukakamavu mkubwa alionao. Kwa maana hiyo nampongeza kwa

ushujaa na maarifa makubwa na elimu kubwa aliyonayo kwa sababu inapotaka kutokea migogoro kati ya wananchi na Jeshi la Polisi yeye anaitatua kwa ustaarabu mzuri tu.

Wananchi wanaposema sisi tutafanya maandamano, wanapoambiwa msifanye yeye anakaa nao anawambia nini tatizo, mnataka kufanya nini, wanasema sisi tunataka kung'oa hiki na hiki, anawaambia hapana. Ruhusa ya maandamano mnapewa lakini msipite hapa, msitukane huyu na msifanye hivi. Sasa ile ni elimu kubwa ambayo sina budi kumshukuru Mkuu wa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba ndugu zangu, swahibu zangu waliosema kwamba wao ni wazungu tunakubali kwamba hawa watu ni wazungu, lakini ni Waarabu weusi, kwa hiyo wao ni Waarabu weusi. Kwa hiyo, ndiyo maana tukawa hatukubali mara nyingi kule Pemba, lakini tumeingia kwa ushujaa wote na miongozo mikubwa ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa kabisa ambalo nataka kulichangia ni kuhusu polisi. Kuna ndugu yangu mmoja Askari Polisi *X2131 PC* Omari Salum Bakari, alifariki dunia mwaka 1991. Naomba mnisikilize vizuri amefariki mwaka 1991 huko Bombo, Tanga, *wallahi* hamwezi kuamini mpaka leo tuna miaka 13 familia yake hawajapewa kiinua mgongo chake. Sasa ni miaka 13 mpaka leo Jeshi la Polisi huyu kijana aliyefariki familia yake hawajalipwa haki yao. Je, kwenye Jeshi la Polisi kuna nini? Hakuna wafanyakazi, hakuna watu wanaoshughulikia suala hili na miaka yote hii 13 mtafanyaje, mtawalipa familia yake *interest* maana kila siku mambo yanabadilika. Ikiwa haiwezekani kuwalipa familia yake *interest,* naomba kwa heshima na taadhima zote familia yake ipewe fedha maalum za kuweza kuwasaidia watoto wake kwa kustahamili miaka hiyo 13 bila kupewa malipo yoyote. Kama hamtafanyi hivyo mtakuwa mmewadhulumu watoto wa marehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna askari mwingine alifariki katika Mkoa wa Morogoro mwaka 1994 anayefuatilia mafao ya marehemu huyo ni Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, mpaka leo malipo yake hajapatikana, ndani ya Jeshi la Polisi kuna nini. Kazi nzuri ya kutulinda sisi mnafanya lazima tunawapongezeni. Lakini haki zenu wenyewe ndani ya Jeshi la Polisi zinapotokea zinakuwa hazipatikani nini tatizo.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri unisaidie tunavyotoka hapa baada ya kikao cha Bunge kumalizika tufuatane ukanipa cheque ya mtu huyo aliyefariki mwaka 1991. Kama hakuna fedha zitafutwe fedha maalum nipewe niwapelekee watoto wa marehemu kwa sababu mke wa marehemu na watoto wake wanakaa pale nyumbani kwangu na mimi inabidi niwape chochote kwa sababu hawajui ya huko. Fedha zangu nilizowapa mimi nazisamehe. Lakini zile ambazo ni haki yao mnipe niende nayo *cheque,* ni aibu miaka yote hiyo kuna nini ndani ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia nadhani ndiyo matatizo. Nadhani Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu hawajapita katika sehemu inayoshughulikia mafaili ya pensheni ndani ya Jeshi la Polisi kule Makao

Makuu.  Huwezi kuingia mle ndani  na kama utatokea moto itakuwa hatari sana, mafaili yamejazana mle, wale wafanyakazi wanaofanya kazi mle  utawakuta  hawana masharti kwa sababu ndani ya chumba hicho kuna joto  na kuna vumbi hakuna feni na hakuna kiyoyozi.  Jeshi  Polisi kwa nini  sehemu ile mnaidharau sana.

Mheshimiwa Waziri  katika ziara zenu mwende mkaangalie na Kamati ya Ulinzi na Usalama nafikiri iende ikatazame sehemu hiyo ni hatari sana, wanaofanya kazi mle ni Maafisa wanawake na Maafisa wanaume wote unawakuta hawana nguo.  Huwezi kuvaa nguo kwa sababu joto kali  linalokuwemo ndani na mafaili yaliyomo ndani.   Sisemi uongo mwende mkaangalie.   Naamini kwamba Wakuu wote wanaohusika hawajapita katika sehemu hiyo, wangepita wangekuwa wameshaijenga, maana Jeshi la Polisi ni hodari sana wa kujenga nyumba.  Sehemu hiyo lazima ijengwe vizuri na iwekewe viyoyozi na iwekewe mafeni na wafanyakazi wale kila asubuhi wakifika wapewe maziwa na yai moja au mtawaua mapema.   Kwa sababu mazingira wanayofanyia kazi ni magumu sana.  *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, halafu jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge hasa  mimi katika Jimbo langu ni la Ziwani, mapolisi wengi tu wamenipiga kura, kwa hiyo najua shida zao ni nyingi na wanapokuwa na shida zao wanakuja kwangu.  Lakini nakutana nao chini ya Mzabarau na  jambo mbaya kabisa ambalo limetudhalilisha sisi Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar  ni kwamba hatukupewa fedha kwa ajili ya ofisi sisi Wabunge wa Zanzibar kwa sababu gani.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kama yupo atueleze tumenuna.  Kwa nini sisi Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar hatukupewa fedha kwa ajili ya ofisi, sasa sisi mapolisi tutakutana nao wapi.  Mwenzangu hapa juzi mama Elizabeth Batenga anasema ooh mimi nimepewa ofisi, lakini sasa nataka karani eeh mama Elizabeth Batenga ana ofisi mimi sina ofisi.   Ni mambo makubwa sana na wala hakuna mahali popote inapozungumzwa.  Kwa nini sisi hatukupewa ofisi na wakati sisi tunakutana  na polisi na wapigakura wanakuja kwa nini  sisi hatupewe  ofisi?  Limetuudhi sana  hilo  na siyo kero ya Muungano, ila ni kero la Waheshimiwa Wabunge, tukiondoka hapa mtupe na sisi *cheque* zetu tukatengeneze ofisi, tumenuna hatuna ofisi.  Huo ujumbe umefika.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu namna ya kuajiri polisi. Wanavyoajiri wale polisi ni utaratibu mzuri tu mimi naukubali na nauafiki. Lakini ninaloliomba ni kwamba wanapoajiriwa polisi wote wanaajiriwe kwa namna moja wawe *pensioner* wasiwe na taratibu mbili, sijui mpaka watimize miaka mitatu wanaambiwa, kwa sababu  wanapotaka haki za Jeshi la Polisi wanaambia aah polisi ni raia wanakwenda  kwa taratibu za kiraia.  Lakini sasa inapobidi sasa kupata *benefit* wanatolewa wanakuwa hawamo katika mambo ya kijeshi, wanaambiwa wao ni raia, kwa  hiyo mambo yao yanakwenda kiraia si vizuri.  Nashauri Polisi wote wawe waajiriwa.  Hizo sheria za ukoloni  zilizokuwepo tuziondoe.  Sasa ni miaka 40 bado tunafuata sheria za wakoloni jamani!

Tunaondoe hizo sheria za kikoloni waajiriwe kwa *format* ya  *pensioner*  wote kwa sababu wanapata dhiki wanapostaafu wanapata shilingi 8,000/= au 10,000/= na wakati

wengine wakistaafu wanapata mamilioni kwa mamilioni na wakati wote wamekwenda kwenye uajiriwa wa namna moja.

Mheshimiwa Waziri naomba hilo uliangalie mlete hizo sheria hapa zifanyiwe marekebisho. Haifai kufuata taratibu za kikoloni na siyo nzuri. Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu maswali hapa kwa kufuata sheria za kikoloni si vizuri. Leteni hapa sheria za zamani zifanyiwe marekebisho ili askari polisi wote waende katika mfumo wa *pensioner.*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizunguma sasa hivi ni kwamba hali ya ndugu zetu wa polisi tunazijua, mishahara wanayopata ni midogo, lakini taratibu kidogo kidogo zinaenda. Lakini polisi lazima wapewe kitu maalum, zamani ilikuwa polisi akifanya kazi nzuri anapewa kitu chohote sasa hivi hakuna.

Kwa mfano, sasa ile ilivyotokea Polisi wetu Mungu awarehemu wameuliwa pamoja na mbwa wao. Lakini siku ya pili na ya tatu, polisi wamefanya kazi nzuri wote wale waliohusika wametiwa mikononi mwa polisi, sasa wale polisi waliofanya kazi hiyo wangepewa zawadi. Hilo tunalisema sisi wapeni zawadi waliofanya kazi hiyo, kwa sababu ukiwapa zawadi wale na mwingine atafanya kazi zaidi kuliko ile. Lakini mnataka mpaka tusema sisi basi tumekwishasema Mheshimiwa Omar Mahita, wapeni zawadi wale polisi waliofanya kazi nzuri, na sasa hivi tunalala vizuri na tunafurahi ingawa matatizo madogo madogo bado yapo, lakini yote yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu Chuo cha Mafunzo cha Polisi kiko Moshi tu, kwa nini kiwe Moshi tu na Zanzibar Chuo kipo kizuri tu na huo uwanja wa shaba uko kule Zanzibar kwa nini polisi hao lazima waende Moshi katika kozi ya mwanzo, watawanywe kanda fulani ziende kule Zanzibar na kanda fulani iende huko Moshi. Sasa Chuo kile kimekaa tu mpaka Maofisa waamue kufanya semina ndiyo wanakuja kufanyia kule, kile chuo hakina kazi yoyote. Nakumbusha kama kile chuo cha Zanzibar kilisahauliwa kipo, kozi ya mwanzo waingie pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nitalisema mpaka nitamaliza Ubunge wangu na nimeishalisema miaka mingi na nalisema tena kwamba Polisi anapoingia katika Jeshi la Polisi na akafanya kazi zaidi ya miaka 10 au 6 kama hajafanya makosa, hajashitakiwa kwa nini asipewe Ukoplo lazima aende kozi, sasa kozi ni nini, miaka 10 tu hajafahamu tu uongozi mdogo mdogo, apandishwe cheo cha Ukoplo si lazima kwenda kupata mafunzo, mafunzo kule yanataka fedha, mafunzo kule yanataka *estimate* ifanywe. Lakini ukimpandisha tu Ukoplo ilimradi umeshamwona nidhamu yake hujamwita kumuonya na hujampata barua ya onyo lolote. Mtu anapochukua rushwa usimlaumu lazima achukue rushwa akishakaa kazini kwa muda wa miaka 10 na kazi yake ni nzuri au miaka 15 hata Ukoplo hajaupata kwa nini asichukue rushwa. Unamlaumu vipi kwa nini asichukue rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri tena cheo cha Koplo wasipewe kwa kufuata waliopata mafunzo zitazamwe nidhamu zao, utazamwe utendaji wao wa kazi na muda

waliokaa kazini wapewe tu. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Mkuu wa Jeshi la Polisi mliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba polisi kule Zanzibar wanakaa katika nyumba nzuri sana zina maji, zina umeme na zina ngazi ya kupandia kwenda kwenye verenda kupumzika. Kwa hiyo, polisi wanajisahau kujenga nyumba zao za kuishi. Tunaomba wapatiwe mikopo nafuu ili walazimishwe mapolisi wajenge nyumba, kwa sababu huko mbele mtu anastaafu kazi anakaa ndani ya nyumba ile ile hana mahali pa kwenda sasa aende wapi hakujenga nyumba yake ya kuishi, kazoea umeme, kazoea maji, kazoe kule juu nyumba yenye upepo mzuri inakuwa dhiki kwa hilo.

Kwa hiyo, tafadhali wakopeshe wale polisi wajenge nyumba, mimi napigania vitu vya ujenzi sisemi mambo ya kuwakopesha magari na pikipiki wakopeshe vifaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vifaa vya kufanyia kazi wapewe. Vifaa vya kufanyia kazi kule kwetu ni duni na vya kizamani sana hata trafiki anakaa usiku humwoni kama pale kuna trafiki. Lakini Dar es Salaam matrafiki wana makoti yanang'ara kabisa unamwona huyo trafiki, lakini trafiki wa Zanzibar hawana. Utawaona wamevaa siku moja kwa sababu Mheshimiwa Rais anakwenda mahali ili isitokee ajali ndiyo trafiki anapewa mmoja basi, sasa kila trafiki apewe. Halafu na *radio calls* kule hakuna ziko mbili, tatu basi, kila trafiki anatakiwa awe na *radio call* yake ili kuzungumza na mwenzake aliyeko sehemu nyingine. Kwa sababu ajali za Unguja ni nyingi sana kuliko ajali za Tanzania Bara ukifanya utafiti. Wale madreva wa daladala ni vijana kuanzia umri wa miaka 20 mpaka 25 wanaua tu, utawakuta katika njia zetu ambazo ni nyembamba zile kama kitanda cha futi tatu, basi wanakwenda wawili hivi, utashangaa eeh, njia hii nyembamba kama kitanda cha futi tano hakifiki, njia ya kizamani ni kama futi nne wao wanakwenda kwa *speed* kubwa wakiwa wawili. Kwa sababu wanajua hata akiua anakwenda kule analipishwa faini shilingi 2,000/= wanatoka.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni la Muungano, nilipouliza mimi kule nikaambiwa haya yanangoja Baraza la Wawakilishi yapitishwe. Hili jambo kwa nini lipitishwe na Baraza la Wawakilishi wakati hiki chombo ni cha Muungano lazima Polisi mambo yao yapitishwe na Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi ya Muungano, tunauawa sana kule kwa hao madreva vijana ambao hawana nidhamu wanaua watu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho kabisa ninaloliomba kwa heshima na taadhima kunapotokea ajira za Polisi hali kule inafanyika vizuri hakuna matatizo. Namshukuru sana Mheshimiwa Khalid, ukimwendea nisaidie anakwambia hapana, mimi siwezi kukusaidia fuata taratibu, kijana afanye mtihani na afaulu na afikie kiwango kinachotakiwa ndiyo aende polisi. Hilo namshukuru sana hivyo ndivyo inavyotakiwa. Lakini tutazamane siyo watu wote tuajiriwe ndani ya Jeshi la Polisi. Zanzibar ni nchi nyingine, ina namna nyingine na ina siasa nyingine, lazima tumchunguze mtu ndiyo umpe kazi na lazima awe wa CCM ndiyo umpe kazi bwana. Usimpe kazi mtu mwingine lazima hiyo. Kwa sababu tukija kuwapa hawa watakuja

kutafanya mambo hawa eeh, usisikilize kama hawa ni watoto wetu ni hatari sana watu hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE ABDUL MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelezwa siku zote kwamba hatutakiwi kuturejee maneno yale yale. Lakini kutokana na tatizo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, mambo yake yanaonekana yanafanana na Waheshimiwa Wabunge wengi wanapata malalamiko kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo, ningekuomba kidogo utuvumilie kurejea baadhi ya mambo kwa sababu yamekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wetu.

**SPIKA:** Ruksa.

**MHE ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa hiyo, nashukuru baada ya kupata ruksa hiyo. Kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya ambao wamechaguliwa kuungana nasi sasa katika kuzungusha gurudumu hili na nawatakia mafanikio mema wawepo kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wake wote nikisema zaidi na Kamishna wa Polisi Zanzibar kutokana na mitikisiko ambayo inatokea Zanzibar na kuweza kuikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja Wizara nzima kutokana na mabadiliko ambayo yametokea ambayo niliyaomba mwaka jana yafanyiwe kazi na naona yamefanyiwa kazi. Yale yanayohusiana na namna ya kupata *Visa* kutoka Italy kwa watalii kuja Zanzibar kitu ambacho kilikuwa tayari kinatuvurugia mapato yetu Zanzibar. Lakini kwa bahati kimerekebishwa kwa hiyo kwanza sina budi kuipongeza Wizara kwa kazi ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nizungumzie suala la linalohusu kubadilishwa kwa sheria zilizopitwa na wakati. Hili ni suala ambalo miaka yote tukisimama hapa Bungeni tunalizungumzia na kwa bahati hata juzi katika kipindi hiki cha Bunge nimejaribu kuuliza swali na nikajibiwa kwamba hiyo hali imeisharekebishwa. Lakini wapiga kura wetu ambao ndiyo waajiri wetu au waajiri wetu bado hawajaridhika na hiyo hali. Kwa nini nikasema kwamba hawajaridhika ni kwamba suala la wafanyakazi wa Polisi ambao wanamaliza miaka 21 kama hawakujiandikisha katika pensheni matokeo yake wanapata malipo madogo ukiwalinganisha na wale wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri ningependelea ulitilie maanani na uone kwamba kuna haja ya kulitazama upya kwa kina kabisa. Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu mpaka sasa kuna watu ambao walibahatika kupigana vita na wamo katika Jeshi la Polisi wanategemea kustaafu katika miaka ya hivi karibuni, na kwa bahati mbaya hawakuingia katika mfumo wa pensheni kwa hiyo wamekuwa na kilio kikubwa. Ni kwamba watatoka wengine ni ma-*Sergeant Major* na wengine ma-*Sergeant* lakini bado watakuwa na malipo kidogo, na ukiangalia kazi walioifanya ni kubwa sana.

Sasa hili ningeomba Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wako kwa nafasi ulioichukua sasa liangalie hilo kwa kina waonee huruma watu hawa. Kitu ambacho Waheshimiwa Wabunge wenyewe tukifanya kazi kwa muda wa miaka mitano tunaona uchungu ule na tunaomba kwamba tupate malipo ambayo yatatuwezesha kuishi na hawa polisi ambao wamefanyakazi kwa muda wa miaka 30 wanatoka pale wanaambiwa kwamba malipo yao nayasitili kwa sababu hii ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lakini kuna haja ya kuyaangalia vizuri. Nafikiri suala hilo limeeleweka na nafikiri message hiyo imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kuzungumzia suala la vifo vilivyotokea katika Mahabusu moja kule Lujewa kwenye Jimbo la Mbarali. Kule kuna jambo ambalo lilinisikitisha kidogo ni kwamba kuna Maaskari wamefukuzwa kazi na kwa utaratibu wa Jeshi la Polisi nafikiri *PGO* inaeleza hivyo wafukuzwe sawa. Lakini kitu kinachonisikitisha ni kwamba kuna Polisi anaitwa *PC* yaani Polisi ambaye hana cheo, alikuwemo katika mkumbo ule kwamba alikuwa zamu pale. Lakini wakati yuko zamu lilipotokea tatizo lile ni kwamba na yeye amejumuishwa kwamba ni mtu wa kuachishwa kazi. Lakini ukijiuliza kama mahabusu ilikuwa ndogo na askari yule ambaye alikuwa zamu je, alitakiwa mahabusu wale awachukue awapeleka kwake au awapeleke wapi.

Kwa kawaida askari unapokuwa uko *charge room,* matokeo yote yanayotokea pale wakubwa wako ndiyo ambao wanaweza kuyakabili kuyatolea ufumbuzi wa mwisho. Lakini jambo la ajabu Polisi wa cheo cha chini ni kwamba yeye mahabusu imejaa na imekuwa na mahabusu wengi kabisa yalipotokea matatizo yale na yeye anajumuishwa katika kuachishwa kazi na haki zake zimepotea na alikuwa hana uwezo wa kuwachukua mahabusu wale kwamba awapeleke mahali pengine kwenda kuwahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoomba kama kweli kwa sababu mimi niko Zanzibar na hili suala limetokea mbali, kwa kweli sijawasiliana vizuri. Ninachoomba Polisi yule atazamwe kwa nini aachishwe kazi, na kama imechukuliwa kwamba aachishwe kazi basi na Maafisa wa Kituo kile wote waachishwe kazi. Lakini mimi nisingelipendelea kwamba Askari Polisi yule akaachishwa kazi, kwa sababu yeye anafanya kazi chini ya amri ya wakubwa wake. Nafikiri *message* hiyo imefika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo kidogo linanipa matatizo na kwa kweli sikufurahi nalo. Lakini kabla sijasahau pamoja na kuwapongeza naunga mkono

hoja hii na ipite hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kitu ambacho kimenifikisha mbali kidogo naomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Kamishna wa Polisi wa Zanzibar uniulizie suala hili na ikiwezekana unipe majibu kwa maandishi ili nilielewe vizuri. Kuna hatua ya raia wetu kuchukua sheria mikononi mwao. Mnajua kwa nini raia wanachukua sheria mikononi mwao? Hii inasababishwa na Vyombo vyetu vya dola kudharau baadhi ya masuala mengine ambayo yanatokea. Hawa raia ambao wapo katika mitaa yetu, katika miji yetu na katika Majimbo yetu wengi wao wapo ambao wanajua sheria naweza kusema pengine kutuzidi sisi Waheshimiwa Wabunge au kama tunavyojua sisi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna masuala ambayo sasa hivi yamekuwa yanakera kabisa. Kwa mfano, iko siku moja mimi mwenyewe binafsi nilikuwa natoka na gari yangu nyumbani, nasafiri na boti ya asubuhi saa 12.30 nimesimamishwa Kituo cha Polisi kidogo Shaurimoyo, nitoe msaada kwa askari polisi ana washitakiwa wawili na mbuzi wawili. Askari Polisi mmoja ana mbuzi wawili na washitakiwa wawili, nimesimama kwa bahati ni kwamba wale askari mimi wananijua, nimesimama nikauliza tatizo lenu ni nini, wakasema tusaidie hawa washitakiwa waende Kituo cha Polisi Ng’ambo, nikawambia jamani mimi nasafiri na muda uliobakia ni dakika 20, kutoka hapo mpaka bandari ni masafa kidogo. Lakini hata hivyo, kwa sababu najua tatizo lenu twendeni.

Mheshimiwa Spika nikawachukua mbuzi wawili na askari polisi mmoja. Jambo linalosikitisha nimefika kituo cha Polisi Ng’ambo askari wawili walioko pale ambao wanatakiwa kukabidhiwa wale washitakiwa wawili, nawaambia njooni msaidie mwenzenu huyu hawa washitakiwa wanaweza wakakimbia, askari polisi aliyekuwepo pale ananiambia namalizia kufagia kwanza.

Mheshimiwa Spika, hao askari polisi nawaelewa vizuri sana majina yao, lakini nawasitili kwa sababu hii ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lakini ninachoomba ni kwamba kama tunaendelea na mfumo ule, mimi nilitaka kuwakamata wale raia ambao walikuwa wezi wa mbuzi, lakini nilichukulia kwamba nikiwa nimeloa damu na nikifika bandari watu watanishangaa, mbona Mheshimiwa Mbunge ana damu anatokea wapi. Kwa hiyo kwa kweli nilishindwa.

Kitu kilichobakia nilimtuma dreva wangu atoke na amkamate mshitakiwa mmoja tukamuingiza kwenye Kituo cha Polisi wakashughulika wenyewe na sisi tukaondoka tukaenda Bandarini. Sasa hii linasababisha kwamba kama wangelikimbia wale washitakiwa, raia wema wa mara ya pili watachukua sheria mikononi mwao. Nafikiri *message* hii imefika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika suala hili ambalo raia wanachukua sheria mikononi mwao. Kuna siku moja ambayo ilikuwa tarehe 22 Desemba, 2002 wakati wa saa 12.00 za jioni kuna kijana mmoja ambaye alikuwa na gari ZNZ 23532 *route number* ya Kiwegwa namba 17, kwa makusudi tu angesababisha ajali ambayo ilikuwa hatari

kubwa ambayo ingeliwezekana raia wanaotoka katika ujenzi wa Taifa Tumbatu waingie kwenye daraja wote kabisa. Wenye gari hilo ali-*over take* hiyo gari iliyokuwa iko mbele yake alipofika katikati ya daraja akasimamisha gari lake kwa ghafla. Ile gari ya nyuma ambayo ilikuwa na wananchi wanatoka Tumbatu kwa ajili ya ujenzi wa Taifa siku ya Jumapili aliendesha gari lake akapita Kituo cha Polisi Mfenesini hakusimama. Raia wale walifanya mbinu ya kutafuta simu, kwa bahati nzuri kulikuwa na baadhi ya wengine walikuwa askari wakapata simu Kituo cha Polisi Bububu akasimamishwa dereva yule amezuiliwa pale.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa habari jambo linalosikitisha kesi ile imemalizwa askari aliniletee salaam ya kwamba tutakukomoeni Tumbatu na mtatuona. Matokeo yake kesi ile imemalizwa hata raia mmoja hakuitwa kutoa ushahidi. Lakini je, kama ingelikuwa watu 30 ambao walikuwemo ndani ya hilo gari wamekufa Serikali ingelihuzunika kiasi gani. Ukiachana na hapo majibu yao wanasema kwamba ikitokea ajali, gari imegongwa kwa nyuma basi gari iliyogonga kwa nyuma ndiyo yenye makosa nakubaliana na hilo. Lakini je, wakiamua wenye malori wote watugonge wenye magari madogo kwa nyuma hali itakuwa ikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri kwa hili aliangalie na namtaka hasa afike Kituo cha Polisi Mahonda aliulizie suala hili limekwenda kwendaje? Kwa sababu mwenye gari amelitengeneza gari lake kwa kutumia gharama ya shilingi 500,000/= hili si tatizo. Lakini tatizo ni kwamba raia wanajiuliza hivi Serikali imechukua hatua gani hata kutuita kutoa ushahidi sisi. Mimi nafikiri kuzungumza sana si suala la msingi, tuzungumze na mengine tuyaweka yawe kwa ajili ya kesho.

Mheshimiwa Spika, nafikiri niendelee katika suala la hali ya vitendea kazi vya askari polisi. Pamoja na kwamba nimesema mabaya ambayo walikuwa wameyafanya. Lakini pia mwaka 2002 nilijaribu kuomba suala la kwamba wapatiwe vitendea kazi na baadhi ya sehemu inaonekana vitendea kazi vimepatikana. Lakini kuna hizi simu ambazo wanazitumia *Radio Call.* Niliomba kwamba Kituo cha Polisi Mkokotoni ambapo kina hadhi ya kwamba ni Kituo cha Polisi Mkoa pana ofisi ya *RPC,* lakini hawana *Radio Call* hata ukilinganisha pamoja na Kituo cha Mwera au Vituo vingine *Radio Call* wanazozitumia ni za kwenye magari. Kwa hiyo, naomba hili suala kidogo litiliwe maanani na lionekane kwamba hii hali inarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu kuongezwa kwa mishahara askari polisi. Ukweli ulivyo kutangaza mishahara si kitu rahisi kwa sababu hali ya uchumi wetu tunaitambua. Lakini mwaka huu Jeshi la Polisi kidogo limepewa kitu kidogo, sasa kama limepewa kitu kidogo namwomba Mheshimiwa Waziri watakapopewa kitu hiki basi wawaone askari polisi wadogo na siyo kuwaona Maofisa. Kwa nini nikasema wawaone askari polisi wadogo kimshahara, kwa sababu Maofisa wa Polisi wengi wao wanatumia magari, wanatumia simu na wanatumia vitu vingine kiasi ambacho maisha yao kidogo yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini hawa askari polisi wa ngazi za chini mshahara wao unapokuwa mdogo wanashindwa kupata mahitaji yao ya lazima katika masuala yao ya

kawaida kiasi ambacho inahuzunisha hivi sasa kuna baadhi ya askari polisi wanapotoka kazini asubuhi, askari polisi yule unamkuta na kofia yake na tenga anakwenda tena baharini kwenda kuvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache sina budi kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake nzuri sana aliyoiandaa Kisayansi kabisa. Pia nampongeza pamoja na wataalamu wake wote walioshiriki kuiandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana na shukrani zangu ziende kwa Serikali pamoja na Waziri aliyekuwepo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba uliofanywa mara iliyopita na aliyeko hivi sasa pamoja na Naibu Waziri wao, *IGP,* Kamishna wa Polisi Zanzibar, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba kwa jinsi walivyoshiriki na kusimamia ujenzi wa nyumba zile hadi kufikia hatua iliyofikia hii leo.

Mheshimiwa Spika, ingawa bado umeme tu kukamilika, lakini utaratibu mzima na ni imani yangu kuwa wakati wowote umeme utafikishwa na nyumba zile kufunguliwa rasmi kwa ajili ya makazi ya askari wetu wapendwa pamoja na familia zao. Ingawa nyumba zimejengwa nje kidogo ya Jimbo langu lakini sina wivu, wakati wa ufunguzi Mheshimiwa Waziri naomba unialike rasmi ili na mimi nijisikie raha ya matunda ya utetezi wangu wa askari wa Polisi ambao karibu wote walikuwa wanaishi katika jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo, katika ukurasa wa 13 kuhusu Jeshi la Polisi. Katika ukurasa huu una uchambuzi wa uwiano tulionao hivi sasa ambao askari mmoja ni kwa wananchi 1,500 na kigezo cha Kimataifa ni askari mmoja kwa wananchi 400 mpaka 700. Sasa suala hili kwa kweli ndilo linalosababisha askari wetu kuzidiwa wakati mwingine. askari mmoja kwa watu 1,500 sio kidogo. Sasa je, Serikali mpaka wakati huu tuliofikia ina mkakati gani juu ya urekebishaji wa suala hili.

Mimi nina pendekezo la utu uzima. Naiomba Serikali kupitia Wizara ihakikishe suala hili inalishughulikia ipasavyo juu ya kuwa hali sio nzuri sana lakini kuna mambo nyeti kama haya wahakikishe kuwa wanaipa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 14 kuna masuala ya vitendea kazi. Mimi nitazungumzia kuhusu eneo la kule Pemba. Kwa kweli vifaa vya mawasiliano kwa Jeshi hili ni muhimu sana, lakini kwa upande wa Pemba vifaa hivi vya mawasiliano ni vichache mno. Kuna wakati napata ziara kule za Rais au viongozi mbalimbali lakini wakati tunapita sisi Wabunge au viongozi wengine waliotangulia unawakuta *Traffic* barabarani wanakusimamisha wanauliza je, vipi yuko wapi hivi sasa, ameshakaribia karibia, sasa yale ni matatizo. Kwa hiyo, ipo haja suala hili Serikali ikalizingatia na ikachukua hatua za haraka ili kutatua matatizo haya. Je, leo askari amepatwa na tatizo anataka kuwasiliana atawasiliana vipi?

Mheshimiwa Spika, kuna kupanda kwa gharama ya maisha. Maisha haya ni magumu kwetu sote kuanzia wananchi, wakulima, wafanyabiashara na wafanyakazi. Wakati huo huo kazi za Polisi tunazijua sote ni ngumu sana. Suala langu je, hawa askari wanapewa motisha gani. Mishahara yao ni midogo sana tunajua kulinganisha na kazi zao wanazozifanya. Kila mwaka na kila mara tunawatetea mishahara yao iongezwe lakini hamfanyi hivyo tatizo ni nini Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Hivi karibuni tulipata taarifa kwenye vigazeti lakini si za uhakika kuwa mishahara ya Polisi itaongezwa lakini hamna kitu. Suala langu naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie je, katika Bajeti ya mwaka huu hawa Polisi mmewaangalia kwa jicho la huruma na mmezingatia utetezi wetu Wabunge wa kila mara tunaowatetea hawa Polisi. Kama hamkuzingatia kwa nini hamkuzingatia na kila wakati sisi tunawatetea hapa.

Mheshimiwa Spika, habari ya *training.* Nauliza kuna utaratibu gani wa askari Polisi kwenda kozi mbalimbali kwa mfano Ukoplo, U-*sergeant* na mengineyo. Kwa sababu wengi huchukua muda mrefu sana bila ya kupelekwa kozi angalau ya U-koplo au U-*sergeant* na kadhalika. Hiyo huwa inasababishwa na nini. Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

Nikikupeni mfano mdogo nilipokuwa mdogo mimi darasa la kwanza kwetu kule Pemba Chake Chake walikuwepo askari wawili mmoja alikuwa anaitwa Khamis Mbarak, marehemu na mwingine Mbeta, marehemu vile vile. Hawa toka walivyokuwa wadogo walikuwa *Private* mpaka tukafika *Form Four* bado Ma-*private* hivyo hivyo *private* mpaka karibu ya kufa wakaja wakapandishwa na Mzee Karume mwaka 1972.

Sasa na hawa mnataka kuwageuza hivyo hivyo ebu nipe sababu ya msingi ni mpaka miaka mingapi hawa ndio wanaweza *at least* kupatiwa angalau ukoplo wakaendelea na vyeo vingine. Ikiwa ni haki yao basi wapewe naona fedha nyingi mara hii zimetengwa kwa ajili ya mambo hayo.

Mheshmiwa Spika, kuna ukarabati wa Ofisi wa nyumba za askari. Kwanza, nimeshukuru kwa nyumba zilizojengwa 53 na nina imani zitaendelea kujengwa mpaka zifikie 100 kama lengo lilivyowekwa. Lakini kuna suala la ukarabati wa nyumba za askari pale Madungu na Ofisi ya Makao Makuu ya Mkoa. Mwaka 2002 nilizungumza suala hilo na nashukuru nilipewa jawabu kuwa kwanza subiri ustahimili kidogo tuendelee na haya ya nyumba. Sasa nyumba zile ni nzuri za ghorofa zinaanza kupasukasuka na ndiyo zinatutoka. Pia na Ofisi ya Makao Makuu ya Mkoa ya Polisi hali yake pia ni chafu.

Hii Mheshimiwa Waziri unaniambia nini mara hii juu ya ukarabati wa Ofisi ile na nyumba zile zikae ziendelee kufa au mna utaratibu wowote au vipi kwani nilipiga kelele nyingi sana mwaka 2002. Lakini katika kuchambua katika vitabu vyako hivi katika *Vote 28 Project Sub vote 5724* kuna nyumba za Polisi Pemba. Mle mna mambo matatu 31021, 310600, 310800 *Rehabiliation, Renovation and Replacement of Equipmenst* kuna shilingi milioni 60. Je, katika hizi fedha ukarabati wa Ofisi ya Makao Makuu ya Mkoa

Kusini Pemba na nyumba za askari zile za Chake Chake zimo au hamna, naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi ufuatao mfanyakazi yaani askari polisi anapofariki kabla ya tarehe ya mwisho wa mwezi akiwa kazini yaani kwa mfano tarehe 10 au 11 ya mwezi je hulipwa mshahara wa mwezi mzima au zile siku alizofanya kazi hulipwa zile tarehe 10 au 11 au akifariki tarehe hizo na fedha alizochuma kwa siku hizo nazo hufariki. Kwa sababu haya yametokea ikiwa ana haki ya kulipwa yule mtu basi mimi nitakuja kukuona Mheshimiwa Waziri kukuelezea ni mtu gani na ni vipi. La ikiwa vingine hakuna haki kama hiyo basi itakuwa umeshafafanua itakuwa basi.

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea *Immigration.* Pongezi kwanza kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara na Serikali kwa kununua mtambo mpya wa kisasa wa kuchapisha hati za kusafiria katika Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar ambao umeshaanza kutoa *passport* za Afrika ya Mashariki. Lakini hiyo natoa pongezi.

Pili, kuna kazi za *Immigration* ni nyingi sana na zaidi kazi za *Immigration* ni za ufuatiliaji. Kwenye Mahoteli ya Kitalii ambayo yako katika maeneo mbalimbali haya yanahitaji mafuta. Nilikuja nikapitia kile kitabu nikaangalia katika *Vote 51 Immigration Zanzibar Sub Vote 2001* ukurasa 180 Kifungu 270500 *fuel and oil.* Hawa *Immigration* Zanzibar wamepewa 37, 970, 974. Sasa ukiichambua hii kwa mwaka Makao Makuu pamoja na mikoa mitano jumla ya kila mmoja atapata 1,800,000 na kidogo. Kwa mwezi 515,000 kila mkoa kwa siku kila mkoa utapata 17,174/29. Mkoa ukigawa mara tatu kwa sababu kuna Wilaya mbili mbili kule kwetu ukiigawa hiyo kwa tatu shilingi 5,724 kila Wilaya shilingi 5,000 pamoja na Mkoa je fedha hizi kweli zitakidhi huyu *Immigration Officer* kufanya kazi yake Makao Makuu. Mkoa mzima una 5,000 hata *ten litres of diesel* haifiki.

Kwa hiyo, naomba suala hili lizingatiwe ikiwa kuna *Supplementary Budget* waifanye lakini hawa wahakikishe kazi zao zinakwenda vizuri kila siku wanalalamika hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwa upande wa Polisi katika *Sub Vote* hii hii nao niliangalia *Sub Vote* yao 2005 Polisi Zanzibar ukurasa 33. Kifungu kidogo 2705 *fuel and oil* hawa bahati nzuri walipewa shilingi 211,400,000. Nashukuru mara hii nilimwambia Kamishna kule katika kuchangia nikamwambia Kamishna vipi huwashirikishi wenzako bwana. Mara hii amejitahidi Kamishna nampongeza.

Naipongeza Wizara na Serikali kwa jinsi ilivyojitahidi mara hii kwa upande wa polisi angalau kwa mwezi Makao Makuu pamoja na mikoa inapata angalau shilingi 2,900,000/=. Sasa sitaki nichanganue mpaka nifike chini kabisa kwa sababu mambo si machafu sana, kwa hivyo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naiunga mkono hoja hii mia kwa mia na niseme ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani kwa mwaka wa 2003/2004. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii nzuri. Pamoja na pongezi hizo ninayo machache ya kushauri Serikali. Kwanza nianzie katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba wote tunaelewa kwamba hivi sasa kumejitokeza ongezeko la wimbi la uhalifu nchini na imeonyesha hata katika takwimu tulizopewa na katika hotuba ya Waziri hapa katika idadi ya mikoa tuliyonayo Dar es Salaam ndiyo inayoongoza ikiwemo na mikoa mingine ya Mpakani kama Arusha, Mbeya na maeneo mengine.

Mimi napenda naishauri Serikali nimwombe Mheshimiwa Waziri naomba kwa sababu Jeshi la Polisi wanapokuwa wanakabiliana na wahalifu mara nyingi unapotokea uhalifu hasa maeneo ya mijini wahalifu wengi wanatumia magari kuhakikisha kwamba wanapokuwa wamefanya uhalifu wanakimbia askari.

Sasa naomba na naishauri Serikali ianzishe Kitengo maalum ndani ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya *Road Highway Patrols* hasa kwenye barabara kuu kwa mfano kutoka DaresSalaam/Chalinze/Segera,DaresSalaam/Chalinze/Morogoro,Sirari/Musoma/Bunda/ Mwanza, Namanga/Arusha na maeneo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kitengo hicho kiimarishwe kwa kupewa maaskari watakaoteuliwa kwenda kitengo hicho wapewe mafunzo maalum nyenzo na wawezeshwe kikamilifu na magari watakayopewa kwa ajili ya shughuli hiyo yasiwe haya ambayo sasa Jeshi la Polisi linayatumia kwa mfano *landrover.* Huwezi kuwa na *landrover* ukafukuzana na mtu ana gari ambayo ni ya Kijapan, wote tunaamini na kwamba tutumie gari ambazo zinaweza kushindana na zile ambazo majambazi na wahalifu wanazitumia.

Sasa mtakapokuwa mnapendekeza naona kwamba mmetengewa fedha nyingi hapa kwa ajili ya Jeshi la Polisi mwaka huu shilingi bilioni 5 na zaidi mnapopendekeza kununua magari kwa mfano mwaka huu kwa ajili ya Jeshi la Polisi basi angalieni namna gani mnaweza kununua magari ambayo yanaweza yakakabiliana na ambayo wahalifu mara nyingi wanayatumia na hasa magari ya aina *Toyota* ambayo ndiyo yenye mwendo mkali. Kwa kuimarisha kitengo hicho ninaamini itasaidia sana kuweza kudhibiti uhalifu unapotokea hasa maeneo ya mijini na mipakani wanapokuwa wanajaribu kukwepa nguvu ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, pili ni kwa upande wa Jeshi la Magereza. Napenda niishauri Serikali kuhusu Magereza yanayojengwa Wilayani hivi sasa na huko Mikoani. Hivi ramani zinazotumika hivi sasa inaonekana ni zile ramani za zamani. Inashangaza kuona kwamba miaka 40 ya Uhuru tulionayo Tanzania bado mtu amefungwa ambaye ni mwanadamu mwenzetu, mtu amehukumiwa mwaka mmoja, miaka miwili, mitatu na

zaidi, lakini bado yuko gerezani kule kule pamoja na shughuli zingine za kutenganishwa na familia yake mtu analazimika tena kubebeshwa kinyesi ndani ya ndoo gerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi la Magereza kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani wabadilishe ramani za mitindo ya sasa kwamba kwa sababu kulingana na hali tulionayo hivi sasa ni lazima twende na mabadiliko ya dunia kwamba mtu anapokuwa amefungwa gerezani basi ijengwe sasa Magereza ambayo yatakuwa na vyoo vya ndani yaani *self contain* na viwe *flashed.* Kwa sababu mtu anakuwa yuko gerezani ameachanishwa na familia yake pamoja na mambo mengine, lakini bado kule kule anapata adhabu ya pili kuondokana na ile ambayo amehukumiwa kutoka Mahakamani.

Mimi nadhani kitendo hiki kinaonyesha kwamba ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa hiyo, naomba niwashauri Magereza kwamba wapitie ramani zao za Magereza inaonekana labda zimeshapitwa na wakati na Magereza yatakayojengwa sasa katika maeneo ambayo yanahitajika yawe ni Magereza yatakayokidhi haja ya maisha ya Mtanzania wa karne hii ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati utakapokuwa una-*wind up* naomba hili nipewe maelezo kwa sababu wananchi wa Jimbo langu la Bunda wamenituma hili kwamba hivi sasa hili linahusu Idara ya Uhamiaji. Wananchi kama tunavyoelewa wanahimizwa washughulikie vyeti vya kuzaliwa kule vijijini. Suala la vyeti vya kuzaliwa linahitaji katika hatua zake ili mtu aweze kupata cheti ni lazima fomu zake ziidhinishwe na Idara ya Uhamiaji. Sasa katika Jimbo langu la Bunda kuna vijiji ambavyo kwa mfano mtu anatoka Kijiji kama Nanchimweru kwenda Bunda Mjini ni zaidi ya kilomita 80.

Sasa mtu anaondoka kule kijijini asubuhi anafika Bunda pale labda mchana saa 7.00 akianza kushughulika na suala la cheti chake cha kuzaliwa labda cha watoto wawili au watatu hadi kuja kumaliza akihitaji kuthibitishiwa na Idara ya Uhamiaji analazimika kusafiri kwenda Musoma Mjini zaidi ya kilomita 80. Kwa hiyo, hili linaongeza gharama kwa wananchi ambao wametoka vijijini. Inampa mtu kusafiri kulala hoteli na akifika Musoma anakuta wakati mwingine saa za Ofisi zimekwisha analazimika kulala. Sasa hii inakuwa ni shida sana.

Kwa hiyo, ombi la wananchi wa Bunda, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kabisa kwamba tufunguliwe Ofisi ya Uhamiaji wa Wilaya pale Bunda ili iweze kutoa huduma iwe kwa wananchi karibu Wilayani. Naamini kwa kufanya hivyo wote tunaelewa kwamba hivi sasa wananchi wengi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa likiwemo pamoja na Jimbo langu la Bunda wanaposafiri kuja maeneo ya Dar es Salaam wengi wanapenda mabasi ya *Scandinavia, Tawfiq* na *Takrim* wanazungukia nchi jirani ya Kenya. Vile vile wanahitaji kuwa na *passport.*

Mheshimiwa Spika, sasa watu wengi wafanyabiashara wanaosafiri pamoja na wanafunzi na watu wengine katika shughuli zao mbalimbali wanajikuta ili waweze kupata huduma hii ya *passport* ni lazima waende Musoma ambapo ni mbali.

Kwa hiyo, ombi hili Mheshimiwa Waziri kupitia kwako Mheshimiwa Spika, naomba atakapokuwa ana-*wind up* aniahidi na ni kwamba wananchi wa Bunda wanaomba na nijue kwamba ni lini tunaweza tukapata huduma hii ili tuweze kupunguza kero za wananchi katika maeneo yao na kupitia utaratibu huo ndiyo maana unaona kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imeondoa kero mojawapo ni kufuta kodi na hii nayo ni kero kwa wananchi kule vijijini naomba tusaidiane sana tuweze kufungua Ofisi ya Uhamiaji ili tuweze kuondokana na mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni pale nilipokuwa nikiangalia majedwali haya jinsi ambavyo kila Idara katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ilivyotengewa fedha. Mimi ninavyoelewa Wizara ya Mambo ya Ndani inazo Idara nyingi. Ina Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Zimamoto pamoja na Uhamiaji. Lakini katika mchanganuo tukisoma pale kwa mfano ukurasa wa 39 kwa idhini yako Mheshimiwa Spika, naomba nisome hapa. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba: "Shilingi 8,200,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo Jeshi la Polisi limetengewa shilingi bilioni 5, 300,000,000 na Magereza wametengewa shilingi 2,900,000,000 kama inavyoonekana katika jedwali la 18." Anasema: " Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja." Je, hivi Wizara ina Idara zaidi ya Polisi na Magereza. Lakini Idara ambazo zimeonyeshwa ni Magereza na Polisi peke yake. Je, Idara ya Uhamiaji pamoja na hawa Zimamoto wamewekwa katika kundi gani? *(Makofi)*

Suala hili nakumbuka mwaka 2001 limeongelewa hapa. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi akaahidi pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliyekuwepo lakini halikufanyiwa kazi. Mwaka uliofuata mwaka 2002 ikawa hivyo hivyo na mwaka huu imetokea hivyo hivyo na Idara hii kwa mfano Idara ya Uhamiaji ndiyo inayoshughulika na utoaji wa uraia kwa wageni. Idara hii hii ndiyo inayoshughulika na utoaji wa visa kwa wageni mbalimbali wanaokuja nchini, vibali vya kuishi nchini inakuwaje Idara kubwa kama hii haionyeshwi na Wizara hii kwa nini inamezwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na atupatie majibu mazuri ya kueleweka kwa nini Idara hizi mbili Idara ya Zimamoto pamoja na Uhamiaji hawatengewi fedha zao za maendeleo matokeo yake Wizara inajiegemeza kwenye Idara mbili tu ya Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Magereza. Ninaamini Mheshimiwa Waziri utakapokuwa una-*wind up* basi pamoja na haya utayapatia maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza nikushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Halafu nimpongeze Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake safi, nzuri na inayoeleweka pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na wataalamu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara hii kwa upande wa Polisi kwa jinsi walivyotekeleza yale malengo ya 2002 hadi 2003 kwa kuweza kukarabati mabweni,

kujenga baadhi ya nyumba za *Field Force* na hivi sasa wanajenga nyumba ya *RPC* kwa fulani kule na ile Kambi ya *Field Force* iliyopo Pemba ambayo kama haijafunguliwa karibu inafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa yeyote yule ambaye amepitia Polisi au Jeshi au ulinzi wowote akisikia kwamba kuna Kambi ya Kijeshi au ya Kipolisi ambayo inaweza kukaa Wanapolisi au Wanajeshi huwa anafarijika sana. Kwa sababu tukitaka tusitake vizuri askari wa Polisi wawe wako kambini kwao wanaishi humo humo. Mimi labda nitoe mfano mdogo tu au mkubwa wakati alivyouawa Marehemu Sheikh Karume.

Mimi nilikuwa mwana polisi na kwa muda wa miaka 12 sikulala *Barracks One Police Line* Zanzibar hata siku moja. Wakati kinatokea kitendo kile nilikuwa nje ya *Barracks One Police Line.* Saa moja usiku taa zimeshazimwa niko nje ya kambi najiuliza nitaingia vipi. Suala la kwanza, la pili, najiuliza je, nikiruhusiwa mimi kuingia hawajitokezi maadui wengine nikaingia nao pamoja. La tatu, najiuliza je, aliyeko mlango wangu ambaye ataniruhusu au nitauawa kipumbavu. Hoja hizo zilikuwa nzito sana.

Baada ya kufika tu karibu ya lango lile sikwenda mchomo kwanza nikakaa pembeni chini ya mwembe, akaenda askari mmoja wa kwanza akasema afande fulani pita uko nje tu, tako la bunduki ndani. Akaenda wa pili, wa tatu na wa nne, baada ya kusikia sauti zote zile nzuri safi za askari wenzangu ndiyo nikaanza kuingia. Kwa hiyo, nilivyosikia haya tu mimi nimefarajika vizuri sana na naipongezi Serikali ya Jamhuri ya Muungano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba polisi ni kioo cha nchi yoyote ile hapa ulimwenguni. Mtu yeyote akienda sehemu yoyote akishashuka tu kwanza anatazama Polisi wamekaa vipi. Anatazama mapokezi ya Polisi na Polisi uzuri wake na ubaya wake kazi zake zimekaa bayana nje zinaonekana. Ndiyo maana Polisi akifanya mazuri yanaonekana lakini akifanya baya kidogo nalo linaonekana haraka.

Kwa hiyo, lazima tuisaidie Polisi kwa hali na mali na tukiri kwamba wanafanya kazi katika hali nzito na mazingira magumu na hasa kutokana na mwongozo huu uliopo kwamba askari mmoja anatakiwa awe na watu wa kuwalinda 400 na sasa hivi tumefika watu 1,500 kwa askari mmoja, lakini najua wazi baada ya sensa hii iliyomalizika watazidi hawa. Hii labda ilikuwa milioni za nyuma sio milioni 34 za sasa.

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, nawaomba wananchi washirikiane na Jeshi la Polisi kutoa msaada wa hali na mali ili kusaidiana kuleta amani na utulivu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile isiwe raia tu au wananchi ndio wanasaidia Jeshi la Polisi kuleta amani na wao Polisi wawe pamoja na wananchi kuleta amani na ushirikiano wakati wanapopeleka taarifa mbalimbali tena wasiwabughudhi wasiwe wanauliza kuna ushahidi gani umeyapata nani, amekwambia nani aah hawawezi kuwa wanajipendekeza na kwenda wakasema kwamba taarifa hii ameipeleka fulani lakini kwa hivyo itabidi tuje, tusingekuja maadamu taarifa hii ameipeleka fulani tunakwenda.

Kwa hali hiyo, wananchi watashindwa kulisaidia Jeshi la Polisi na Jeshi la Polisi likiwa halisaidiwi na wananchi, usalama utakuwa haupo na hata takwimu zinaonyesha hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuongelea ukurasa wa 17 wa kitabu chetu kuhusu Maafisa wetu wa Polisi ambao wamefanyiwa semina ya muafaka. Polisi na muafaka ni mbali kabisa, muafaka ni wetu sisi Wanachama pamoja na Viongozi wa Vyama, lakini kama hatutaenda nao vizuri na ukivunjika tu, Polisi ni lazima wachukue mkondo wa Sheria. Kwa kuwa muafaka upo Zanzibar tu isije ikawa tena Polisi wanasema: “Muafaka bwana, aah.” Mambo yaliyopo sasa Zanzibar, ndugu zetu wanajenga mahali popote, ukimwambia: “Usijenge” anasema: “Aah, muafaka bwana.” Ukimwambia: “Ndio ni muafaka na Sheria je?” Anakujibu: “Tutaonana 2005.” Kwa hiyo, Polisi na muafaka *different* kabisa, *positive and ...*

**MBUNGE FULANI:** *Negative. (Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** *Positive and negative,* hiyo hiyo. Wasizubae, wasilale na muafaka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yupo msemaji mmoja hapa amesema hivi: “Tunashukuru uchaguzi umekwenda vizuri na Polisi wanafanya kazi nzuri.” Napenda kusema kwamba, Chama cha Mapinduzi ndicho kilichoendesha vizuri uchaguzi wa Pemba. *(Makofi)*

Jambo ambalo mwaka 2005 halitatokea kama lilivyotokea Pemba, kwamba watu wameishi Tanzania Bara kwa muda wa miaka 15 wasipige kura, wamekataliwa tena tukubali hilo ng’o halitatokea! Au watu kutoka Unguja wamekwenda kule na wanasema: “Huyu hafai, asipige kura” hilo hatutalifumbia macho na hatutakubali hata dakika moja, kwa sababu muafaka haukuja ili Mapinduzi yaondoke Zanzibar na nchi ichukuliwe kirahisi! CCM Zanzibar na CCM Tanzania Bara hatutakubali hata kwa dakika moja. Ni wajibu wetu wote kulinda muafaka wetu, kufuata muafaka wetu na kufuata Sheria, hapo ndipo kazi za Polisi zitakwenda vizuri, tukivunja Sheria, Sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kwamba, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mwera, hawa Askari ambao wako Pemba wanaulizwa wanafanya nini, basi Mwera ninawataka waje walinde. Kama wao hawawataki, basi mie nawataka. Sisi viongozi hapa tusionyeshe udhaifu wetu, ikiwa unasema askari polisi au askari mwingine anafanya nini nchini na si askari wa Kiingereza wala si Mrusi, unakusudia nini! Inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu *PGO.* Wenzangu wengi wamezungumzia suala hili, lakini hawajafafanua. Huu ni mwaka wa tatu ninapigia kelele suala hili, hii *Police General Order* ninakiri kwamba ilisimamishwa siku za kikoloni.

Hii *PGO* ina mambo mengi tu ambayo mengine ni maslahi kwa Jeshi la Polisi na mengine si maslahi kwa Jeshi la Polisi, mengine yamefutwa na mengine bado.

Mheshimiwa Spika, juzi kuna swali la nyongeza lilijibiwa kwamba kuna Sheria Askari Polisi akae Wilayani kwa muda wa miaka mitatu, Mkoani ni miaka sita, lakini suala hilo halifanyiki kutokana na hali yetu ngumu ya uchumi. Halafu kuna Sheria kwamba Askari mmoja alinde Wananchi 400, lakini Askari mmoja analinda Wananchi 1,500, hapo hatukuelewa! Sasa, kwa nini na hii *PGO* isirekebishwe? Leo Askari Polisi wa Tanzania ana Mikataba zaidi ya minne ndani ya Jeshi la Polisi kama Jeshi hilo tumelikodi! Mkataba wa miaka mitatu aende *re-engagement*, sita aende, tisa aende, kumi na mbili aende, hee, sasa ikishafikia miaka 12, kweli Waziri husikitiki kuona askari yule anaacha kazi! Au umwambie utaongeza tena miaka mitatu au ni vipi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumaini ikifika miaka 12, askari yule moja kwa moja awe *pensioner,* kama hakuwa *pensioner,* basi aache pale pale! Akishafika miaka 12 hana uwezo wa kuacha kazi na hao wakiacha kazi ndiyo wanatutaabisha, wanatukera na hivi sasa wako zaidi ya 400 ambao Mkataba huu umewabana. Kwa hiyo, naomba marekebisho yafanywe na wale walionasa kwenye Mkataba huo wapate *offer,* wasamehewe ili wafanye kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mtu anafanya kazi kwa muda wa miaka 25 au 28 unampa shilingi 8,000/=!

**MBUNGE FULANI:** Au ni milioni nane?

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Siyo shilingi milioni nane, ni shilingi 8,000/=! Eeeh, atafanya kazi kweli? Baada ya miaka mitatu anajua kwamba yeye siyo Afisa tena, kwa sababu ukishakuwa Afisa tu unaruka, haki ya Mungu hatafanya kazi, atajiimarisha kwa rushwa tu! Naomba na suala hili litazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu mafunzo. Kuna mafunzo mengine madogo madogo na kwa jinsi wakati unavyokwenda ni lazima tuwe nayo, mfano ni sarakasi, judo na kadhalika. Leo watoto wadogo wanajifunza judo na tukiona watoto wanajua judo, tunaanza kutumia nguvu! Ndio Polisi inavyokwenda namna hiyo! Kwa hiyo, mafunzo yaliyopo kwenye uwezo wetu ni lazima tujifunze na tuwafundishe askari wetu wa Polisi ili waende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisije kusahau kuunga mkono hoja hii, lakini namuomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atembelee katika Jimbo langu akague *Police Stations* za Mwera, Fuoni na Mwanakwerekwe. Japokuwa *Station* ya Mwera anaijua, lakini naomba aje tu atazame jinsi hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI SHEHA MUSSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nitakuwa na mambo matatu, manne, tu ya kuchangia kwa sababu mengi yamekwishachangiwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwashukuru wenzetu polisi, kwani wanafanya kazi sana. Wanafanyakazi usiku na mchana hata kama sisi tumelala, wao wanakuwa macho na wanaifanya kazi hiyo kwa mazingira magumu, lakini hata hivyo Mungu atawasaidia na sisi Mungu atatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo napenda niwe wazi na nimpe pongezi maalum Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai, Ndugu Adadi Rajab. Nimesema hivyo kwa sababu sasa hivi nchini mwetu kunatokea mambo makubwa sana ya mauaji na mambo mengine mazito mazito, siyo mepesi mepesi, lakini maskini kijana huyo anafanya vizuri, wewe kaa siku mbili tu utapata habari zote, mambo yote hadharani unayaona. Kwa hiyo, sina budi kulipongeza Jeshi la Polisi na hasa Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai kwa jinsi anavyofanya kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika kipindi cha nyuma niliiuliza Serikali swali juu ya *Speed Monitor* kule Zanzibar kwamba upande mmoja wa nchi una Vyombo kama hivyo na mbona upande mwingine hakuna? Serikali ilijibu kwamba suala hilo litapelekwa Baraza la Wawakilishi. Baraza la wawakilishi limekaa mara mbili na sisi tumekaa mara mbili, lakini mpaka leo hii ufafanuzi bado haujapatikana!

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar ajali ni nyingi sana. Kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, barabara zetu ni ulimi wa nyoka yaani ni nyembamba sana na vijana wa daladala tulionao kule wanaendesha kwa sana. Ndiyo maana tunaomba chombo hiki kije pengine kinaweza kupunguza ajali ama kitasaidia. Askari wa *traffic* wakikitumia vizuri, wananchi wetu wataokoka na ajali hizo za kipuuzi puuzi. Naomba Serikali ipeleke hoja hiyo Baraza la Wawakilishi, japo wao wana hiari ya kukubali ama kukataa!

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuzungumzia kuhusu ujenzi wa *barracks* katika Mkoa wa Kaskazini hasa pale Mahonda. Mkoa huo una watu wengi sana na una maeneo mengi muhimu ya vitega uchumi kama kule Kiwengwa, Mchangani, Nungwi na kadhalika. Pia, kuna msongamano wa matukio mbalimbali, lakini Askari ni wachache. Sasa, tukijenga hizi *barracks* watakuwepo wengi na tatizo likitokea wanaweza kulikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hilo ni muhimu sana, japokuwa najua kwamba hali ya uchumi ni ngumu, lakini hata hivyo barracks zianzishwe hata kama yatakuwa ni mahema, ili inapotokea mambo mbalimbali madogo madogo ya hatari vijana wetu waweze kukabili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, sasa hivi nimegundua tatizo lingine pale *Dar es Salaam Custom* kwa vijana wetu wa Polisi. Sisemi kwamba wanahusika, lakini kuna harufu ya rushwa inaweza kuwakuta! Pale kuna boti na ninajua zinahusika na watu

wa Mawasiliano na Uchukuzi, lakini Polisi wanafanya kazi ya kusaidia saidia. Sasa hao wenye boti wameanzisha mtindo, ikifika saa sita wanakwambia tiketi hakuna, lakini majibu atakupa askari kwamba: "Mzee kama unataka kusafiri onana na mtu fulani hapo!" Haya mambo kidogo yananichanganya! Ushahidi ni tarehe 04 Julai, 2003 niliona jambo hilo pale na jambo hilo sikulipenda kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, askari wetu nimewasifu sana hapa kwa jinsi wanavyofanya kazi vizuri, lakini miongoni mwao wawili, watatu, wanataka kutumbukia kwenye mtego ambao sipendi waingie. Naiomba Wizara husika itupie macho sehemu hiyo, kwani jambo hilo linaudhi sana, si zuri kwa askari polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu vitambulisho. Sasa wakati umefika kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwapa Wananchi wake vitambulisho. Jana katika kumuulizia swali Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, kuhusu vitambulisho katika Jimbo lake la Nungwi na mie Jimbo langu la Mkwajuni, nilisema wageni wanaotumia njia ya bahari ni wengi sana na wanakuja makundi kwa makundi, huwezi kuelewa kama hawa wanatoka Bara, wanatoka Kenya au wanatoka pengine, wanatumia tu bahari. Masheha peke yao hawawezi kuwadhibiti, naomba vitambulisho viharakishwe ili tuelewane kwamba huyu ni wa wapi na huyu ni nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sipendi kuwa na maneno mengi sana ili yasiharibu maana. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Pia napenda kuwapongeza Watendaji wote, nasema wote kwa maana ya mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja napenda nianze kuzungumza yale niliyokusudia. Kwanza, ni kuhusu kustaafishwa kwa Askari katika Jeshi la Polisi. Utaratibu unaotumiwa nadhani una matatizo, nasema una matatizo kwa sababu si busara kwa mfanyakazi wetu ambaye tumekuwa naye labda zaidi ya miaka 10 au 20 na tunakuwa tunamuenzi na tunampa sifa zote, lakini inapofikia mahali anastaafu kutokana na utaratibu wa kisheria, inachukua miaka 6 au 10 hatujampa haki yake! Nadhani kwa vyovyote vile si uungwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeeleza tatizo, lakini pia napenda kushauri kwamba, wale watendaji wote wanaohusika na mambo haya ya pensheni na viinua mgongo, waandae kabisa mambo yao kwa sababu wastaafu wanaeleweka. Kwa sababu tunajua kabisa kwamba ni askari wetu wangapi mwaka ujao watastaafu, basi tuwaandalie mazingira mazuri. Mfano, mtu amestaafu labda mwaka 2000 mpaka mwaka 2007 au 2010 hujampa haki yake, unamwezesha mtu huyo kufanya jambo lolote baya katika nchi hii na

ndiyo maana wakati mwingine huwa tunaona wanashiriki katika vitendo vya ujambazi, mambo mabaya kama ulanguzi na kadhalika. Sasa, ninaishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, iandae utaratibu mzuri kuhusiana na hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia hapa ni kwamba, mfano inapotokea askari ana cheo fulani na bado ana kama siku 20 ili apate cheo kikubwa zaidi ya kile alichonacho, utashangaa kuona mtu yule anastaafishwa wakati yeye mwenyewe amekwishajiweka tayari kwa kile cheo kipya! Hali hii inatokea sana kwamba ikiwa askari ana muda mfupi ili apate cheo kipya, yanaandaliwa mazingira ya kustaafishwa kiasi kwamba anakuwa na huzuni na masikitiko makubwa, kwa kuona kuwa labda hakutendewa haki na mambo mengine kama hayo. Hili naliona kama ni tatizo na ninaomba Wizara iliangalie na ikiwezekana basi iandae utaratibu mzuri kulingana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, uzoefu unaonyesha hasa kule Zanzibar kuwa askari wengi wa Jeshi la Polisi na Majeshi mengine wanapostaafu yaani utashangaa, hata kama labda alikuwa na cheo cha juu kidogo hata mwezi mmoja haumalizi utakuta askari yule ameanza kuhangaika! Wengine wanapika gongo na wengine wanaajiriwa kwenda kulinda sehemu ambazo kwa kweli kulingana na cheo alichoachia kazi haistahili! Sasa, huwa najiuliza hivi huko kwenye uaskari kuna tatizo gani? Kwa sababu haiwezekani mtu umefanya kazi vizuri na kwa heshima zote, baada ya mwezi mmoja unaanza kuhangaika mara umefukuzwa huku umeenda kupika gongo, mara umepita na machupa, mara umechukua maji kwa mzegazega, kwa kweli hapa tunawashushia hadhi hawa askari wetu. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULENI:** Waambie!

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Spika, hawa askari labda wanapokuwa katika zile nafasi zao za uongozi au katika shughuli zao za kazi, hakuna vile vipindi ambavyo wanawekwa labda na viongozi wao wa juu ili kupewa mawazo au hali halisi ya kule uraiani wanakokwenda. Napendekeza kwa Jeshi la Polisi, kuwe na uratatibu wa kuwaeleza hawa askari na hasa wale ambao wamebakisha kama miezi sita au pungufu kidogo kustaafu kwamba, jamani mtakapokwenda huko uraiani kuna hali hii na hii ili isifike mahali mtu anafanya vitu kiasi ambacho unaweza ukashangaa kwamba, huyu ndiye alikuwa anazuia haya mambo, lakini leo yeye ndiye amekuwa mstari wa mbele kuyafanya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuzungumzia kuhusu askari wa Kikosi cha *FFU*. Nimekuwa nikizingumza na askari hao mara nyingi na inavyoonekana ni kwamba, ukimkera labda kiongozi wako wa juu au ukiwa hupendezi kituoni basi utapelekwa *FFU* na nina ushahidi kamili! Mara nyingi najiuliza, hii *FFU* ndiyo sehemu ya kuwapa adhabu hawa askari wetu? Kama hivyo ndivyo, mbona tunafanya mambo ambayo si sahihi, kwa sababu hao ndiyo wanawalinda Marais, Makamu wao na watu wengine! Nadhani hali hii siyo sahihi. Nitamwomba Waziri atakapokuwa anatoa maelezo, atueleze labda ni sababu zipi zinazomfanya askari apelekwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni sababu za kuwahamisha askari kutoka kituo kimoja hadi kingine. Ilielezwa kwamba askari anatakiwa akae miezi sita au zaidi Wilayani na Mkoani ni miaka sita kabla ya kuhamishwa, lakini inaonekana kwamba askari anapofanya kazi zake vizuri katika kituo kimoja na ikabainika kwamba baada ya shughuli zake za kazi anajiendeleza na shughuli zake nyingine, labda za kufanya biashara ndogo ndogo na ikibainika kuwa shughuli zake au maisha yake yanakwenda vizuri ukilinganisha na baadhi ya Askari wengine walioko pale, askari huyo atapewa uhamisho hata kama hautaki na hata kama muda wa kuhama haujafika!

Mheshimiwa Spika, huwa ninashangaa sana kwa suala hilo! Je, tunataka hao askari wetu waweje? Tunajua kwamba mishahara tunayowapa haikidhi haja, lakini inapotokea askari anajituma baada ya shughuli zake za kawaida inaonekana ni tatizo, hatimaye anatafutiwa mambo mengine, anafanyiwa utaratibu wa kuondolewa pale ili huko atakakokwenda akaanze tena maisha! Kama Mheshimiwa Waziri hajui suala hili, sasa ajue kwamba lipo na alitafutie utaratibu ili inapotokea kwamba askari ameji-*organize* vizuri sehemu na kazi anafanya vizuri, basi ule utaratibu wa Sheria zilizopo uachwe ili uchukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu askari na matatizo ya madawa ya kulevya. Niliwahi kuuliza hapa kwamba wanaoleta madawa ya kulevya wanajulikana, lakini cha kushangaza wanaokamatwa ni wale wadogo wadogo yaani wavutaji na wauzaji, ni kwa nini? Nilipojibiwa, nilipewa tu majina hapa mawili, matatu, lakini hali kila siku inazidi kuwa mbaya, askari wapo, madawa yanaletwa na kesi Mahakamani hazimaliziki! Nadhani hapa kuna tatizo na tatizo hilo tusipoangalia sijui litatufikisha wapi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na ule utaratibu wa kuwaonea wadogo, lakini wakubwa wapo, wanajulikana na wanatazamwa hivi hivi! Nashauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Serikali kwa jumla watuonyeshe uthabiti wake kwenye jambo hili la madawa ya kulevya. Si busara kusema tu tunapiga vita, kwamba wasiyalete, wasiyaingize, lakini wakishayaleta hawakamatwi japo wanaoleta wanajulikana na wakikamatwa kesi hazifiki mwisho na wala hutasikia mhusika amehukumiwa vipi! Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup,* atupe maelezo mazuri kwamba wale waletaji hasa wanaotuma vijana wetu wamefanywa nini na siyo wale wadogo wadogo ambao wameweka tumboni tembe mbili, tatu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuongelea kuhusu mishahara ya askari polisi. Mwaka 2002 kuna baadhi ya askari polisi wawili au watatu walinifuata na wakaniuliza: "Sasa Mheshimiwa mmetufanyia nini? Mmesema mmeongeza kima cha chini cha mshahara, lakini kwenye mshahara wangu wangu nimeongezewa shilingi thelathini!"

**MBUNGE FULANI:** Siyo 30,000/=?

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Hapana, siyo 30,000/=, ni shilingi thelathini yaani kumi kumi tatu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilishindwa kumjibu huyo mtu, nikamwambia: "Safari hii mambo yenu yatakuwa mazuri, nitawaeleza wahusika."

Sasa napenda kushauri kuhusiana na mishahara hiyo. Huwa tunasema hapa kwamba, tutaongeza kima cha chini kwa asilimia 25 na wanaofuata itafika asilimia 10. Lakini wale tuliowapa kazi za kupanga hii mishahara nao ni binadamu, wana mapungufu chungu nzima, ukiacha hayo ya kawaida kama binadamu, huwa wana matatizo na watu wengine katika shughuli za kawaida na hiyo tunajua. Naomba ziundwe Kamati maalum kila mahali ambapo tunahisi kwamba tuna matatizo kama Polisi na Taasisi nyingine zinazohusika kwamba wanaoshughulika na mishahara, basi tunaposema kina cha chini tutaongeza labda kwa asilimia 25 au 10 iwe ni hizo asilimia kweli kwa wale wote wa kima cha chini. Isitokee kama ilivyotokea mwaka jana kwamba wengine wamepata fedha chungu nzima na wengine wanapata shilingi thelathini kama nilivyopata malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote napenda kuwapongeza Wabunge wapya walioungana nasi katika Bunge hili, ambao ni Wabunge wa *CUF* na Wabunge wa CCM, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba nzuri ya Bajeti ambayo ameitoa na pia kwa kazi nzuri ambayo inafanywa chini ya Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kutoa pongezi kwa Idara ya Polisi kwa kazi nzuri ya kukamata majambazi. Hasa napenda kumpongeza afande Alfred Tibaigana na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kusambaratisha majambazi hao ambao wanatuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutoa pongezi kwa kazi inayoendelea kufanyika katika Vituo mbalimbali hususan Kituo cha Polisi cha *Salender Bridge,* kazi ya ujenzi ni nzuri sana, kile kituo nimekiona miaka nenda miaka rudi, nadhani kwa mara ya kwanza ndiyo nimeona kinakarabatiwa sasa hivi, lakini kazi ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona kuna matarajio ya Wizara ambayo yameainishwa, napenda kutoa hongera ya kuamua kukarabati Vituo na Ofisi za Polisi mbalimbali zikiwemo za Mkoa wa Mara na Sirari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hili ningependa kusisitiza sana kwani nafurahi kusikia kwamba kutakuwa na ajira za polisi wapya 370. Sasa naona hapa kunatokea ubishi kwamba hao polisi waajiriwe kutoka wapi. Mimi ningependa kushauri kwamba hao polisi waajiriwe kutoka Mkoa wa Mara. Kwa sababu sisi wananchi wa Mara kazi ya uaskari kwetu iko ndani ya damu. *(Makofi)*

Ningependa kusisitizia hili kwa sababu kulikuwa kuna vijana wawili wa Mara ambao walikuwa wanasoma shule pamoja. Mmoja alikwenda kufanyakazi Dar es Salaam mwingine katoka Bara baada ya muda mrefu akaja Dar es Salaam akamkuta mwenzake posta anafanyakazi. Akamuuliza, unafanya nini hapa, akamwambia, nafanyakazi. Akamwambia Chacha unashindwa kwenda kufanyakazi *zesi* (Jeshi)*,maghereza* (Magereza), *borisi* (Polisi) *angharau mghambo unakuja kuramba stembu." Unaramba stembu* (kuuza stempu katika Shirika la Posta) *hata mghambo?* Hakuweza kuelewa kwa kweli! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi badala ya ubishi wote wa kwamba aajiriwe nani, ajira leteni Mkoa wa Mara. Hii kazi ni yetu. Kuna binti mmoja alichumbiwa akaenda kule akaulizwa huyo mchumba wako anafanya kazi gani, akasema ni *Wasiri* (Waziri). Akamwambia mwongo anakudanganya hicho cheo kwenye *zesi* (Jeshi) hakipo! Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri ataweza kutatua hili tatizo kwamba ajira ipelekwa wapi ya hawa polisi 370. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nimetoa hongera, nimempongeza Bwana Alfred Tibaigana, kwa kazi nzuri na ningependa kusema kazi ni nzuri sana na iendelee kuweko na *consistence,* isisimame hata siku moja ikawa kama ni nguvu ya soda, iendelee mpaka hawa majambazi wajue kwamba jeshi la polisi limepata wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili ningependa kuzungumzia kuhusu mambo mawili au matatu juu ya makazi ya askari polisi hayaridhishi kwa kweli. Hata tukienda hapa Dodoma tu wanakaa kwenye zile nyumba za *fullsuit* kama Mheshimiwa Mbunge alivyozungumzia leo asubuhi nyumba za *full suit* ya bati kutoka juu mpaka chini, jua hili mchana, baridi hii usiku yaani ni hali ni mbaya sana hata kama ni polisi lakini ni binadamu wana hali mbaya sana. Kwa hilo naomba liangaliwe. Hata kule Mkoa wa Mara, Musoma nyumba za askari ziko mbali kidogo, lakini huku barabarani yanakuja maji machafu kutoka majumbani kwao yanatembea mpaka barabarani. Sasa huko kwao kwenyewe kukoje? Nadhani tunaelewa nikisema maji machafu ni nini siyo ya kuoshea vyombo. Hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni mambo madogo madogo lakini mambo makubwa makubwa, *speed* ya magari. Tuliambiwa kwamba kuna *speed governors* sijui kama bado zinafanya kazi au hazifanyi kazi. Sijui *speed limit* ni ngapi, hasa *public transports,* mabasi yana *speed* sana.

Mimi huwa napanda mabasi kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam na kurudi. Mabasi yanakwenda mwendo wa kasi sana. Hii inahatarisha sana usalama wa abiria wetu.

Kuna wakati pia nilipanda basi nilikuwa natoka Bunda naelekea Mwanza, nikapanda *Bunda Bus,* lilikuwa linatoka Sirari, basi hili lilikuwa linakwenda kwa kasi. Ukiongea na kondakta na hata abiria pia wanakutukana wanakwambia kwamba hii *speed* wala siyo kubwa yaani waendelee kuongeza *speed.* Wanafukuzana na basi lingine la nyuma, wanajuana. Aah, yule kule nyuma ni dreva fulani, yule Jumanne anaendesha gari kweli.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda hivyo tulinusurika lakini baada ya siku nne ikatokea ajali mbaya sana ya *Bunda Bus* iliua watu wengi dreva pamoja na kondakta wa *Bunda Bus* hiyo hiyo iliyokuwa inatoka Sirari ikielekea Mwanza. Lakini inaelekea kwamba mchezo huo wa madreva kufukuzana wenye mabasi unajulikana sana hata na abiria wanajua hilo kwa hiyo, haiwezekani kwamba polisi hawajui. Kwa hiyo, hilo suala lingeangaliwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu uvunjaji wa sheria barabarani, kuna *zebra crossing.* Mtu anayetembea kwa miguu akifika kwenye *zebra crossing* gari linapaswa kusisimama ili aweze kupita. Lakini madreva wakiona watu wanavuka wanaotembea kwa miguu wao ndiyo wanakanyaga *accelerator* kama vile yeye ndiyo mwenye haki ya kuvuka kwenye *zebra crossing.* Sielewi kwamba hawaelewi sheria au tatizo ni nini. Wakati mwingine kwenye *zebra crossing* anakuwepo *traffic police* yeye mwenyewe ndiyo kwanza anaruhusu magari yapite. Pale kwenye zebra *crossing* kuna watu, watoto wa shule wanataka kuvuka lakini hawawezi kuvuka hata *traffic police* mwenyewe badala ya kuwasaidia *pedestrians* wavuke hawezi kuwasaidia. Hilo pia nafikiria kwamba lingeangaliwa kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukizungumzia ambacho ni cha mwisho ni mambo madogo madogo lakini mambo makubwa makubwa. Ni jinsi askari wanavyoshika silaha barabarani siyo wote lakini wapo baadhi. Anashika silaha, mtutu unaelekea mbele badala mtutu kuelekea juu. Hii ni hatari sana. Kwa sababu bahati mbaya akiwa hajafunga *safety catch* yake vizuri risasi ikitoka inaweza kwenda na mtu. Lakini kama imeelekea juu basi tunajua kwamba labda sana sana ataua ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa haya machache ningependa kusema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hii Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote nataka nichukue nafasi hii, kukupongeza sana wewe mwenyewe kwa kazi yako unavyoifanya ya Uspika ndani ya Bunge hili. Nimekuwa nafuatilia katika nchi za Kiafrika kuna Maspika wengi, lakini miongoni mwa Spika aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Mabunge ya *Commonwealth* ni wewe. Sifa hizo ni za kwako lakini ni za Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapotamka kwamba siku za usoni hatakuja hapa kutusaidia sisi wenzako unatuacha kwenye mataa. Tungekushauri mambo haya usiwe

unatamkatamka kwa sababu sisi ndiyo tuliokuchagua tutakapochoka tutakuambia usijali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba nichukue nafasi hii niwapongeze rafiki zangu wote ambao wamepata nafasi ya kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, wale wa Chama cha Mapinduzi na wale wanaotoka Chama cha wWananchi *(CUF).* Nawakaribisha sana na kuwatikia kila la kheri katika kazi hii ya Ubunge. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Waziri ana jina la Mapuri. Watu wa Kusini wanasema tafsiri yake ni ndovu lakini usahihi ni tembo. Kule Zanzibar aliwahi kutunga kitabu, kile kitabu alipokitunga wasiompenda wakamwita Ngosha, kumbe ukitaka kumsifia mtu wa maeneo yale ukimwita Ngosha maana ni mwanaume hasa aliyejitahidi aliyejikusulu. Sasa huyu Ngosha anaonyesha hasa kazi katika kupambana na majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimpongeza Naibu Waziri kwa kazi nzuri, Katibu Mkuu, *IGP* na viongozi wote, watumishi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini nimpe pongezi za makusudi Kamishina wa Polisi Zanzibar kwa jitihada zake za kazi nzuri na kwa usikivu na ushirikiano wake. Namwomba na namwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumsaidia kumpa hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wamewapongeza Ma-*RPC,* mimi nataka nimpongeza *RPC* wa hapa Dodoma ndugu Gumbo, ingawa simjui. Nimekuwepo hapa Dodoma kwa mfululizo sasa ni mwaka wa 17 nakuja na kurudi, nimeviona vituko vingi, lakini wakati wa *RPC* Ndugu Gumbo, vituko hivyo vya majambazi na wale wezi wa vichochoroni vimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Namwombea kazi njema, namtakia kila la heri na Mwenyezi Mungu ampe uwezo wa kuipenda vizuri kazi yake zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka na mimi niiombe kwa makusudi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mimi natoka Jimbo la Dole ambalo halina Kituo cha Polisi. Siyo kwamba halina kituo cha polisi kwa sababu ndiyo kuna amani na utulivu na watu hawana makosa, hapana! Inawezekana ni kwa sababu zisizoweza kuepukika, lakini pengine ningeomba Serikali sasa ichukue juhudi za makusudi za kujenga Kituo cha Polisi Jimbo la Dole pengine itasaidia kuwaweka wananchi katika hali ya ulinzi na usalama na sisi tujivunie kwamba tunacho chombo chetu cha Serikali. Hilo ombi langu la kwanza. *(Makofi)*

Lakini lingine ambalo wenzangu wengi wamelizungumza na Mheshimiwa aliyemaliza hivi sasa namuunga mkono amezungumzia kuhusu ukarabati wa nyumba za polisi. Ndugu zetu hawa wa polisi wanaishi katika maisha magumu sana. Wanafanyakazi katika Taifa letu kwa uzalendo na uaminifu na upendo, siyo kwa sababu ya mazingira yenyewe. Nyumba wanazoishi baadhi ya nyumba ambayo anazotakiwa kuishi mtu mmoja wao wanaishi familia zaidi ya tatu na hili si jambo la kusema utafute utafiti

hapana! Hata sasa tukitaka tuandamane na Mheshimiwa Waziri, twende hapo kwenye nyumba za mabati utaikuta hiyo hali utawahurumia sana.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale Zanzibar Ziwani ukaingia mle ndani kuna nyumba zimejengwa mwaka 1963 na 1965 hazijafanyiwa ukarabati mpaka hivi leo. Vyoo wanavyotumia wale vijana wa polisi hakuna sababu kwamba kusiwe na kipindupindu. Lakini kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu yupo hali ya vyoo si nzuri, nyumba zao si nzuri, wanaishi katika hali ngumu. Kwa hiyo, naiomba Wizara pamoja na jitihada za makusudi inayofanya iongezee bajeti kwa askari polisi. *(Makofi)*

Lakini la pili, tunaelewa kwamba kila askari anayeingia au mtumishi anayefanya kazi anategemea baada ya kustaafu apate mahali pa kupumzika. Mara nyingi askari polisi akistaafu ama atakuwa mpishi wa gongo, ama atakufa kabla ya wakati wake. Kwa sababu askari wengi polisi akihamishwa Dar es Salaam akija Dodoma nyumba ipo, akihamishwa Dodoma kwenda Mwanza anafikia katika nyumba. Mazingira ya kukumbuka kwamba ajenge nyumba hayapo, uwezo wa anachopewa kwamba kitabakia katika ujenzi hakipo. Naiomba Serikali kwa jitihada za makusudi kabisa kwamba iandae mkakati wa makusudi wa vijana wa jeshi la polisi wapewe mikopo maalumu ya vifaa vya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunaweza tukawasaidia vifaa vya ujenzi hawa vijana wetu bila shaka watakapostaafu watakuwa na uwezo mzuri wa kuishi mahali pazuri na hili litawasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia utendaji wa jeshi la polisi, ukilinganisha miaka iliyopita na mwaka huu unagundua kwa kweli kazi ya jeshi la polisi kwa mwaka huu ni nzuri na hatuna sababu za kusema kwamba kazi yao ni mbaya ni nzuri. Lakini ukifanya kazi katika chombo cha dola, ukifanya kosa dogo tu hasa polisi, unaweza ukasababisha amani katika nchi ikapotea mara moja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa yako matukio ya ujambazi yanayoshughulikiwa na polisi na wanayashughulikia kweli kweli na wanapopambana na jambazi wanapambana kweli kweli kwa sababu ama yake ama ya kwake. Lakini sasa Tanzania ni nchi moja ambayo duniani imesifika kwa suala la utulivu na amani, hilo watu wote wanajua. Lakini sasa hawa wenzetu wanapofanya hiyo kazi hivi haya matukio tunayosikia majambazi watano wameuwawa na polisi, sita wameuwawa na polisi, watatu wameuawawa na polisi hivi ni chombo gani kinachothibitisha kwamba waliouwawa kweli walikuwa ni majambazi?

Mheshimiwa Spika, Mbunge mwenzangu kama alivyosema kwamba askari wanashika silaha vibaya. Kwa mfano, pale Manzese ilitokea siku moja kulipokuwa na maandamano yaliyofanyika Mwembechai, askari wakapita wakamkuta kijana anachonga katika sehemu yake, akatandikwa risasi.

Sasa kitendo kama hiki kwa kweli wananchi imani yao kwa chombo cha dola inapungua, ikipungua watafanya jambo lolote lile litakalotokea, wakifanya jambo lolote nchi itakuwa haina amani. Sasa hili ningependa mimi nielimishwe kwamba matukio

kama haya yanapotokea wahusika wanathibitisha vipi ndani ya Serikali au mahakamani kwamba yule aliyehusika kweli ni jambazi? Ili kuondokana kwamba mtu anaweza kuwa na chuki binafsi, basi kwa sababu na mimi nimeshashika silaha jana tuligombana kwa sababu ya mama fulani na leo nina silaha nitakushughulikia na nikasema hili ni jambazi sugu. Nikishamaliza kusema jambazi sugu basi maneno yamemalizika.

Sasa nilitaka nielewe hapa Waziri anisaidie baadaye kunielimisha kwamba kipo chombo ambacho likitokea tukio kama hili askari ambaye anajieleza au mazingira kwamba yule aliyeuwawa ni mtu kweli alikuwa ni jambazi na askari anabakia kwamba yeye ni raia mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nizungumzie kwa kifupi sana suala la uhamiaji. Idara ya Uhamiaji ni idara inayojulika, kwanza ni idara ya Kimataifa inajulikana nje na ndani lakini ni idara ambayo ni nyongofu maana ni idara ambayo iko kama yatima hivi.

Kutoka mwaka 1964 imekuweka Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Idara hii mpaka leo haina *Vote* yake yenyewe ya matumizi. Idara kubwa kama hii ambayo ina mambo makubwa ya kimataifa ya ndani haina vote yake. *Vote* inayotumia ni ya Wizara *Vote 51* sijui kuna sababu gani?

Nilikuwa naangalia hapo hapo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ziko idara ndogo ndogo lakini zina *vote* kwa mfano Serikalini kuna Mahakama ya ardhi ina vote yake. Kuna ndugu zetu wa Redio Tanzania wana *Vote, Anti Drugs* wana *Vote,* wakimbizi wana *Vote* yao, lakini idara ya uhamiaji kwa nini wamekosa vote yao? Nilikuwa naiomba Serikali sasa umefika wakati ndugu zetu hawa wa Idara ya Uhamiaji wawe na vote yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo katika Idara ya Uhamiaji nataka niulize kuna Afisa mmoja amehamishwa Zanzibara akapelekwa Kilimanjaro, Afisa huyu ndiyo alikuwa Kiongozi wa Idara ya Uhamiaji, lakini mke wake pale Zanzibar ni Katibu Mkuu wa Wizara. Sasa huwezi ukamhamisha yule mama kwenda Kilimanjaro wala huyu Afisa. Sasa kwa nini huyu kijana amepelekwa mbali kutenganishwa na familia yake? Kuna msingi gani? Hivi Mheshimiwa Waziri huyu kijana hawezi kusogezwa karibu na familia yake ili akatumikia taifa hili vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nieleze hilo suala la huyo kijana nadhani Mheshimiwa Waziri atalitafuta vizuri atanielewa na atamwelewa ni nani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, ikiwa leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia tangu kuingia katika Bunge hili.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ina mwelekeo mzuri ambayo italeta mafanikio. Vile vile nawapongeza Wabunge wote tuliowakuta kwa mapokezi yenu mazuri kwa hiyo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nielekee katika mchango wangu, kwanza nitazungumzia kuhusu suala la polisi. Kwa kweli polisi ni vijana ambao tuna ushirikiano wa pamoja katika nyanja zote. Kwa hiyo, wanastahili kupewa sifa kwa kazi zao nzuri. Lakini pamoja na kazi nzuri nahisi ingelikuwa ni vizuri wapewa taaluma nzuri kuhusu haki za binadamu kwa sababu kule Zanzibar ni wakulima wazuri wa karafuu na ndiyo tegemeo la kuondokana na matatizo yetu pale inafika wakati wa kuvuna mazao. Hata Serikali inategemea zao hilo.

Kwa hiyo, asili yetu kule Zanzibar sisemi kwamba ni maskini lakini inapofikia kipindi kama hiki hutegemea sana karafuu. Sasa inafikia kipindi tayari mtu kashatayarisha mali yake kwa ajili ya akiba kwa sababu hawezi kuuza mali yote kwa sababu maisha yake ni ya kubahatisha wanakuja askari wanavamia nyumba wanachukua mali kwa kisingizio kwamba tumekamata mali inataka kusafirishwa kwa njia ya magendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki si kitendo kizuri wakati mwingine. Anapofanya hivi wananchi wanakosa imani kati ya raia na askari. Sisi tunategemea askari wawe ndiyo walinzi wetu, wawe ndiyo marafiki zetu, ili kuwapa taarifa ambazo tunaziona siyo nzuri. Kwa hiyo, wanavyofanya hivyo tayari raia kashajenga imani mbaya na askari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunaomba Jeshi lako la Polisi uwape elimu kidogo kuhusu haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, jingine ni kuhusu ajira za polisi. Kwa kweli raia wote katika nchi hii wanayo haki ya kuajiriwa wanapokuwa na sifa inapotokea wakati wa ajira atakayekuwa na sifa akitaka ile kazi aombe na ikithibitika kwamba anazo sifa aweze kuajiriwa. Lakini nashangaa kusikia Mheshimiwa mmoja anasema ajira zote zielekezwe upande wa CCM kwa sababu hawa wengine wanaweza wakaleta matatizo.

Hilo siyo jambo zuri kwa sababu hujui nani ataleta matatizo. Yeyote anaweza akaleta matatizo, huwezi ukajua imani ya mtu na yeyote anayekubali kuingia katika Jeshi kakubali kuilinda nchi, hakukubali kumlinda mtu fulani, anayo haki ya kuzuia lolote baya ambalo analiona ni baya, lenye madhara na nchi yake ni lazima adhibiti. Kwa hiyo, ukisema kwamba lazima uajiri upande fulani itaonekana kwamba pengine una kitu katika moyo wako na siyo inavyotakiwa. Inatakiwa kila mwenye sifa, Mtanzania aombe aajiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kambi ya *FFU* iliyoko Finya Pemba, ile kambi ina muda mrefu sasa hivi si kambi ya kuzuka tu juzi au jana. Lakini ukiangalia hali ya kambi ile ni mbaya kabisa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba haikuweza kuendelezwa kwa sababu ya madeni. Inaonyesha kwamba kuna madeni mengi na katika mwelekeo wa Bajeti tuliyonayo tunakusudia kuendeleza ujenzi ule.

Lakini hatujajua kwamba hayo madeni yameisha au bado na hii bajeti tutakuja kulipia hayo hayo madeni. Kwa hiyo labda Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up* atueleze kwamba madeni hakuna tena kwa hiyo tutaendeleza kujenzi kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika ripoti ya kamati hii inayoambatana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imezungumzia kwamba ni vizuri askari wakalala katika makambi. Hata mimi nakubali askari walale katika makambi kwa sababu askari wakati wote inapotokea dharura katika nchi wanatakiwa wapatikane kwa urahisi, inapotokea fujo waende wakazuie fujo hususan askari wa *FFU* naona ndiyo tegemea kubwa sana katika kuzuia fujo.

Lakini leo pale Finya hata ukimwambia askari akakale pale hana sehemu ya kulala, bado kumekusanywa matofali, pana mabanda mawili, matatu hiyo kambi ina zaidi ya miaka 10 inaendelea kujengwa tu, hatujui lini itakuwa na sifa angalau askari 20 walale pale.

Kwa hiyo, hilo ni jambo gumu. Sasa hivi ukipita wakati wa asubuhi utaona msululu wa askari wanatoka sehemu mbalimbali si chini ya kilometa tano ambako huwa wanalala wanakuja kazini. Kwa hiyo, hali siyo nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, inaweza ikatokea dharura wanatafutwa askari, majumbani wakatafutwe mmoja mmoja hawaonekani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili alione kwamba ipo haja ya kujenga haraka pamoja na kuwa kuna madeni lakini aendelee na ujenzi mdogo mdogo wa hizi kambi angalau zifikie katika hatua ya kwamba wale askari wetu waweze kukaa pale.

Mheshimiwa Spika, halafu si vizuri askari kukaa katika mitaa wanagongana huyu na huyu na raia, askari anaweza kuwa na chuki na mtu fulani ikawa ndiyo sababu, kwa sababu nyumba hii na hii kama kuna chuki anaweza akamtafutia sababu ya kumhujumu. Lakini atakapokuwa katika kambi hizo dhana zinaweza zikaondoka na kukawa kuna imani nzuri kati ya askari na raia. Ikiwa kuna kubadilishana mawazo yanapotokea matukio siyo ya kuridhisha ataweza kuwasiliana na askari na kumweleza na hilo ndiyo lengo la raia wema na askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hii kero ya majambazi. Askari wanajitahidi kudhibiti majambazi lakini bado, sababu kubwa imekuwa ni kutokujulikana Mtanzania ni yupi na mgeni ni yupi. Hii itajulikana tutakapokuwa na vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, hivi leo mimi ukiniambia alama ya kuwa ni Mtanzania sina kwa sababu sina kitambulisho na wengine watakuwa hawana hivyo vitambulisho. Lakini tutakapokuwa na vitambulisho tutakuwa tunajua huyu ni Mtanzania au siyo. Kwa mfano nchi jirani ya Kenya ukifika tu kama huna kitambulisho ujue siku hiyo utalala ndani.

Lakini sisi wanaingia wageni tunaishi nao tunashirikiana nao hata ukilinganisha kwamba mipakani wale watu wanaingiliana sana, pengine kabila hili liko huku na huku, wanazungumza lugha moja, wanafahamiana sura zao ni moja. Huwezi kujua kwamba

huyu ni Mtanzania au huyu si Mtanzania. Kwa hiyo, wana fursa pale ya kuingia na kufanya hujuma ambazo wamekusudia.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hili suala la vitambulisho ilione kwamba ni kitu muhimu sana. Lingine ni kuhusu suala la rushwa kwa askari wetu. Hili inawezekana lipo na lipo kwa sababu moja, kulinganisha na hali ya maisha, hali ya mishahara yao na mafao yao hayakidhi mahitaji yao. Mshahara unakuwa ni mdogo kuliko matumizi yake au mafao yake ya nyumbani. Mfano, askari pengine ana watoto wanasoma, huduma zote zinatokana na mshahara ule ule, kuna matibabu, sasa utaona haitoshi, hata utastukia pengine askari afanya kazi ambayo haifanani na yeye. Anafanya biashara za mkononi, mitaani au kule kwetu pengine utamwona askari kabeba gunia la mkaa anaenda kuuza. Kwa hiyo, hii siyo heshima ya mtu kama huyu ambaye tunataka sisi atulinde afanye kazi kama hizo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara kwamba iwaangalie askari wetu ili awe askari wazuri, waweze kufanya kazi ambayo tumewatuma, wasifanye kazi ambazo kwamba hazifanani na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG’ONG’O:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi nami kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri na ya uchambuzi wa kina. Naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu na Makamishna wote na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa juhudi ambazo wamekuwa wanafanya, Wizara inafanya kazi kubwa sana, kulinda amani na usalama wa raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niitumie nafasi hii kumpongeza *RPC* wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kazi nzuri anayoifanya. Wote tunaelewa, Jiji lile ni kubwa na kesi za majambazi ni nyingi, lakini anakuwa anakuwa anajitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na amani.

Napenda pia niipongeze Idara ya Upelelezi kwa sababu bila Idara ya Upelelezi kufanya kazi nzuri hata hayo mengine tunayoyasema yanaweza yasifanikiwe. Nampongeza Mkuu wa Idara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nizungumzie Jeshi la Polisi. Ninaanza na suala la pale unapokuwa na matatizo au una malalamiko. Unapokwenda kwenye Kituo cha Polisi. Kituo cha Polisi kina sehemu ya mapokezi. Lakini yale mapokezi yanakuwa ya ujumla. Nafikiri sasa ni wakati umefika wa kuhakikisha kwamba tuangalie matatizo kwa undani. Inakuwa ni vigumu sana kesi nyingine kwenda kuripotiwa pale Polisi. Matukio mengine yanakuwa ni vigumu, kwa mfano matukio ya ubakaji, mtu anakwenda pale, lile benchi la mapokezi liko wazi, wako watu wengi. Anashindwa kujieleza.

Nafikiri sasa Wizara iangalie kuweka Kitengo Maalum ambacho matukio kama haya yanaweza kuripotiwa kwa faragha ili watu wengi waweze kujitokeza kwenda kusema na pia ningeshauri Wizara ianze utaratibu wa kufundisha askari polisi masuala ya ushauri nasaha wanapopokea kesi kama hizi basi wawe na lugha nzuri ya kuweza kuwavutia mtu kuweza kutoa matukio yale. Kwa sababu ukifika pale kuko wazi mtu anaingia unaulizwa ehee, shida yako ni nini?

Sasa pale, kaa hapo. Lugha hiyo ambayo mtu mwingine sasa kwa vile lile suala anaona hata haya kulisema, hataki mtu mwingine asikie. Hana mahala anapoweza kulisemea. Kwa hiyo, hapa ataambiwa basi, kama wewe husemi, mwingine! Ni kwa sababu wapo wengi, yanakuwa matukio ni mengi na muda wa kusikiliza haupo. Kwa hiyo, nafikiri ya kwamba Wizara itazame sasa utaratibu wa kuwa na Kitengo Maalum ambapo kesi kama hizo wanaweza wakaenda wakaandikisha kwa pembeni kidogo mtu akawa na nafasi kujieleza.

Mheshimiwa Spika, pia liangaliwe suala la watoto. Sehemu zingine nchi nyingine, kuna sehemu ukifika pale Polisi kuna mahala wameweka, yawezekana chumba tofauti au hata kontena tu limetengenezwa vizuri ambako matukio kama yanayoweza kuwapata watoto wanaweza kwenda ndani wakajieleza. Sasa tuanze pia kuwafundisha mapolisi wale sehemu ya mapokezi kuweza kuhojiana na watoto, kuwa na lugha ambayo watoto wanaweza wakasikilizwa. Hili linaendana na kesi za ubakaji nilizozizungumzia kwamba iwepo sehemu ambapo watoto wanaweza wakaeleza matatizo yao badala ya kuwa wazi.

Baada ya kusema hayo naomba nizungumzie Magereza. Kama wenzangu walivyozungumza hali ya magereza yetu sio nzuri na asubuhi Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu amekiri pia mlundikano wa mahabusu. Lakini suala la magereza linakuja pia kuangalia haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuna magereza mengine ambayo yapo kwenye maeneo ya baridi. Maeneo kama ya Makete, maeneo kama Kilolo kule. Hawa wafungwa wana nguo, yaani kinguo chepesi kabisa, hata haiangalii ni majira gani, ni wakati gani wa msimu wa mwaka, wakati wa baridi, hawana hata nguo za kujihifadhi kwa ajili ya baridi. Hata sehemu wanazolala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia tuangalie mazingira kama hayo, wapewe nafasi ile ya kuweza kupata nguo za kujikinga na baridi na tunazungumzia masuala ya haki za binadamu. Kukosea au makosa waliofanya haina maana sasa hata saa nyingine wakose zile haki za binadamu, haki zile za msingi. Kwa sababu kama wataugua vifua ina maana pia itakuwa gharama kwa Serikali kwenda kuwatibu.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba Serikali ianze kuangalia wafungwa au magereza kwa mahala ambapo gereza lipo, kama gereza liko kwenye sehemu ambayo ina mazingira tofauti basi pia wafungwa waangaliwe kwa njia hiyo ili pia waweze kupata hifadhi ya kuweza kupata nguo na mablanketi ya kutosha kwa ajili ya kujihifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia kwenye magereza wale wafungwa wanawake wenye watoto. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa msamaha alioutoa wakati wa maadhimisho ya miaka 42 ya Uhuru alipowasamehe wafungwa wakiwemo wanawake wenye watoto na wajawazito. *(Makofi)*

Nina uhakika kwa huruma yake ataendelea kuwasamehe na kuwatoa hao. Ninazungumzia hilo kwa sababu watoto hawa ningekuwa nafikiria Wizara iangalie pia kuweka vituo vya kulelea wadogo. Nina hakika waliokosa ni wale mama zao. Lakini hawa watoto hawakukosa. Kwa hiyo, uwepo utaratibu wa kuhakikisha kwamba hawa watoto wanakuwa na vituo na wanapata lishe bora ya kuweza kuwalinda afya zao. Wanawake hawakupata haki sawa na watoto wengine, wazazi wao kuwa gerezani sio kwamba na wenyewe wapate adhabu ambayo wazazi wao wanaipata.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba Wizara iangalie utaratibu wa kuwa na vituo na kuhakikisha kwamba hawa watoto afya zao zinalindwa nikizingatia pia kama nilivyozungumzia mavazi na chakula bora na hii pia ni pamoja na wafungwa wakina mama wajawazito, waweze pia kupata huduma muhimu wanazostahili kupata ikiwa pamoja na chakula bora na elimu ambayo pia wanaweza kuipata kama wakina mama wengine wanaokwenda kuhudhuria *clinic.* Kwa sababu hawana muda wa kutosha kuweza kupata, basi magereza yafanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanapata elimu pale walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nipongeze jeshi la polisi kwa mafunzo wanayoyatoa au pamoja na magereza, hasa elimu inayotolewa, elimu ya masuala ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuishauri Wizara kwamba elimu wanayotoa hapa wametuelezea kwamba wameshatoa kwa wale maafisa wa ngazi ya juu sasa wanaenda kwa ngazi ya chini wakiwemo askari polisi na Idara nyingine zote. Sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba sasa wakati umefika hasa upande wa magereza, elimu itolewe lakini wafungwa wapewe elimu hii.

Mheshimiwa Spika, kama wafungwa hawatapewa elimu hii ikaishia kwa wale askari, wafungwa wasipewe elimu, wote tunajua vitendo vinavyotendeka kule magerezani na tunajua kwamba baada ya muda hawa wafungwa wataruhusiwa kwenda uraiani na tunajua pia kwamba hawa wafungwa kama ni wanawake au wanaume wengine wameoa au wengine wameolewa huko wameacha familia zao.

Kwa hiyo, kama hii elimu hawataipata tunaweza pia tukajikuta kwamba tatizo linaendelea kuwa kubwa. Sasa mimi nilikuwa naishauri Wizara kwamba itoe elimu kwa makundi yote kwa askari lakini pia iende mpaka kwa wafungwa na nina uhakika Mheshimiwa Waziri hili atalizingatia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia pamoja na elimu hii pia kuwepo na kitengo maalum cha masuala ya jinsia. Kitengo hiki kikiwa upande wa Wizara tu, kwamba pale

Wizarani kuna *desk* la masuala ya jinsia. Iwe kila Idara, Idara ya Magereza, Idara ya Polisi, Idara zote. Idara ya Uhamiaji, wote wawe na vitengo vya namna hii ili kuhakikisha kwamba masuala ya jinsia yanaingizwa na kama masuala ya jinsia hayapo ndiyo matatizo yanapoanzia hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba hivi vitengo vyote viwepo. Lakini visiwe upande wa Wizara tu. Pia viwe mpaka upande wa Idara zote zinazohusika. Naomba nizungumzie pia nyumba za askari na nyumba za Polisi. Nashukuru kwamba Wizara ina mpango wa kujenga nyumba. Lakini mimi nilikuwa nafikiria kwamba pamoja na kwamba tunafikiria kuwaweka polisi wote kambini, kama wenzangu walivyosema pia wakaangalie nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, polisi ana nyumba ya chumba kimoja na sebule, ana watoto wa kike na wa kiume. Hivi kweli maadili hayo ya Kitanzania tunayofundisha watoto yanakuwaje Mheshimiwa Spika? Hawa watoto wa kike wanalala wapi na hawa watoto wa kiume wanalala wapi? Kwenye chumba kimoja?

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria pia pamoja na kuangalia kuwarudisha vituoni pia tuangalie nyumba wanazoishi. Nyumba zimechakaa lakini pia vyumba ni vidogo kwa wale wenye familia. Kwa hiyo, tuanze pia kulitazama upya na kwa utaratibu ambao Serikali inafanya huu nzuri wa kujenga nyumba kujengea watumishi, basi na Wizara hii pia iwe na utaratibu huo. Kwa vile imeshaanza kufanya kazi kama hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kuongelea suala la haki za binadamu. Napongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo wamefanya kutoa mafunzo kwa maafisa wake kwenye masuala ya haki za binadamu na haya mafunzo mimi ningeshauri yafike mpaka chini kwa wale askari wa kawaida ili haki za binadamu ziweze kutendeka na hasa pale wanapomkamata mtu kabla ya hawajamhukumu kama ni mhalifu basi atendewe haki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia. Lakini vile vile kama ulivyozungumza kwamba mimi na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, tulikuwa tumo katika orodha ya kesho na ni kweli kwa sababu tuliona pale nje. Lakini kwa sababu mimi na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, wastahimilivu na Waswahili wanasema: "Mstahimilivu hula mbivu." Kwa hiyo, tumeshakula mbivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri ambayo wameitayarisha na vile vile walivyoeleza baadhi ya malengo ambayo wameyatekeleza katika kipindi cha mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, inatia moyo sana. Mimi kwa upande wangu kabla sijaendelea naiunga mkono hoja hii mia kwa mia na nasema hayo kwa sababu vile vile

hata ukiangalia hawa Watendaji yaani Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni watu wenye mashirikiano mazuri na ukweli ni watendaji wanaofanya yao pamoja na wengine na nasema hayo kwa sababu sisi Warabu wa Pemba tunajuana kwa vilemba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuchangia kwa kusema kwamba naanzia kwenye operesheni ya majambazi. Kipindi cha miaka miwili mitatu ya nyuma Waheshimiwa Wabunge wote hapa ilikuwa kelele zao kuhusu suala la ujambazi nchini. Lakini kwa bahati nzuri mwaka huu tumeanza vyema. Jeshi la Polisi limefanya jitihada zake ya oparesheni maalum kwa ajili ya majambazi na jitihada zao zimezaa matunda mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya kazi yote hii nzuri ambayo inafanywa na Jeshi la Polisi, lazima Serikali ione baadhi ya mambo ambayo bado ni tatizo, mambo ambayo ni vikwazo kwa wao na siku zote tutakuwa humu Bungeni tunapiga kelele kuwalaumu na kuwahujumu kwa matatizo ambayo siyo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majambazi wana mbinu nyingi. Majambazi hawaendi kufanya ujambazi kama wana gari aina ya *Hyundai,* wanachukua gari ambazo wana hakika ni gari yenye kwenda kwa *speed* kubwa, yenye uwezo kufanya ujambazi na wakakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu nyuma tulipiga kelele hapa, kwa kupiga kelele kwa nini tukasema kwamba ununuzi wa gari za *Hyundai* hauwendani na wakati kabisa. Lakini matokeo yake gari za *Hyundai* zikanunuliwa kwa wingi kabisa, sijui zilitolewa bure gari zile, sijui watu walikuwa wanapata chau mle ndani ya magari yale. Lakini ukweli hazilingani kabisa kuwa gari zile zifanyiwe kazi na Polisi wetu. Mimi naomba Polisi wapewe gari zenye uwezo.

Mtu ameshaiba gari au ameishaiba pesa benki, anaifukuza kwa *Hyundai.* Mimi nitatoa mfano, nilikuwa na jirani yangu hapo zamani wakati ambapo nilikuwa na umri wa miaka 20 alikuwa na punda Kirongwe. Kule kwetu Unguja punda Kirongwe anakuwa hana speed ya kwenda. Sasa akaenda kwa babu yangu. Babu ni mtu wa mikasa mikasa hivi, sasa yule bwana alipotaka ushauri punda wangu haendi. Akamwambia: "Sikiliza bwana, tatizo liko dogo tu kabisa, chukua pilipili hoho, pilipili hoho kwetu sisi ni zile kichaa zile, kali kabisa, ndogo ndogo." Akamwambia chukua aina mbili, aina mbichi na mbivu. Sasa wewe ukimwona umeshamkalia juu mnakwenda haendi, isugue ile pilipili mbichi mtie machoni, ukimtia machoni atakwenda *speed hundred.* Akamwambia kama ukiona haitoshi *speed* ile msugulie pilipili nyekundu yaani ile *speed 200."* *(Kicheko)*

Baada ya kukaa juu ya punda akaona haendi, akaisugua ile pilipili hoho ya kijani ile mbichi akamsugulia nayo. Yule akaruka, kwa sababu pilipili inamwasha, akaruka yule bwana akaanguka chini akabakia na kamba, akawa anaburutwa. Sasa akaona nitampata vipi mie punda wangu huyu. Akaichukua pilipili hoho nyekundu akajisugulia yeye ndani ya macho yake. Haa, matokeo yake kagalauka pale chali, hawezi kwenda, punda kakimbia. Sasa na askari watakuwa hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vi-*Hyundai* haviendi hivi namwomba Mheshimiwa Waziri safari hii afanye jitihada zake afanye kazi nzuri sana. Vile vile kuhusu magari haya kuna baadhi ya Wilaya, hizi Wilaya mpya zilizokubaliwa na Mheshimiwa Rais kwamba ziwe Wilaya. Natoa mfano wa Wilaya moja tu, Wilaya ya Kilolo, Jimbo la Mheshimiwa Mwamoto. Hawa watu wa eneo hili wana tabia ya kujinyonga kwa ajili ya mapenzi. *(Kicheko/Makofi)*

Maiti inakaa siku nyingi haifiki hospitali kwa sababu hakuna gari la kuwabebea. Kwa kupitia Bunge hili Tukufu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, baada ya Bunge hili, afanye juhudi zake zote kama alivyofanya Unguja Ukuu, Mheshimiwa Naibu Waziri, anajua. Unguja Ukuu nilitamka hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri, alishughulikia akawapelekea gari, sasa na Kilolo awapelekee gari pale, waache kujinyonga nyonga ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia habari za Uhamiaji. Katika hotuba ya mwanzo nilipoingia Bungeni hapa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 1996 katika mchango wangu nilizungumzia suala la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Kusini na nilizungumza kwa jazba kwa sababu wakati ule walikuwa wakikaa ndani ya banda la kuku ndiyo wakifanyia kazi za Uhamiaji. Tuliahidiwa sana hapa muda wote, wakasema hawana kiwanja. Serikali ya Mkoa wa Kusini imewapatia kiwanja na nadhani ningemwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake wafuate mfano wako.Walipoona kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibari bado haijajibu kuhusu suala la kiwanja eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar ulikuja mwenyewe. *(Makofi)*

Tena hukuja wewe peke yako, ukaja na Mwenyekiti wa *UWT* wa CCM ukaja naye pale. Nilikupongeza sana kwa sababu umekuja naye yeye ili mshauriane na mliposhauriana, mama akasema kiwanja kidogo. Wewe mwenyewe ukaenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, ukaomba kiwanja kiongezwe. Nasema kimeshaongezwa na umeshatuahidi kwamba pesa ziko tayari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naye aende akashughulikie kiwanja na fedha atutamkie hapa, fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Kusini Unguja, itakuwa ni aibu sana miaka saba tunazungumzia suala hili na CCM haina desturi kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia habari ya ongezeko la ajali nchini. Wamezungumzia Waheshimiwa Wabunge mambo mengi kuhusiana na ajali. Mimi nasema kama hatujasimamia vilivyo ajali zitatumaliza. Sisi wenyewe tunashuhudia, tunatoka Dodoma, huwezi kwenda toka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma kabla hujakuta ajali tatu, nne na haziui mtu mmoja, kumi, kumi na nane, sita ndiyo kidogo kabisa.

Nasema watafute rai nyingine. Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake watafute rai. Lakini lingine ambalo ningeliomba vile vile kupitia kwako, hapo zamani nakumbuka tulipokuwa tunasoma sisi, siku ile ya Usalama Barabarani, ukweli ilikuwa skuli zote zilizokuwa ziko karibu na maeneo ya barabara wanaambiwa walimu wa shule waende katika maeneo fulani ili wanafunzi wajue taratibu za kutumia barabara. Sasa hivi

wanafunzi wetu, watoto wetu, wanamalizika kwa kupondwa kwa sababu kwanza wao wenyewe wanapita pande zote mbili. Zamani tulikuwa tukifahamishwa piteni upande mmoja tu wakati wa kwenda na kurudi. Lakini sasa wanatawanyika barabarani, madereva wenyewe vichaa, wameshavuta bangi zao, wanauliwa ovyo. Lakini vile vile sioni sababu kwa kupitia kwako kwa nini kusiwe na taratibu za humu kwenye shule zote zilizokuwa karibu na barabara yakawekwa matuta kwa kuwasalimisha watoto wetu. Watamalizika hawa. Mimi naomba kwa kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili la usalama wa barabarani ili kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, sasa naingia katika nyumba za askari. Mimi nikizungumzia suala la Polisi linanigusa sana kwa sababu mimi mwenyewe nimepitia huko huko. Nilipomaliza shule kazi yangu ya mwanzo nimeingia Polisi. Ninajua matatizo ya Polisi, ninajua adha ya kazi ya Polisi. Polisi siku 7 anakwenda kukaa doria kumlinda bwana mkubwa, mkewe huko hana mlinzi yuko pekee. Lakini anafanya kazi kwa wema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pale anaporudi apate pahala pazuri pa kulala. Nitatoa mfano wa nyumba za aina mbili Vituo viwili. Nyumba zilizokuwepo katika Kituo cha Polisi Mwera zimejengwa baadhi yake vimejengwa kabla ya mwaka 1915 na ninasema hivyo nina ushahidi kamili. Kwa sababu katika hizo ndiyo mahala Marehemu Abeid Karume, alisoma darasa la kwanza na la pili. Sasa mpaka leo tumeweka askari mle, mabanda ya kuku sasa yamekuwa mazuri kuliko nyumba za askari? Jamani hii ni aibu kwa nchi iliyoendelea kama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa nyumba nyingine ambazo nashukuru sana na napongeza jeshi, kwani nimesikia tu, sijaenda Chake Chake, wameshaanzisha nyumba mpya. Kwa sababu hizo nyumba za Chake Chake zilizokuwa zikikaliwa na askari huwezi kuamini, nyumba za gorofa, hazina choo juu, hazina choo chini. Unakwenda robo kilomita ndiyo choo. Sasa niambie usiku umebanwa na mkojo, sasa wanaume pale ninapokaa kwa sababu nina ushahidi kamili, mwanamme angalau tukitumia chupa za *juice,* asubuhi tunakwenda kumwaga. Sasa niambie hawa wengine wanatumia nini? *(Kicheko/Makofi)*

Sasa twende na wakati, nyumba za aina hii hazifai. Hata zile wanaweza Mheshimiwa Waziri akazikarabati kwa angalau kuzinyanyua nyanyua upande akajenga vyoo juu jamani. Jamani kweli tunawaheshimu wake zetu? Tunawaheshimu watoto wetu, watoke juu usiku na kitaulo na kikanga wanakwenda chooni robo kilomita? Aibu sana hii. Naona uchungu kabisa na wala haiingii akilini, wakati huu tunazungumza kwamba ni wakati wa sayansi na teknolojia nyumba ya gorofa moja halafu ateremke chini kwenye ngazi, kila mmoja anajua sasa hivi tena mmh, haiwezekani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani yalikuwa yangu ni hayo, isipokuwa la mwisho ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri wakati kilipokuja kufunguliwa Kituo cha Polisi cha Unguja Ukuu katika Jimbo la Koani, katika risala pale alisomewa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa kwamba baada ya Kituo kizuri kama kile tungeliomba tukapata

nyumba kwa ajili ya askari wanaokaa pale. Hakuna nyumba za Polisi karibu, watoke Tunguu ambayo ni maeneo ya mbali kabisa kuja kazini pale. Ukweli ni kwamba wanapata shida sana.

Naomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu sikuona humu, nimepekua pekua sikuona. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho angalau anipe tamaa kwa kuanzia shilingi milioni 500 kwa askari hao. Baada ya kusema hayo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja yake mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa msemaji wa mwisho kwa siku ya leo. Nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa kuongeza Bajeti kuipa Wizara hii ambayo umuhimu wake unafahamika bila usalama mambo mengi hayawezi kufanyika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri. Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa juhudi mnazofanya, tunajua lipo wimbi la ujambazi sasa hivi lakini kazi mnayofanya kwa kweli wananchi wanaiona na wana imani kubwa sana nanyi. *(Makofi)*

Upo umuhimu mkubwa sana wa Serikali kuendelea kuongeza Bajeti hasa Bajeti ya masuala la Maendeleo kwa Wizara hii ili kuweza kujenga nyumba za askari polisi kama Waheshimiwa Wabunge ambavyo wamekuwa wakisema, askari magereza. Maofisi ya askari wetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nataka nianze na moja la jumla kwanza la Serikali nzima kabla sijajaza na masuala ya Wizara hii. Ni kwamba masuala yote ya mipango yetu ya maendeleo kwa ujumla wake sasa hivi tumekuwa na miradi mikubwa mikubwa ambayo inaenda kwa awamu. Sasa nataka nisemee tu kidogo kwa kifupi hili suala la awamu kwamba ni vizuri Serikali ikawa na uratibu wa aina fulani wa kutazama hizi awamu inamahanisha nini. Kwa mfano, mradi mzuri kama *TASAF* uko katika Wilaya chache tu nchini na mwakani utasogea katika Wilaya nyingine chache na hivyo hivyo labda ita-*cover* nchi nzima baada muda sana. Lakini tunao mradi kupitia TAMISEMI wa maboresho, baadhi ya Wilaya na baadhi ya Wilaya ziko na baadhi ya Wilaya hazimo, sasa kwa vile mradi mzuri kama Waziri wa Kilimo na Chakula wa *STABEX* ni vizuri basi mradi huu unapokuja ukaangalia zile Wilaya ambazo hazijaguswa na maeneo yale mengine nazo zikaguswa. Itakuwa sio vizuri Wilaya haina *TASAF* na *TASAF* iko sehemu fulani na *STABEX* nayo ikaenda Wilaya ile ile wakati Wilaya jirani haina mradi kama ile, ni suala la uratibu tu. Nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri kutazama ili miradi yote iwe na impact sehemu za nchi yetu. Nikirudi kwenye Wizara na hasa nikianza na Jimbo langu la Kongwa, tunayo matatizo ya uhalifu wa ujambazi ambao unatokea mara kwa mara katika maeneo ya kuanzia Panda Mbili, Kibaigwa hadi Njia Panda *NARCO* na Mbande kwenye njia ya Morogoro-Dodoma pamekuwa na ujambazi kwa muda mrefu tangu mwaka 2000 ambapo iliwahi kutekwa bus pale wakavuliwa nguo abiria wote, ilikuwa ni jambo la kusikitisha sana na mpaka sasa pamekuwa na matukio ya ujambazi mara kwa mara ambayo yanatokea. Unafahamu hata wale majambazi wa Dar es Salaam juzi walikamatiwa kwenye eneo hilo hilo la Wilaya ya Kongwa. Kwa hiyo, tunayo matatizo halafu ni barabara kuu. Askari ambao wako Makao Makuu ya Wilaya ya Kongwa, wanashindwa kuwa na *response* ya haraka kwa sababu wanayo gari bovu

sana, *OCD* analo gari bovu na kuna uchache mkubwa wa askari. Kwa hiyo, kwa ushauri wangu panahitajika magari mawili, moja liwe stationed pale Kibaigwa kwa ajili ya jambo lolote likitokea. Kwa sababu sasa hivi anayetegemewa ni *RPC* huku kupeleka askari wa doria kila siku. Kwa hiyo, hata gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa sana. Kwa hiyo, pawe *stationed* pale Kibaigwa na ikiwezekana *OCD* na yeye apewe gari ya kuweza kufanyia kazi na pawe na *highway patrol car* ya Polisi ya kuweza kuangalia masuala haya hasa hii ambayo itakuwa *stationed* pale Kibaigwa.

Lakini Kituo cha Kibaigwa hakijaanza kufanya kazi. Wananchi walijitahidi wakajenga Kituo lakini mara ya kwanza wakawa wamejenga kituo kama hivi *Police Post* za mijini kidogo kidogo hivi, Wizara ikashauri hapana, jengeni jengo zuri lenye heshima, kubwa linalofanana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wamejitahidi wananchi wale wamejenga jengo bado kumalizia tu masuala ya madirisha na milango na nini. Sasa kama mnavyojua Mheshimiwa Waziri, kuchangisha kila mara ina ugumu wake. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali ituongezee nguvu ili tumalizie kile Kituo cha Kibaigwa na askari wawe stationed pale pale Kibaigwa kwa kuanzia ili hali ya usalama ya eneo hilo iwe nzuri zaidi na vile vile tumejenga Ofisi ya *OCD* Kongwa sisi wenyewe wananchi, tungeliomba tunapokuwa tunapofanya juhudi hizo basi Serikali nayo ituunge mkono kwa kutusaidia ili tuweze kuchangia zaidi. *(Makofi)*

Kama nilivyosema askari wa Kongwa wanapata matatizo sana kwenda kwenye maeneo ya doria inabidi wategemee *lift* za magari ya raia *lift* ambazo inabidi wapande wakiwa na silaha nzito nzito jambo ambalo si zuri maana yake majambazi wanaweza kupata habari kwamba hawa jamaa wanakuja, ikawa ni vigumu kufanya kazi yao. Kwa hiyo, tunaomba sana suala la gari zima linaloweza kufanya kazi katika Wilaya ya Kongwa litazamwe kwa umuhimu wake na kwa sababu liko gari moja kama nilivyosema na gari yenyewe ni bovu na Wilaya ile ina watu laki mbili na nusu kuwapa gari moja tena bovu itakuwa ni vigumu sana Polisi kuweza kufanya kazi yao vizuri, na ili ma-*OCD* wafanyekazi vizuri kama walivyosema wenzangu ni vizuri mafungu yao yakaenda moja kwa moja kule kule Wilayani ili aweze kufanya kazi yao kama inavyopasa. Kwa sababu sasa hivi kutokana na mafungu haya kukaa mbali unakuta wakati mwingine panapotokea tatizo inabidi Polisi wategemee wananchi kuchangia mafuta dizeli ili waweze kwenda mahali. Wananchi wamewahi kuniuliza je, hii ndiyo sera ya Serikali? Kwa hiyo, turekebisho hilo.

Mheshimiwa Spika, hali ya nyumba za polisi na askari wa magereza Kongwa ni mbaya sana. Tunajua Bajeti ni ndogo, lakini tunasema kwa mwakani muone uwezekano wa kuweza kutusaidia na japo sio Wizara hii lakini ilikuwa imeahidiwa mwaka kwamba Wilaya ya Kongwa ingejengewa Mahakama ya Wilaya kwa sababu ni moja ya Wilaya mpya. Lakini bahati mbaya jambo hilo halikutekelezeka tunaamini kabisa kwamba mwaka huu kwenye Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, litakuwepo suala hilo la kujenga Mahakama ya Wilaya ili kupunguza adha wanayoipata askari polisi na askari magereza kupeleka mahabusu Mpwapwa na kurudi kila wakati, katika usafiri niliouelezea ambao ni sawasawa na haupo. Kwa hiyo, tungeshukuru sana endapo tutapata Mahakama ya Wilaya katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 na mimi naamini kabisa Serikali inashughulikia jambo hilo linakuja.

Lingine la ushauri lilikuwa kwamba nilishawahi kuahidiwa hapa suala *PF3.* Naomba itarekebishwa na sio tu kurekebishwa lakini upatikanaji wake na taratibu zake zitaangaliwa na kuwekwa vizuri ni jambo ambalo ningelishauri sana lifanyiwe kazi kwa haraka iwezekanavyo ili kupunguza usumbufu mkubwa sana ambao wananchi wanaupata na vile vile masuala ya vyeti vya uraia ili mwananchi aweze kupata *passport* linasumbua sana. Ni vizuri taratibu zake nazo zikarekebishwa ili wananchi waweze kupata vyeti vya uraia mapema na kwa haraka kuwawezesha wanaotaka kwenda kusoma maeneo mbalimbali au wanaohitaji kupata kazi wanaopewa masharti ya kwamba lazima waonyeshe vyeti vya kuzaliwa basi wasipate matatizo ya kutoweza kufanikiwa katika majukumu yao hayo. Katika barabara ya Dodoma-Dar es Salaam, Dar es Salaam-Mbeya, Dar es Salaam-Arusha, mtu yeyote anayesafiri katika barabara hizi atakutana na *Traffic* njiani wengi sana ambao baadhi yao wako kwenye maeneo ya kujificha ya vichaka vichaka. Sasa labda wananchi tunashindwa kuelewa ni mbinu za midani za aina hizo na kwa nini askari hawa wajifiche kwenye vichaka nafikiri ni jambo la wazi kabisa hata Katibu Mkuu wakati unakuja huku nasikia umewakuta wengi huko. Tulikuwa tunashauri ni vizuri sana Wizara ikatoa tamko linaloeleweka kuhusiana na masuala haya, maana ujambazi umeongezeka, watu wanaweza kuvaa nguo kama za *Traffic* machakani humo ikawa ni vigumu sana kutofautisha.

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu ulikuwa ni kwamba wakae kwenye vituo ambavyo vinaeleweka au kwenye vijiji au kwenye miji midogo ili shughuli zao ziweze kueleweka katika maeneo yale kuliko kujifichaficha kwenye vichaka jambo ambalo linatilia wasiwasi kwamba labda kuna *insentive* nyingine zaidi ya kufanyakazi za *Traffic. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni msemaji wa mwisho nisingependa kuongea sana, lakini nimalizie tu kwa kuainisha yale mambo ambayo nimeyazungumzia ambayo ni manne. La kwanza nimezungumzia habari ya umuhimu wa Wilaya ya Kongwa kupewa gari ya polisi kwa haraka iwezekanavyo katika mgao wowote ujao wa Wizara hiyo wa magari, la pili, naomba pale na gari maalum la *highway patrol* ambalo litakuwa *stationed* Kongwa badala ya kuwa hapa Dodoma ili kukabili hali hiyo ambayo imejitokeza na ambayo nimeieleza ya ujambazi, la tatu, kuongezewa idadi ya askari na wawe *stationed* Kibaigwa kitu ambacho hakipo kwa sasa inabidi watoke Kongwa kila siku kwenda Kibaigwa na kurudi na maeneo yale, jambo ambalo ni gharama na ni gumu sana kufanyika na mwisho naomba Wizara itusaidie kutuunga mkono wananchi tunapokuwa tunafanya juhudi za kujenga vituo hivi vya Polisi basi itusaidie kwa kutuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema nashukuru sana na naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kazi ya siku ya leo. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa*

*Tarehe 11 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*